# Nipashe

Jumatatu Desemba 26, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581171

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13


SUPA JACKPOT

TZS. 1,059,844,733

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#


RIPOTI MAALUM

**Mizizi** ya moto Kilimanjaro na yanayokwamisha vita vya kuukabili



UKURASA 4



Askofu Dk. Fredrick Shoo



Mchungaji Anthony Mlyashimba



Askofu Issack Amani



Askofu Ludovick Minde

# Maaskofu wakumbusha Katiba Mpya

• **Waonya** viongozi kupenda kusifiwa, kuendekeza rushwa... *Endelea ukurasa 2, 3, 5 & 7*

## YALIYOMO

UKURASA WA 8

### UMMY ATOA ANGALIZO SHEREHE ZA KRISMASI NA MWAKA MPYA



WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amewataka wananchi kuchukua hatua za kujikinga dhidi ya magonjwa ya...

## Viongozi wa dini wataka vibanda umiza vifungwe

UKURASA 7



Waumini wa Kanisa Katoliki la Kristo Mfufuka wilayani Muheza mkoani Tanga wakitoka kanisani baada ya ibada ya Krismasi jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## ...wakemea kukithiri vitendo vya ukatili na malezi mabovu

UKURASA 3

**MICHEZO** SAIDO AWAAHIDI MAKUBWA SIMBA UK.28

**KATUNI** UK.6

# Maaskofu wakumbusha Katiba Mpya

**Na Waandishi Wetu**

MWANGWI wa hitaji la Katiba Mpya, umesikika kwenye baadhi ya nyumba za ibada za Krismasi kwa maaskofu kusema ni muhimu mchakato huo kuharakishwa ili kuwezesha upatikanaji wa haki na kupata viongozi wanaoweza kuwajibishwa na wananchi.

Pia maaskofu na wachungaji wamekemea rushwa kwenye kupata uongozi, ubinafsi uliopita kiasi kwa baadhi ya wateule na wanaosifia marais ili kuficha uovu wao huku wakizuia habari mbaya zisimfikie Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya ibada, kuhusu mwelekeo wa nchi kwa mwaka 2023, Askofu wa Kanisa la Baptisti Jimbo la Dodoma, Antony Mlyashimba, alisema ni muhimu serikali ikaharakisha mchakato wa Katiba Mpya kwa kuwa ni hitaji la muhimu.

Alisema kuwa ili furaha na amani ya kweli izidi kutamalaki ni vyema serikali ione umuhimu wa kurejesha mchakato wa Katiba Mpya kwa kuijadili Rasimu ya Katiba mpya iliyoandaliwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba chini ya uenyekiti wa Jaji Warioba ambayo ina mapendekezo halisi ya wananchi na sio wanasiasa.

"Tunajua Katiba iliyopo imesababisha kuwapo kwa makovu makubwa kwa watu kutokana na jinsi ilivyo, lakini ile rasimu ya Jaji Warioba ilikuwa na mapendekezo mengi na mazuri ya wananchi ambayo kama yangefanyiwa kazi yangeweza kuondoa makovu yaliyosababishwa na Katiba ya sasa," alisema.

Mkuu wa Kanisa la Moravian la Uamsho Tanzania na Afrika Mashariki, Emmaus Mwamakula, aliitaka 2023 iwe ya kudai Katiba Mpya.

"Kwa muono wetu, tatizo la upungufu wa ajira Tanzania linasababishwa na Katiba ambayo haitoi fursa ya kutatua tatizo hilo. Baadhi ya viongozi wanapata au kupewa nafasi za uongozi kwa kigezo cha rushwa, upendeleo na kulipa fedha," alisema.

"Kuzaliwa kwa Yesu Kristo kulitikisa mfumo wa utawala ambao haukuwa rafiki kwa maendeleo ya kiroho na kiuchumi. Mtu ambaye uchumi wake hauko sawa na mtu ambaye haki yake inafinywa hawezi kuzalisha vizuri.

"Kwa sababu hiyo, tunauasa umma kushiriki katika kuleta mapinduzi ya kiuchumi kwa kuwa sehemu ya kudai Katiba Mpya. Krismasi hii itusaidie kuona umuhimu wa kuufanya mwaka 2023 kuwa ni mwaka wa Katiba Mpya."

**RUSHWA YAWAKERA**

Askofu Mlyashimba alikemea viongozi wanaotafuta nafasi kwa kutumia rushwa na kwamba kama haitakemewa kila atakayeingia madarakani atapambana kurejesha alichotumia kushika nafasi husika, huku akiwataka viongozi wa dini kuisaidia serikali kwa kusema ukweli na kukosoa kwa hekima na kupongeza inapofanya vizuri bila kufunikafunika mambo.

"Viongozi wa dini wajibu wetu ni kuhakikisha tunasema kweli kuikosoa serikali kwa hekima pale inapoteleza, lakini na kuipongeza pale inapofanya vizuri sambamba na kuhakikisha inawakemea washirika wake pale wanapokuwa wakijihusisha na matendo maovu yasiyofaa.

"Ili nchi iweze kupona na kustawi katika kweli ni lazima viongozi wa dini wasimame katika nafasi zao na njia zao nyoofu na ili waweze kufanya hivyo ni lazima na wao wawe wamesimama katika kweli ya Mungu pasi na kuchanganya mambo mengine ambayo hayampendezi Mungu," alisema Askofu Mlyashimba.

**UBINAFSI**

Askofu wa Jimbo Kuu la Zanzibar, Augustine Shao, alisema kiongozi yeyote anayejali maslahi ya familia yake pekee ni mbinafsi na hafai kuongoza.

Akihubiri wakati wa Ibada ya Krismasi katika Kanisa Katoliki Minara Miwili Shangani, Zanzibar, alisema viongozi wenye nyadhifa serikalini ni watu wenye mishahara mikubwa na ya kutosheleza mahitaji, lakini kwasababu ya ubinafsi na uroho wa mali wamefanya wengi kuishi katika hali ya shida kubwa ili wao wafaidi.

"Ni hivi majuzi tu, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alipewa taarifa ya uchepushaji maji kwenye Mto wa Ruaha Mkuu. Kitendo hiki kimefanywa na familia 12 za viongozi wanaopaswa kujali na kulinda maslahi ya wengi," alibainisha.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, ni vyema kujifunza kujishusha na kujinyima kwa ajili ya wengi kwasababu hakuna yeyote atakayehitaji ardhi zaidi ya mita mbili mwisho wa safari ya binadamu duniani.

Alivitaka vyombo husika viwawajibishe na kuwachukulia hatua kali viongozi waliohusika na kadhia hiyo ili kitendo kama hicho kisirudiwe.

Alisema agizo la Naibu Waziri kwamba viongozi hao waondoke mara moja ni jepesi mno ikilinganishwa na madhara yaliyofanyika.

"Tunasikia pia kwa ajili ya kulindana Naibu Waziri fulani aliagiza mifugo iliyokamatwa kwasababu ya uharibifu wa mazingira kwenye bonde hilo waachiliwe mara moja. Kwa akili za Watanzania wengi waliositisha shughuli zao za kujipatia kipato kwa sababu ya kukosa nishati, hawawezi kuelewa uwajibikaji wa Naibu Waziri huyo," alisema.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza na waumini wa Parokia ya ya Kristo Mfalme Veyula mkoani Dodoma baada ya kumalizika kwa Ibada ya Misa Takatifu ya Sikukuu ya Krismasi jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

**WANAOSIFIA**

Aliwaasa viongozi wakuu wa nchi kuwa makini na viongozi waliowateua, kwa kuwa wengi wanaowasifia marais kila waendapo ni mbinu ya kuficha uovu wao.

Alisema mabadiliko ya tabianchi Tanzania ni kwasababu ya umaskini wa wananchi wengi kukosa njia mbadala ya nishati na kutegemea misitu ambayo ndiyo kivutio kikubwa cha mvua.

"Nawahimiza viongozi wengi kupanda miti na kuacha kukata miti kungezaa matunda kama serikali zetu zingejizatiti kupunguza bei za gesi na mafuta kwa fidia fulani na kuhimiza wengi kutumia nyenzo hizo," alisema Askofu Shao.

Alisema Watanzania wengi walifurahia waliposikia Tanzania ina gesi asilia na wakawa na matumaini makubwa kwamba kiasi kitatumika nyumbani.

Aliomba serikali zote mbili zitafute uwezekano wa kuchakata gesi ili kutumika nyumbani na ili agizo la kutokata miti na kutumia mkaa litafanikiwa.

"Ujumbe tunaoachiwa katika sherehe hii ni kuwa chombo cha haki na amani kwa maskini na wahitaji ni lazima kila mmoja wetu ahusike na mabadiliko tunayotumainia utunzaji wa mazingira ili tuishi kwa amani."

Alisema licha ya mafanikio mazuri yaliyoko, lakini changamoto za mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira yanadhoofisha amani na furaha ya Watanzania.

**VIONGOZI WAJITATHIMINI**

Askofu wa Kanisa Anglikana Tanzania Dayosisi ya Central Tanganyika, Dk. Dickson Chilongani, amewataka viongozi wa serikali kuitumia Sikukuu ya Krismasi kujitathmini na kubadili mwelekeo katika kuwatumikia wananchi.

Dk. Chilongani alibainisha hayo jana wakati wa mahubiri ya Krismasi iliyofanyika katika Kanisa Kuu la Roho Mtakatifu jijini hapo.

Aliwataka viongozi wa serikali kujitathmini na kubadili mwelekeo katika kuwahudumia wananchi kwenye maeneo yao ya kazi ili kuondoa manung'uniko.

"Nitoe rai kwamba, Krismasi hii viongozi wetu wa serikali wajitathmini, wabadili mwelekeo, watoke katika njia iletayo mauti, wapite katika njia iletayo uzima wavue roho ya Herode, wavae roho ya mtoto Yesu aliyezaliwa," alisema.

"Natambua nia ya Rais wetu ni njema anataka tupite njia iliyo salama, anatamani kutufikisha Bethlehem, lakini huku chini kuna akina Herode, watu wanaolinda vyeo vyao kuliko kuwatumikia wananchi," alisema.

Baadhi ya viongozi hao alisema wamekuwa wakizuia hata habari mbaya zisimfikie mkuu wa nchi ambaye ni Rais Samia Suluhu Hassan.

Kadhalika, alisema kauli za viongozi kupitia hotuba zao zimekuwa zikiwaumiza baadhi ya watu na kusababisha kujichukulia sheria mkononi.

Alishauri Sikukuu ya Krismas iwe sehemu ya kuwakumbusha viongozi hao kuzingatia sheria katika kuwahudumia wananchi.

Kadhalika, kuna matukio ya mauaji yanayotokeza kwenye jamii, lakini wananchi hawapewi taarifa za uhakika kuhusu hali hiyo.

"Mwezi huu mwanzoni Askofu wetu mstaafu Boniface Kwangu wa Dayosisi ya Victoria Nyanza aliuawa lakini hadi leo hatujui kinachoendelea. Ukimya huu ndiyo ambao husababisha wananchi kuchukua hatua mkononi," alisema.

**PAPA FRANCIS**

Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, amelaani njaa ya mali na madaraka ya wanadamu akionekana kurejelea vita vya Ukraine na migogoro mingine na kubainisha kwamba waathirika wakubwa wa migogoro hiyo ni wanyonge na maskini.

Alikuwa akiwahutubia waumini katika Kanisa la St Peter's Jiji la Vatican, katika Misa ya Mkesha wa Krismasi uliofanyika usiku wa kuamkia jana.

"Wakati wanyama wanakula katika mabanda yao, binadamu wanaume na wanawake katika dunia yetu, kwa njaa yao ya mali na madaraka, hula hata majirani zao, mama zao na dada zao," alisema.

***Imeandikwa na Peter Mkwavila, Ibrahimu Joseph na Renatha Msungu (DODOMA), Marco Maduhu, (SHINYANGA), Vitus Audax (MWANZA) na Rahma Suleiman (ZANZIBAR)**

HABARI KITAIFA

# Rais Samia afagiliwa kwa miradi kimkakati

**Na Oscar Assenga,** TANGA

ASKOFU Mkuu wa The Free Pentecostal Church of Tanzania (FPCT), Stevie Mulenga, amesema uwekezaji mkubwa unaofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan katika sekta ya elimu kwenye ujenzi wa madarasa ya shule za msingi na sekondari na miradi mikubwa ya kimkakati ni kielelezo cha uhodari na ushupavu wake.

Amesema kutokana na kazi hizo zinazoleta matokeo chanya kwenye maisha ya Watanzania, Rais Samia anastahili kuungwa mkono ili atekeleze majukumu yake kwa ukamilifu zaidi.

Mulenga aliyasema hayo jana wakati akitoa salamu za Sikukuu ya Krismasi wakati wa ibada iliyofanyika katika Kanisa la (FPCT) Novert, jijini Tanga.

Alisema taifa lolote ili liweze kuendelea linahitaji elimu na maarifa yanayoweza kuwasaidia watu kuchochea maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Alisema serikali inapotekeleza miradi ya kielimu inaiwezesha jamii kuelimika na kupata manufaa makubwa kwa kuwa elimu ndio msingi mkubwa wa mafanikio ya jambo lolote na uwekezaji huo una tija kwa maendeleo.

"Kwa kweli nimpongeze Rais Samia Suluhu na wasaidizi wake hasa kwa uwekezaji wa miradi ya kimkakati inayoendelea hapa nchini, lakini kubwa zaidi ni sekta ya elimu ambayo kwa hakika ina umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya nchi na taifa lolote. Ili liweze kuendelea linahitaji elimu kwanza," alisema.



Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la KKKT Usharika wa Muheza mkoani Tanga, John Ndimbo (kulia), akiwatakia mkono wa baraka ya heri ya Krismasi waumini wa kanisa hilo jana katika ibada ya Krismasi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# ...wakemea kukithiri ulawiti, malezi mabovu

**Na Waandishi Wetu**

VIONGOZI wa dini wamekemea unywaji pombe uliokithiri kwa vijana na ukatili dhidi ya watoto hasa ulawiti kinyume na mafundisho ya dini, huku wakiwataka wazazi kutimiza wajibu wa malezi kama walivyopewa na Mungu.

Vile vile, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema ukatili dhidi ya watoto nchini umekithiri, kunahitajika ushirikiano wa jamii kukomesha matukio hayo ambayo ni kinyume na upendo wa Mungu.

Viongozi hao walitoa wito huo kwa nyakati tofauti wakati wa ibada ya mkesha na Sikukuu ya Krismasi ambayo waumini wa kikirsto duniani wanaungana kukumbuka siku ya kuzaliwa Yesu Kirsto zaidi ya miaka 2000 iliyopita.

**POMBE KWA VIJANA**

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amekemea kundi kubwa la vijana wenye umri mdogo chini ya miaka 25, kuanza matumizi ya kunywa pombe kali kupita kiasi huku akitahadharisha wanaoendekeza ulevi wa aina hiyo wasiratajie 'kutoboa' miaka 50.

Askofu Dk. Shoo, ambaye ni Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini, alitoa onyo hilo jana wakati wa ibada ya Krismasi iliyofanyika Kanisa Kuu la Usharika wa Moshi Mjini.

"Kijana wa miaka 25 umri mdogo tu anakunywa pombe kali sana na wanafikiria eti yaani huo ndio mtindo, kama unataka kuonekana wa kisasa. Pombe kali, sio bia hii zenye saba sijui point (kiwango cha ulevi) ngapi (alcohol). Kweli vijana nawaonya, nimeona kuna trend (mwenendo) hii ni hatari sana," alisema na kuongeza:

"Unaanza kunywa pombe kali Whisky zenye asilimia, huwa ni ngapi? (waumini wanaangua kicheko), najua ni 48. Unaanza na miaka 25. Nakuhakikishia ukiendelea hivyo hutafikisha miaka 50, ini litakuwa limekwisha."

Askofu Shoo alisema: "Kwa hiyo vijana nawaombeni kunyweni, kuleni lakini tuwe na kiasi na kwa hiyo ya 'percent' (asilimia) ya kilevi. Nawaomba, nawaonya acheni vijana kutumia pombe kali.

**KUKITHIRI UKATILI**

Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Arusha, Askofu Isaack Amani, aliwataka Watanzania kupinga vitendo vya ulawiti ambao ni matendo ya kishetani huku akiwakumbusha kwa kufanya hivyo ni kutofautiana na maadili ya kidini.

Kiongozi huyo alitoa wito huo wakati wa mahubiri kwenye ibada ya misa ya mkesha wa Sikukuu ya Krismasi iliyofanyika Kanisa la Mtakatifu Theresia wa Mtoto Yesu, jijini Arusha.

Alisema baadhi ya watu wamejiingiza kwenye vitendo vya ulawiti, ambavyo ni vya kinyume cha maadili ya Mtanzania, pia ni dhambi na laana kwa Mwenyezi Mungu.

"Watu wamekuwa vituko sijui wameiga wapi tabia hii ya ajabu, mbona hata fisi na wanyama wa porini hawafanyi tabia kama hizi, tunatafuta laana za bure tu, tuishi kadiri ya mpango wa Mungu na maelekezo yake. Yesu azaliwe leo kwa watu wenye tabia hii na waache," alisema.

Aidha, alisema vitendo vya ulawiti, vimekuwa vikitendwa kwa watoto wadogo ambao hawana hatia yoyote.

"Tuwe makini na ndugu tunaowakaribisha, sio ndugu anafika nyumbani kwako analala na watoto, hapana tuwe makini, ndugu wa karibu unaweza usifikirie kufanya jambo baya kiasi hicho, tuwe makini na tulinde watoto wetu, mpaka watakapojitegemea," alisisitiza Askofu Amani.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alisisitiza Watanzania kutunza heshima dhidi ya watoto na kwamba haipendezi kuendelea kusikia dhuluma inayofanywa na watu wazima, huku akiwataka kutubu kwa dhambi hiyo na kutimiza wajibu wa malezi ikiwamo kuwapa elimu.

Dk. Mpango aliyasema hayo jana wakati akitoa salamu za sikukuu kwa waumini baada ya kushiriki Ibada ya Misa Takatifu ya Krismasi katika Parokia ya Kristo Mfalme, Veyula mkoani Dodoma.

"Tunasikia mambo ya ovyo sana, dhuluma dhidi ya watoto wanaonyanyaswa sana, wanauawa, kuna ulawiti wa watoto wetu. Tumuombe Mungu msamaha na atujalie neema ya kutambua jinsia yeye alivyowapenda watoto na sisi tufanye mengi ya kuwatunza hawa watoto na kumrudishia Mungu wakiwa weupe

kama tunavyoweka ishara ya kitambaa cheupe," alisema.

Vile vile, aliwataka Watanzania kumshukuru Mungu kwa mvua na kwamba hali ilikuwa ngumu kutokana na ukame na sehemu nyingine mifugo ilianza kufa huku akiwataka waitumie vyema kupanda mazao kupata chakula.

"Kila familia ipande miti mitatu, miwili ya matunda na mmoja wa kivuli. Hali ni mbaya sana maeneo mbalimbali, nchi yetu imeharibika sana, tukipanda miti neema ya Mungu itashuka juu yetu.

**WAZAZI**

Askofu wa Jimbo Katoliki la Moshi, Ludrovick Minde, amezungumzia utamaduni wa sasa wa wazazi wengi kuacha jukumu la malezi ya vijana na kutumia muda mwingi kutafuta pesa au kuwekeza miradi inayowabana muda wao kwamba wanapanda mbegu ya uovu.

Akihubiri kwenye misa ya mkesha wa Krismasi, Askofu Minde, alisema ni jambo la kumiza, kama wazazi watawekeza zaidi kwenye utafutaji na kuacha kwenye malezi ya makuzi.

"Tutakuwa tunapanda mbegu ya uovu itakayozaa matunda na kutuumiza wenyewe. Ni jambo la kusikitika sana, vijana wa sasa wamekuwa tishio katika kufanya matendo maovu, na hii ni kutokana na wazazi kushindwa kusimamia malezi yao na kuwaacha watoto hao kujilea wenyewe.

"Huko wamekutana na uovu mwingi na wameshindwa kuchagua lipi jema na lipi baya. Umefika wakati wazazi kurudi na kufanya marekebisho ili kukomboa taifa na kizazi hiki."

**UTOAJI MIMBA**

Askofu wa Jimbo Katoliki Kahama, Christopher Ndizeye, amekemea vitendo vya utoaji wa mimba kwa mabinti na wanawake kwamba kufanya hivyo hakuna tofauti na mtu aliyefanya mauaji.

Alisema hakuna mwanadamu yeyote mwenye mamlaka ya kuua na kuwataka wajifunze kulinda uhai wa watoto wawapo tumboni.

Alisema kila anayebeba ujauzito anatakiwa kumpatia nafasi mtoto aliyeko tumboni kuzaliwa salama atapofikisha umri wa kuzaliwa, ikiwa ni pamoja na kumpatia malezi mema na kukuza kipawa chake alichopewa na Mungu wakati wa ukuaji wake.

Aidha, Ndizeye alisema wazazi wana wajibu wa kuwalea watoto wao katika misingi mizuri hususani ya kiimani na mtoto anapolelewa na mzazi wa upande mmoja anakuwa na akili za upande huo na kwamba jukumu la malezi ni la wazazi wote.

"Tujifunze kulinda uhai wa watoto, tuwapatie nafasi ya kuzaliwa salama pale muda wake unapowadia na baada ya kujifungua na kulea tuhakikishe tunawapeleka shuleni kwani ni haki yao kwa sababu hakuna anayetambua mtoto aliyemzaa atakuja kuwa na nani hapo baadaye," alisema Ndizeye.

Alisema wazazi wengi wamewageuza watoto wao kuwa yatima kwa kuwapeleka shule za kutwa wakati wakiwa na umri wa uangalizi wa wazazi na kwamba mtoto anayeweza kukaa mbali na wazazi ni mwenye umri wa miaka 10 na kuendelea.

***Imeandikwa na Godfrey Mushi (MOSHI), Daniel Sabuni (ARUSHA), Mary Mosha (MOSHI) na Shaban Njia, (KAHAMA).**

RIPOTI MAALUM

# Mizizi ya moto hifadhini Kilimanjaro na yanayokwamisha vita vya kuukabili

**Na Mwandishi Wetu, aliyekuwa** MOSHI

NI vigumu kuuzungumzia uchumi wa Tanzania pasi na kuitaja Sekta ya Utalii. Kwa mujibu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, sekta hiyo inachangia asilimia 17.5 ya Pato la Taifa huku ikiipatia nchi asilimia 25 ya fedha zote za kigeni na kutoa ajira za moja kwa moja 600,000 na nyinginezo zaidi ya milioni mbili.

Wizara hiyo inaitaja Sekta ya Utalii kujumuisha Idara ya Mambo ya Kale na hifadhi za taifa zilizopo chini ya Shirika la Hifadhi ya Taifa (TANAPA).

Orodha ya hifadhi za taifa 22 zilizoko nchini, inajumuisha Hifadhi ya Taifa Serengeti na Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA) ambazo kimapato zinasaidia kuendesha hifadhi zingine zenye mapato kidogo.

Wakati sekta hiyo ikiendelea kuwa tegemeo kwa kuingiza fedha za kigeni na kuchangia Pato la Taifa, uendelevu wa ikolojia na utalii wa KINAPA uko shakani kutokana na matukio ya moto yanayoikumba hifadhi hiyo mara kwa mara.

Tukio la hivi karibuni ni la usiku wa Oktoba 21, mwaka huu, moto ulipozuka kwenye Kambi ya Karanga na kuteketeza uoto wa asili kwenye eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 34, kwa mujibu wa Ofisa Uhifadhi Mwandamizi - Mawasiliano wa TANAPA, Catherine Mbena.

Inakopatikana kambi hiyo, ni umbali wa mita 3,963 kutoka usawa wa bahari, eneo hilo likiwa na sifa ya kuwa na mimea aina ya Erica na Protea, inayoshika moto kwa kasi wakati wa ukame.

Hata inaporejewa kanzidata ya KINAPA, ina matukio mengine makubwa manne ya moto kwenye hifadhi hiyo yaliyotokea ndani ya miaka mitano kuanzia mwaka 2015/16.

Kanzidata hiyo inabainisha kuwa mwaka 2015/16, eneo liliiloteketea kwa moto ni hekta 49.13, mwaka 2016/17 hekta 17, mwaka 2017/18 hekta 82, mwaka 2018/19 hekta 72.3 na la Oktoba 2020 hekta 22.05, shida kuu ikitajwa kuwa uvunaji mbaya wa asali, ujangili na mbinu mbaya za kilimo.

**WENYEJI WANENA**

Mkazi wa Moshi mkoani Kilimanjaro, Mwalimu Ruston Msangi (33), katika mazungumzo na Nipashe, anaeleza uzoefu wake kuhusu matukio ya moto kwenye Mlima Kilimanjaro, akisema:

"Huenda yanasababishwa na wenyeji wanaokaa karibu na hifadhi, ambao kwa makusudi au kwa bahati mbaya wanapoandaa mashamba yao, wanachoma hadi eneo la hifadhi.

"Pia kuna watu ambao wanaingia hifadhini kuwinda au kurina asali, hao pia huenda kwa makusudi au bahati mbaya wanachoma hifadhi."



Askari wakizima moto kwenye Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro Oktoba 2020. **PICHA NDOGO CHINI:** Kabla ya kudhibitiwa kwa moto huo hifadhini.

Ni hoja inayoungwa mkono na Emmanuel Lyimo (38), mkazi wa Kibosho wilayani Moshi Vijijini anayewasilisha mtazamo wake, akiamini shughuli za kilimo ni chanzo kikuu cha matukio ya moto KINAPA.

"Unakuta baadhi ya watu wanasafisha mashamba kwa kuchoma moto, hivyo wakati mwingine moto unapeperushwa na upepo kwenda hifadhini," Lyimo anasema.

Mkazi mwingine wa Kibosho, Upendo Tarimo (45), anadai matukio ya moto KINAPA ni hujuma zinazofanywa na baadhi ya watu kwa lengo la kujipatia fedha zinazotolewa kwa ajili ya kuzima moto hifadhini pindi matukio hayo yanapotokea.

Ofisa Utumishi na Utawala wa Kampuni ya ZARA Tours inayoratibu upandaji wa watalii KINAPA, Benard Sahini, anasema majanga ya moto hifadhini yanasababisha kupoteza nguvukazi, fedha na gharama za matibabu kwa wahusika.

"Mbali na kusababisha mabadiliko ya tabianchi, matukio ya moto hifadhini pia hupunguza idadi ya watalii wanaokuja kufanya utalii nchini kutokana na kuwapo picha za matukio ya moto kwenye mitandao ya kijamii," anafafanua.

**KAULI YA TANAPA**

Kamishna wa Uhifadhi wa TANAPA, William Mwakilema, katika taarifa yake rasmi kwa umma kuhusu uchunguzi wa moto uliozuka Oktoba 21, mwaka huu kwenye maeneo mbalimbali ya Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro, anabainisha kuwa ulisababishwa na shughuli za binadamu.

Anakiri moto huo kuteketeza mimea na ikolojia ya hifadhi hiyo japo hakuna madhara yaliyotokea kwa watalii, waongoza watalii, wapagazi na miundombinu ya barabara wanazotumia watalii wakati wa kupanda Mlima Kilimanjaro.

"Moto huo umeteketeza kilomita za mraba 34.2 za uoto wa asili kwenye eneo la Mlima Kilimanjaro ambalo lina mimea aina ya Erica na Protea inayoshika moto kwa kasi kutokana na ukame.

"Taarifa za awali zimebaini kuwa chanzo cha moto huo ni shughuli za binadamu. Kitengo cha Usalama cha TANAPA kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama, vinaendelea na utafiti ili kubaini wahusika wa tukio hilo.

"Pia tulifungua jalada la uchunguzi kwenye Kituo Kikuu cha Polisi Moshi lenye kumbukumbu namba MOS/RB/RB/9563 2020 na MOS/IR/877. Kwa minajili hiyo, atakayebainika pasi na shaka kuhusika na tukio hilo, atachukuliwa hatua stahiki ili iwe fundisho kwa watu wenye tabia ya kusababisha moto kwenye hifadhi hiyo," Kamishna Mwakilema anawasilisha.

Kwa mujibu wa Kamishna Mwakilema, TANAPA ilipata taarifa za moto huo kuzuka eneo la Karanga majira ya saa 2:30 usiku wa Oktoba 21, mwaka huu, kupitia kwa Mwalimu wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori (Mweka) kutokana na bonde hilo kuonekana vizuri kutokea maeneo ya chuo hicho.

Katika kinachoonekana TANAPA kuwa na mbinu hafifu kukabili majanga ya moto, Kamishna Mwakilema anasema kazi ya kuzima moto huo ilianza Oktoba 22, mwaka huu (yaani siku iliyofuata baada ya moto kuzuka) hadi Oktoba 28 mwaka huu moto huo ulidhibitiwa kwenye maeneo mengi korofi, ikiwa ni wastani wa siku saba.

Kwa mujibu wa bosi huyo wa TANAPA, Oktoba 29, mwaka huu, ikiwa ni siku moja baada ya moto huo kudhibitiwa kwenye maeneo korofi, ulilipuka tena eneo la Mto Karanga na kusambaa kuelekea maeneo ya Umbwe na Baranco kutokana na upepo mkali uliosababisha kulipuka moto kutoka kwenye magogo yaliyokuwa yametengeneza mboji.

"Usiku wa Oktoba 29, mwaka huu, moto mpya uliwaka eneo la Mandara, upande wa Marangu na kusambaa kushuka msitu wa asili lakini kutokana na upepo mkali uliokuwa unabadilisha mwelekeo mara kwa mara, ulisambaa kuelekea Kwa Masheu na Mlima Kifinika lakini hadi Novemba Mosi mwaka huu (yaani baada ya siku nne) kukawa na mafanikio makubwa ya kudhibiti moto huo," anasema.

Kamishna Mwakilema anabainisha kuwa katika harakati za kuuzima moto huo, walikumbana na vikwazo mbalimbali yakiwamo makorongo makubwa ambayo ni vigumu kuyafikia kwa miguu, hususani makorongo ya Karanga, Baranco, Umbwe, Lyamungo na Mweka.



Anataja vikwazo vingine ni pamoja na uzoefu mdogo wa uzimaji moto kwenye mazingira ya milimani hususani kwa wadau ambao hawana uzoefu wa kupanda mlima, ukame, upepo mkali, kuwapo mimea ya Erica inayoshika moto haraka na mrundikano wa mboji kwenye udongo iliyokuwa inahifadhi moto aridhini.

"Eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 34.2 lenye mimea ya Erica na Protea limeteketea kwa moto, mimea hii inahifadhi maji ardhini, imeteketea kwa moto kwenye maeneo moto ulikowaka.

"Kuna madhara ya kiikolojia pamoja na wanyama wadogo wagodo kufa kutokana na moto huo," Kamishna Mwakilema anafafanua.

Katika kile kinachoonekana TANAPA kutokuwa na uwezo wa vifaa na hata kuwa na maandalizi hafifu kupambana na majanga ya asili, Kamishna wa Uhifadhi wa TANAPA Kanda ya Kaskazini, Betrita James anasema kuwa baada ya kupata taarifa za moto huo kuzuka hifadhini Oktoba 21 mwaka huu, Menejimenti ya KINAPA ilianza kukusanya nguvu kazi, vifaa na timu ya watu mbalimbali na wadau wengine kwa ajili ya kusaidia juhudi za kuuzima moto huo.

Vilevile, wakati uzimaji moto ukiendelea hifadhini huko, Kaimu Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Kilimanjaro, Abraham Ntezidyo, alikaririwa na Nipashe Oktoba 23, mwaka huu akisema jitihada za kuuzima moto huo zilikuwa zinaendelea mlimani na walitarajia kutafuta ndege maalum ya uokoaji kwa ajili ya kuzima moto, kauli inayotoa fasili kwamba mamlaka hazina uwezo wa vifaa na maandalizi ya kupambana na majanga ya aina hiyo.

**INAENDELEA KESHO**



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, akisalimiana na baadhi ya viongozi wa Madrasat Hayaatul Atfaal ya Baghani Wete, Pemba, alipowasili kufungua mkutano wa tano wa mwaka wa madrasa hiyo uliofanyika Wilaya ya Magharib B Unguja jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS**

# Maaskofu wahimiza kulinda maadili

**Na Waandishi Wetu**

MAASKOFU wamewataka Watanzania kudumisha amani na utulivu na kushiriki kikamilifu kwenye malezi ya watoto na kulinda maadili mema ya kumcha Mungu wakati wote.

Wito huo ulitolewa jana na Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mbeya, Gervas Nyaisonga, katika mabubiri ya mkesha wa Krismasi uliofanyika kwenye Kanisa Kuu la Mtakatifu Anthon wa Padua, jijini humo.

Alisema ni muhimu inapoadhimishwa sikukuu ya kuzaliwa Yesu Kristo, wazazi wawafundishe watoto wao kumcha Mungu ili kuwaepusha na maovu mbalimbali yanayotokea kwenye jamii, kwa kuwa kwenye maisha kuna nuru na giza.

Nyaisonga ambaye ni Katibu wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), alisema kwenye maeneo ya giza ndiko vitendo kama uzinzi, chuki na matendo yote maovu yanafanyika na kuwaathiri watoto.

"Hata hawa watoto watakaozaliwa leo (jana) hakikisheni mnawalea katika maadili mema ili wakue wakimwamini Mungu, siku hizi maovu yanayofanyika kwenye jamii ni mengi sana, hivyo tuwafundishe watoto wetu kutotumbukia kwenye giza.

Aidha, aliwataka viongozi wa ngazi mbalimbali za serikali na taasisi za umma kuwa waadilifu ili kuwahudumia vizuri wananchi na kujenga imani kwa wanaowahudumia na kukumbusha kuwa uadilifu ni muhimu kwenye maisha ya kiongozi yeyote bila kujali ngazi anayoongoza.

**UBINAFSI**

Askofu Mkuu Mwandamizi wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam Tanzania, Yuda Thaddeus Ruwa'ichi, aliwataka Wakristo kutumia sikukuu hiyo kumpokea Yesu kwenye mioyo yao kwa maslahi ya watu wote na si yao binafsi na kuwa wakweli.

Pia aliwataka kumpokea kwenye mioyo yao na sio kwa jina ikiwamo kutenda mema yanayompendeza kwa ajili yake na wanadamu.

"Ujumbe ni kwamba tuwe macho kwa kumpokea mwokozi kwenye mioyo yetu na si kwa jina. Sisi ni watoto wa Mungu, si kwa masilahi yetu binafsi, tumuombe atufanye watoto wake," alisema Askofu Ruwa'ichi.

"Katika zawadi hii ya Krismasi tunapomshukuru Mungu kwa zawadi hii, tumuombe atupe roho wake mtakatifu, tupate kuwa wakweli, wafuasi na mashahidi wake, tumfanye atambulike kwa walimwengu, aaminiwe na ashuhudiwe na walimwengu wote.

"Katika mahusiano yetu na wengine, tutende mema kwa wengine, kwa kila mtu tunayekutana naye. Kwa maneno mengine, tukiwa kama wapelekwa wa Mungu, twende tukiangazwa na mwana wake, ambaye ndiye ukweli wa maisha yetu.

Naye Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, Amon Kinyunyu, akihubiri kwenye ibada iliyofanyika Kanisa Kuu Usharika wa Dodoma Mjini, alisema jamii inatakiwa kushirikiana katika kusherehekea sikukuu hiyo.

Askofu Kinyunyu, alisema Yesu Kristo alikuja kuwakomboa wote bila kujali dini ya mtu yeyote na kutaka watoto washirikiane katika sikukuu hiyo.

Aliwaomba wazazi kukaa na familia zao kwenye sikukuu hizi ili kutafakari kwa pamoja na kuwafundisha mambo mema.

"Tunajua watu wengi wamekuwa katika kazi zao kwa muda mrefu hivyo sikukuu hii tuitumie kukaa pamoja na kutafakari mambo mema," alisema.

Kadhalika, alisema Krismasi imekuwa ikiwakumbusha jamii zote kuishi kwa amani na upendo na kushauri watu wavumiliane katika maeneo wanayoishi

Askofu Mkuu wa Jimbo Katoliki Dodoma, Beatus Kinyaiya, aliwataka waumini kubadilika kwa kutenda matendo matakatifu katika mwaka 2023 tofauti na walivyofanya mwaka huu.

Aliitaka jamii kukemea ukatili na ulawiti kwa jamii ili kuhakikisha watoto wanakuwa katika maadili mema alipohubiri katika Kanisa Katoliki la Paulo wa Msalaba lililoko jijini hapo.

Alisema hivi sasa ukatili umeshamiri maeneo mbalimbali jamii inapaswa kubadilika ili kusaidia watoto kukua na kutimiza ndoto zao kielimu.

Kadhalika watu wanapaswa kuwa na malaika wa amani katika vinywa vyao ambaye atawasaidia kuzungumza mambo mema.

Alisema muumini anapaswa kuwa mstari wa mbele kukemea uovu ili jamii iweze kuwa katika mstari unaopendeza.

**MAZINGIRA**

Askofu wa Jimbo Katoliki la Mbulu, Anthony Lagwen, aliwataka Watanzania kuyachukua matokeo ya sasa ya athari za mabadiliko ya tabianchi na kujifunza namna ya kukabiliana na hali hiyo ili kuzuia madhara zaidi kwa binadamu na viumbe wengine.

"Ninawasihi sana Watanzania kutunza mazingira ili kuepusha mabadiliko ya tabianchi, ambayo yanaleta madhara kwa maisha ya binadamu.

"Tujenge tabia ya kupanda miti na kuitunza ili kuhifadhi uoto wa asili, ambao unasaidia upatikanaji wa mvua. Mazingira yasipotunzwa vizuri yanasababisha madhara kwa binadamu, wanyama, mimea na ndege ambavyo vyote ni muhimu na vinategemeana," alisema Askofu Lagwen.

**MAADILI**

Maaskofu wa Kanisa Katoliki kutoka Jimbo la Shinyanga na Mwanza wamewataka waamini wa Katoliki kuimarisha amani na kuishi imani zao kwa kutoa malezi bora kwa watoto, ili kulijenga taifa tulivu kuanzia kwa watoto hao.

Alisema amani dunia imepungua kwa sababu kila siku machafuko yanatokea, vita vinaendelea, watu wanauana ovyo, wanakatili watoto wao na wengine kuwazika wakiwa hai.

"Dunia imepungukiwa na amani kwa sababu watu hawana Kristo mioyoni mwao wala hofu ya Mungu, ndiyo maana kila kukicha tunashuhudia matukio ya ajabu, watoto wanaua wazazi wao na wazazi pia wanaua watoto wao tena kwa kuwazika wakiwa hai," alisema Askofu Sangu.

Alisema chimbuko la amani pekee ni kumpokea Yesu Kristo ndani ya mioyo, na hakutakuwa tena na machafuko, mafarakano, ugomvi, ufisadi, vita, mauaji ya watu wasio na hatia, wala vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

Naye Askofu wa Jimbo Kuu la Mwanza, Renatus Nkwande, aliwataka Watanzania kuwapa malezi bora watoto bila kujali undugu pamoja na ukaribu walionao kwa watoto, kwa kuwasaidia kukua katika maadili mema na kutokomeza ukatili.

Aliwataka wazazi kuwa makini na utandawazi hususani kwa watoto wao ambao kwa sasa umeonekana kuwafanya waamini wa Katoliki kuwa watumwa wa matumizi ya mitandao ya kijamii na kusahau kujiweka karibu na Mwenyezi Mungu.

Aliwataka Watanzania washerehekee pamoja na familia zao na kusaidia watu wenye uhitaji badala ya kufanya mambo ya anasa ikiwamo ulevi na kuwaruhusu watoto kushiriki katika kumbi za starehe maarufu kama disko toto ambazo zipo kinyume na maadili ya dini hiyo na utamaduni.

Baadhi ya waumini wa kanisa hilo, Yuritha Albert, waliahidi kuishi imani yao kwa kutenda matendo mema yampendezayo Mwenyezi Mungu ikiwa ni pamoja na kusherehekea sikukuu hiyo kwa kuwajali wenye uhitaji.

Naye Padri Silvester Litunga wa Kanisa Katoliki, Jimbo la Tanga, aliwataka waumini watumie sikukuu ya kuzaliwa Yesu Kristo kurudisha furaha na amani kwenye mioyo yao badala ya vilio wala mifarakano, wakati akihubiri katika Kanisa la St. Theresia Barabara ya 20 jijini Tanga.

Padri Litunga ambaye ni Mwanasheria wa Jimbo la Tanga alisema kwamba Yesu Kristo alikuja ili kuwakomboa na utumwa wa dhambi.

"Hatuna furaha kwa sababu tupo kwenye ulimwengu wenye chuki, mifarakano na watu mioyo yao imeumizwa hivyo tutumie kuzaliwa kwa mwokozi Yesu kurudisha furaha katika mioyo yetu na kusameheana," alisema.

Naye Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa Muheza wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), John Ndimbo, alisema wataitumia sikukuu ya Krismasi kuliombea taifa lisiingie katika machafuko wala uvujifu wa amani.

Mchungaji Mchungaji wa KKKT Usharika wa Maili Moja, Ezekiel Ngao aliwakumbusha Watanzania kuenzi tunu ya taifa ya amani wakati na kuachana na vitendo viovu ambavyo vitasababisha uvunjifu wa amani.

Alisema kuwa amani inatakiwa ianzie kwenye familia, nyumba za watu, vikundi na maeneo mbalimbali, lakini Watanzania wanatakiwa kutokubaliana na watu wanaotaka kuwagawa.

Aidha, alisema kuwa watu wasimkaribishe shetani kwa kufanya mambo yanayokwenda kinyume na maadili ya kitanzania ikiwa ni pamoja na kuachana na ulevi.

Mchungaji wa Kanisa Anglikana Mt. Gabriel Kibaha, Exavia Mpambichile, aliwashauri waumini kutumia Sikukuu za Krismasi na mwaka mpya kutulia na familia zao nyumbani na wakienda matembezini waambatane pamoja ili kujenga upendo wa familia ambao ni msingi wa kila kitu.

***Imeandikwa na Elizabeth Zaya (DAR), Nebart Msokwa (MBEYA), Jaliwason Jasson (MBULU), Oscar Assenga na Steven William (TANGA) na Julieth Mkireri (KIBAHA).**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu ziheshimu mikataba na maamuzi ya wachezaji

**DIRISHA** dogo la usajili limeanza kupamba moto kwa baadhi ya klabu kuanza kutangaza wachezaji wanaowasajili kwa ajili ya kuboresha vikosi vyao wakati huu mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara ukiendelea kutimua vumbi kwa klabu kucheza mechi zao za 18 msimu huu.

Tayari Klabu ya Simba imetangaza kufikia makubaliano na kumsajili rasmi kiungo wa Geita Gold, Saido Ntibazonkiza, kwa mkataba wa mwaka mmoja na nusu, ambaye amejiunga na wachezaji wenzake jijini Mwanza kuendelea na maandalizi ya ligi hiyo dhidi ya KMC FC leo.

Mbali na Simba, pia imeshuhudiwa kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto', barua aliyoiandikia klabu yake ya kuvunja mkataba kwa mujibu wa kipengele alichoeleza kuwamo katika mkataba wake cha kulipa ada ya uhamisho ya Sh. milioni 100 pamoja na mishahara ya miezi mitatu endapo atataka kuuvunja.

Katika barua hiyo, ambayo imesambaa kwenye mitandao ya kijamii na yeye kukiri ni yake, ameandika akieleza kuambatanisha na vielelezo vya malipo ya benki kiasi cha Sh. milioni 112, ambazo ni pamoja na mishahara ya miezi mitatu, ambazo zinamfanya kuwa mchezaji huru, huku ikidaiwa kwamba Azam FC ni miongoni mwa klabu zinazovutia na huduma yake.

Hata hivyo, uamuzi huo wa Fei Toto umeonekana kupingwa huku uongozi wa klabu hiyo ukieleza kumrejeshea fedha hizo, kwa kuwa haukubaliani na uamuzi huo, na ukiweka wazi kuwa ni mchezaji wao halali huku ukimtaka kuheshimu mkataba wake.

Kwa ujumla hatutaki kuingilia uamuzi wa pande mbili hizo, bali dhamira yetu ni kutaka kuona mikataba inaheshimiwa na pande zote bila kujali ukubwa wa klabu ama mchezaji.

Lakini katika hilo kila klabu ifike wakati ifahamu maisha ya mchezaji kisoka uwanjani ni mafupi sana, hivyo anahitaji kutumia kipindi chake vizuri wakati akiwa katika kiwango bora cha kuvutia, ili kujitafutia maslahi mazuri kwa maisha yake ya baadaye.

Aidha, ni muhimu kwa klabu kutambua kwamba mchezaji anapokiri hadharani kwamba amepoteza mapenzi na klabu anayoichezea, basi ni wakati wa kukaa pamoja chini na kuangalia namna ya kuvunja mkataba kwa maslahi ya pande zote ili kumwacha huru aende kucheza alipoonyesha mapenzi nako.

Hakuna haja ya kumng'ang'ania mchezaji ambaye amepoteza mapenzi na klabu, lakini kwa kulinda chapa ya klabu ili kuwafanya wachezaji wengine kuiona ni sehemu sahihi ya kufanya kazi, mchezaji anapopata malisho mazuri na kufuata taratibu za kimkataba za kuuvunja ni vema kupeana mkono wa kwaheri kwa amani.

Tunatambua mkataba ni siri kati ya mwajiri na mwajiriwa, hivyo pande hizo mbili ndizo zinazojua ukweli ulipo lakini Yanga kama klabu kubwa nchini na Afrika Mashariki, haipaswi kuendelea kumshinikiza mchezaji aliyepoteza mapenzi na klabu yao tena katika kipindi hiki ambacho dirisha la usajili lipo wazi ambapo wanaweza kupata mbadala. Lakini pia sakata hili la Fei Toto na Yanga, ni limekuja wakati muafaka ambao wachezaji wengi wanasajiliwa, hivyo hawana budi kulibeba kama mfano wa kuigwa wakati wakisaini mikataba yao kuisoma vema na kuielewa badala tu ya kukimbilia kuangalia usahihi wa tarakimu za namba za maslahi yao.

Hili linapaswa kuwa somo kwa wachezaji wengine wa Tanzania, ambao mara nyingi wanapoingia mikataba, kikubwa wanachotazama ni kiasi cha fedha watakazolipwa na si vipengele muhimu kama hivyo ambavyo vinaweza kuwasaidia baadaye watakapoona mambo hayaendi sawa. Kadhalika, umefika wakati kwa klabu zetu kuona haja ya kuwalipa wachezaji kulingana na ubora wanaouonyesha uwanjani na si viwango vya mishahara kutegemea na nchi mchezaji anayotoka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

### Usajili ufanywe haraka wachezaji wasaidie timu

**KABLA** ya dirisha dogo la usajili karibuni klabu zote za Ligi Kuu zilkuwa zikilalamika kuwapo kwa mapungufu kwenye vikosi vyao na makocha wakiahidi kufanya marekebisho litakapofunguliwa.

Ni klabu mbili tu ambazo zilionekana hazina mahitaji makubwa sana kwenye dirisha hili, nazo ni Yanga na Azam FC.

Nilimsikia hata Kaimu Kocha Mkuu wa Azam FC, Kalimangonga Ongala, akisema kikosi chake hakihitaji marekebisho sana, na kinaweza kuendelea hata kilivyo bila kusajili, lakini kama akiingia mtu mmoja ama wawili, basi wanatosha. Hata Yanga kikosi kinavyoonekana hakihitaji maingizo mengi, ni mchezaji mmoja au wawili tu. Yanga na Azam ndiyo timu ambazo hata kusingekuwa na dirisha dogo la usajili wana vikosi ambavyo vingeweza kucheza hadi mwisho wa msimu zisiwe na matatizo makubwa. Zilizobaki zina mapungufu makubwa ambayo yanahitaji wachezaji angalau kuanzia wawili kwenda mbele ili kuboresha vikosi vyao, ikiwamo Simba.

Naona tayari Simba imeanza kufanya usajili kwa kumtambulisha Saido Ntibazonkiza kutoka Geita Gold. Na jana jioni pia ilitarajia kumtambulisha mchezaji mwingine. Singida Big Stars nayo imeshamsajili Nickson Kibabage kutoka Mtibwa Sugar.

Zoezi la usajili wa wachezaji kipindi hiki linaendelea hadi Januari 15, mwakani. Hata hivyo, imeonekana klabu nyingi au viongozi wake bado wana usajili wa kimazoea. Ule usajili wa kusibiri siku chache kabla dirisha kufungwa.

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), awali kabisa wakati linafungua dirisha lilitahadharisha mambo kadhaa, ikiwamo kuzitaka klabu zisajili wachezaji haraka na kuacha tabia ya kusubiri hadi dakika za mwisho. Kwanza kabisa inasababisha mtandao kuwa 'bize' sana na kutofanya kazi yake kama unavyotakiwa kiasi cha kusababisha matatizo mengi. Ni kwa sababu klabu nyingi zimekuwa zinatuma majina mengi kwa wakati mmoja.

Kama nilivyosema awali, yale malalamiko ya mapungufu ya vikosi vyao nilitegemea saa hizi klabu zingekuwa zikipigana vikumbo kutambulisha wachezaji. Lakini ukiondoa Simba na Singida Big Stars, nyingine kimya kimetawala. Ninavyojua mimi siyo kama hazitosajili, tabia ni ile ile ya kusubiri dakika za mwisho. Lakini kama wakisibiri hivyo itakula kwao.

Kwa msimu wa tatu sasa wachezaji wanaosajiliwa kipindi cha dirisha dogo, wanaingia moja kwa moja na kucheza, tofauti na zamani. Miaka ya nyuma ambapo dirisha lilipokuwa likifunguliwa Novemba 16, hata kama klabu ikisajili mchezaji hawezi kuanza kuichezea timu yake mpya mpaka Desemba 15, bado anakuwa nje ya dimba hadi kamati inayoshughulikia masuala ya wachezaji ikae na kupitisha majina hayo.

Siku hizi mchezaji anasajiliwa leo, kama jina likiingia kwenye mfumo tu kesho yake anacheza kama kocha akimpanga. Hakuna kusubiri kamati tena. Nashangaa kuna timu ambazo zina mapungufu makubwa, huu ulikuwa ndiyo wakati ambao tayari wangekuwa wamesajili haraka wachezaji kwa ajili ya kuviimarisha vikosi vyao.

Itakuwa haina maana yoyote kama timu itayokamilisha usajili wake Januari mwakani, halafu tayari imeshapoteza mechi nyingi kiasi cha hata wachezaji waliosajiliwa wasiweze kufanya chochote cha kuziokoa timu hizo.

Mfano mdogo timu ya Ruvu Shooting ambayo kocha wake, Mbwana Makata anasema wachezaji wanane wamekwenda kwenye mafunzo ya kijeshi na inachezesha mawinga nafasi ya ushambuliaji na mabeki kwenye eneo la kiungo. Muda huu ninaoandika nilitarajia tayari ingekuwa imeshusha vifaa kwa ajili ya kusaidia kuiokoa kwenye janga la kushuka daraja.

Mpaka sasa sijasikia imemsajili mchezaji yoyote. Sijui nayo inasubiria Januari mwakani. Huu ndiyo muda ambao inatakiwa ipambane kujinusuru. Juzi imefungwa na Namungo bao 1-0 ikiwa ni mechi ya 12 bila kupata ushindi. Je, nayo inasubiri wachezaji Januari? Na siyo hiyo tu, kuna Coastal Union, Polisi Tanzania na zingine nyingi.

Itakuwa ni makosa kama dirisha limefunguliwa ndiyo baadhi ya klabu zinaanza kujongea wachezaji kwa ajili ya usajili.

Kama kuna viongozi ambao walikuwa wanasubiria dirisha lifunguliwe ndiyo waanze kusaka wachezaji basi watakuwa wamechelewa sana.

Nadhani huu ndio ulikuwa wakati wa kufanya haraka ili wachezaji waje kuziokoa au kuzipa nguvu timu. Viongozi wakisubiri mpaka wakati wa kufunga usajili wakati zitakuwa zimebaki mechi chache itakuwa imekula kwao.

HABARI KITAIFA

# Mgodi wapeleka faraja Kituo cha Afya Bugarama

**Na Mwandishi Wetu**

MGODI wa Barrick Bulyanhulu umekabidhi zawadi za Sikukuu ya Krismasi kwa wazazi na wagonjwa waliolazwa kwenye wodi katika Kituo cha Afya Bugarama, Halmashauri ya Msalala na wafanyakazi wa kituo hicho.

Akizungumza baada ya kugawa zawadi hizo, Meneja Mkuu wa Barrick Bulyanhulu, Cheick Sangare, alisema kampuni itaendelea kushiriki shughuli za maendeleo kwa jamii inayoishi kuzunguka mgodi huo.

Alisema Barrick Bulyanhulu imefanikiwa kutekeleza miradi ya ujenzi wa zahanati 28 katika Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga na Halmashauri ya Nyang'hwale, mkoani Geita ambazo zimekamilika na kuanza kutoa huduma na nyingine katika hatua mbalimbali ya ujenzi.

Alisema, mgodi pia umechangia fedha za utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo sekta ya elimu kwa kujenga shule za sekondari halmashauri za Msalala na Nyang'hwale na miradi mingine ya sekta za kimkakati ikiwamo maji.

Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Msalala, Charles Fusi, aliupongeza mgodi huo kwa kuchangia kuleta maendeleo na kushiriki kusaidia changamoto zinazowakabili wakazi wa maeneo ya jirani.

"Hili zoezi linalofanyika hapa la kutoa zawadi kwa wagonjwa na watumishi wa Kituo cha Afya Bugarama ni ishara kubwa jinsi mgodi huo unavyoshirikiana na jamii yetu kwa upendo," alisema Fusi.

Vile vile, alisema katika mwaka huu wa fedha 2022/2023, jumla ya zahanati 18 zimejengwa kwenye halmashauri yake na tisa kati yake zimeanza kutoa huduma ya afya kwa wananchi.

"Kwa niaba ya serikali nichukue nafasi hii kuwashukuru wenzetu wa mgodi wa Barrick Bulyanhulu kwa ushirikiano na kazi nzuri kwa jamii ya Msalala, hasa kwa wananchi wanaoishi kuzunguka mgodi wa Barrick, sisi kama serikali kupitia halmashauri yetu tunawapongeza kwa mchango mkubwa katika shughuli za maendeleo," alisema Fusi.

Mganga Mfawidhi, Kituo cha Afya Bugarama, Dk. Silas Kayanda, alisema mgodi huo kupitia kitengo cha uhusiano kimekuwa mstari wa mbele kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika kituo hicho.

Diwani wa Kata ya Bugarama, Jesca Msomi, alisema mgodi huo umefanikiwa kutekeleza ujenzi wa Shule ya Sekondari Ilogi iliyoko katika kata hiyo, kwa asilimia 100 na kwamba fedha zinazotokana na pato ghafi la uzalishaji wa madini ya dhahabu (CSR), zimefanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo ya elimu, afya na maji.

Mmoja wa wagonjwa waliopokea zawadi, Elizabert Nicolaus, alitoa shukrani kwa Barrick Bulyanhulu kwa kuwakumbuka katika kipindi hiki cha sikukuu.



Waumini wa Kanisa Katoliki wakifuatilia misa ya mkesha wa Krismasi kwenye kanisa la St. Joseph mjini Zanzibar jana. **PICHA: MARTIN DONALD**

# Vibanda 'umiza' vipigwe marufuku

**Na Elizabeth Zaya**

KANISA Katoliki Tanzania limependekeza kuondolewa kwa vibanda 'umiza' kwa madai ya kuchangia vitendo vya ulawiti kwa watoto hasa wa kiume nchini.

Askofu Isaack Amani, alisema hayo wakati akihubiri kwenye mkesha wa misa takatifu ya Sikukuu ya Krismasi ilifanyika kitaifa katika Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Arusha.

"Hivi wanyama wengine wanafanya mambo hayo? ulishaona mbwa anabaka? Wenyewe wanakwenda katika sheria za maumbile jinsi Mungu alivyopanga. Leo hii watoto wetu tumewafundisha wanafanyiana wenyewe na hilo ni baa kubwa kabisa na ni mkosi kweli kweli," alionya Askofu Amani.

"Lakini na vile vibanda umiza vinawapoteza, mambo haya yapo kule, utandawazi unachangia mambo haya, shule ziko huko, wanajifunza vitu hivyo huko na nchi nzima sasa hivi vimetapakaa, tunalia mmomonyoko nani anamomonyoa kama sio sisi wenyewe.

"Kwa nini tusiviondoe hivyo vibandaumiza nchi nzima, vipo kwa wingi na watu wanagharamia na vinaongezeka bei. Mwaka juzi vilikuwa vinatoza Sh. 200, leo wanatoza Sh. 500, mwaka kesho vitaongezeka na wanavipenda sana, wanafanya kila mahali sasa hivi."

Kuhusu ndoa za jinsia moja, Askofu Amani alisema vimeanza kuongezeka na kuna haja ya taifa kuomba toba ya nguvu na kukemea mambo hayo.


"Na kuna ambao pia wanapigania ushoga, nasikia pia kule Kilimanjaro waliandamana watu 200 wanataka watambuliwe kuwa ni mashoga wana haki zao, hata hapa Arusha vimeshaingia tayari, hayo mambo ni ushahidi tosha kwamba kama jamii tunahitaji kujifikiria upya kuhusu kuumbwa kwetu na kukombolewa kwetu na tufanye toba ya ngvu," alifafanua Askofu Amani.

Kuhusu utoaji mimba, Askofu Amani alisema damu za mimba zinazotolewa nchini na duniani kwa sasa zinachafua nchi na dunia.

"Mimba ambazo zinauawa na kutupwa kwenye majalala zinatisha, je, wanyama wasio na akili hutupa mimba? Mauaji tunafanya tumboni kuchinja watoto, huu uhuru wa wanawake sasa hivi wa kuondoa mimba sio sawa, damu hizi zinachafua nchi na dunia nzima," alisema Askofu Amani.

"Takwimu zinaonyesha kwa hiari kabisa watu wanaua wengine katika uchanga wao, Mungu amekuaminisha kwa kukuumba vizuri, wewe unachezea nafasi hiyo na ndio maana wengine inapofika kutafuta mtoto hawapati wanaiba wa wenzie, wamechinja wa kwao sasa wanatafuta wa wengine, binadamu ifike mahali tuone jinsi gani Mungu ametuagiza tujali uhai wa binadamu."

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed





Kinamama wakitoa huduma ya kukodisha viatu kwa Sh. 1,000 ili kuingia sokoni kutokana na hali ya matope iliyoko katika soko la Mapipo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ummy atoa angalizo sherehe za Krismasi na Mwaka Mpya

## * Wagonjwa wa mfumo wa hewa waongezeka

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amewataka wananchi kuchukua hatua za kujikinga dhidi ya magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza na yanayoambukizwa kwa njia ya hewa katika msimu huu wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya.

Katika taarifa yake kwa umma juzi jioni, Waziri Ummy alisema Wizara ya Afya inawatakia wananchi wote gheri ya Krismasi na Mwaka Mpya wa 2023.

"Kama tunavyofahamu mtu ni afya, hivyo nitumie fursa hii pia kuwakumbusha wananchi kuchukua hatua kujikinga na magonjwa.

"Kwa mujibu wa taarifa zetu, katika kipindi cha kati ya wiki ya kwanza ya mwezi Novemba na wiki ya pili ya Desemba 2022, kumekuwa na ongezeko la magonjwa ya mfumo wa njia ya hewa.

"Ufuatiliaji wa wizara umeonyesha kuwa visababishi vikuu vya magonjwa haya ni virusi vya UVIKO-19 pamoja na virusi wengine wenye kusababisha mafua na kikohozi, mfano virusi vya Influenza (Influenza viruses)," alitahadharisha.

Waziri Ummy alibainisha kuwa wagonjwa wa UVIKO-19 wameongezeka kutoka asilimia 4.1 hadi asilimia 5.5 ambapo takwimu za wiki ya kwanza ya mwezi Novemba 2022 zinaonyesha kuwa watu 1,154 waliopima UVIKO-19, kati yao watu 47 walikuwa wanaugua UVIKO-19 huku takwimu za wiki ya pili ya mwezi Desemba 2022 zinaonyesha kuwa kati ya watu 1,294 waliopima UVIKO-19, watu 71 walikuwa wanaugua UVIKO-19.

Alisema wagonjwa wa Influenza wameongezeka kutoka asilimia 4.8 hadi asilimia 6.5. Alibainisha kuwa kati ya watu 277 waliopima Influenza katika wiki ya kwanza ya mwezi Novemba mwaka huu watu 11 walikuwa wanaugua ugonjwa huo huku takwimu hizo hizo pia katika wiki ya pili ya mwezi Desemba zikionyesha kuwa kati ya watu 155 waliopima, watu 10 walikuwa wanaugua ugonjwa wa Influenza.

"Kutokana na hali hii, wizara inaendea kuwakumbusha wananchi kuchukua hatua ili kujikinga na magonjwa haya ikiwamo kupata dozi kamili ya chanjo ya UVIKO-19 kwa ambao hawajachanja.

"Hatua hii itawaepusha kupata ugonjwa mkali wa UVIKO-19 na hata kifo. Pia kuvaa barakoa pindi mtu anapokuwa na dalili za mafua au kikohozi na awapo kwenye mikusanyiko.

"Pia tunakumbusha kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka mara kwa mara, kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima na kuzingatia kanuni za afya na usafi binafsi ikiwamo kujikinga kwa kitambaa au kiwiko cha mkono wakati wa kupiga chafya au kukohoa," alisema.

Waziri Ummy alisema wizara inaendelea kuwakumbusha wananchi kuchukua hatua za kujikinga na magonjwa kwa kufanya mazoezi ya mwili mara kwa mara angalau mara tatu kwa wiki kwa muda usiopungua dakika 30, kuzingatia lishe bora na ulaji wa vyakula unaofaa pamoja na kupunguza unywaji wa pombe na vilevi vingine.

Alisisitiza pindi mtu anapohisi ugonjwa wowote kuwahi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya uchunguzi na matibabu pamoja na kutoa taarifa za kuwapo watu wenye dalili za magonjwa ya kuambukiza katika jamii kupitia namba ya simu ya bure 199.

"Sambamba na kuchukua tahadhari ili kujikinga na magonjwa ya kuambukiza, ninatoa rai kwa watumiaji wote wa vyombo vya moto barabarani katika kipindi hiki cha sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya, kuchukua tahadhari ili kuepuka ajali zinazoweza kusababisha vifo au ulemavu wa kudumu na kuipa serikali mzigo mkubwa wa kuhudumia waathirika.

"Takwimu za Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) za kipindi cha Julai hadi Septemba 2022 zinaonyesha kuwa wagonjwa wa ajali walikuwa 2,410 na kati yao asilimia 70 walikuwa ni wagonjwa kutokana na ajali za barabarani.

"Wakati tunaufunga mwaka huu wa 2022, tathmini ya utendaji wa Sekta ya Afya, inaonyesha kuwa tumepiga hatua zaidi katika kuboresha huduma za afya nchini ikiwamo kuendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya kutoa huduma za afya kuanzia ngazi ya zahanati hadi taifa.

"Pia tumeimarisha upatikanaji wa dawa katika Bohari ya Dawa (MSD) na kwenye vituo vya kutoa huduma, kununua vifaa tiba vya kisasa ikiwamo mashine za uchunguzi za CT SCAN kwa hospitali zote za rufani za mikoa nchini pamoja na Xray na vifaa tiba vinginevyo kwenye zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na hospitali za rufani za kanda, taifa na Hospitali Maalum.

"Pia tumeweza kuongeza idadi ya watumishi wa afya katika ngazi zote sambamba na kuanzisha Mpango wa Mafunzo ya Ubingwa na Ubingwa Bobezi kwa Wataalamu wa Sekta ya Afya unaojulikana kama Samia Health Super Specialization Program ambapo mpango huu katika mwaka 2022/23 utazalisha wataalamu 457 wa kutoa huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi katika nchi yetu," alisema.

Waziri Ummy alisema kuwa kwa mwaka ujao wa 2023 wataendelea kuboresha zaidi utoaji wa huduma za afya kwa wananchi, vipaumbele vyao vikuu vikiwa ni pamoja na kuimarisha ubora wa huduma za afya ili wananchi wapate huduma bora za afya kwa wakati na katika mazingira bora na rafiki.

Kingine ni kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora za afya bila ya kikwazo cha fedha kupitia utaratibu wa Bima ya Afya kwa Wote.

"Hivyo, ninatoa rai kwa wananchi kujiunga na skimu mbalimbali za bima ya afya ili kuwa na uhakika wa matibabu kabla ya kuugua.

"Mwisho, ninapenda kuwashukuru watumishi wote wa Sekta ya Afya nchini kuanzia ngazi ya msingi hadi Taifa, watoa huduma wa afya ngazi ya jamii pamoja na wadau wote wa maendeleo ya Sekta ya Afya kwa kuwa mstari wa mbele katika kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

"Tuendelee na kazi hii ya kuwahudumia Watanzania kwa kuzingatia weledi, maadili, utu na upendo kwa wagonjwa. Na kwa Watanzania wenzangu, tungane pamoja kuzilinda afya zetu na za wenzetu kwa mustakabali wa maendeleo yetu, jamii zetu na ya Taifa kwa ujumla. Mtu ni afya, jali afya yako," Ummy alihimiza.

# Polisi, SBL watoa mafunzo ya unywaji pombe kistaarabu

**Na Frank Monyo**

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kwa kushirikiana na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) wametoa mafunzo ya unywaji pombe kistaarabu kwa madereva zaidi ya 100 wa pikipiki na bajaji na kuwaelimisha juu ya uendeshaji salama wa vyombo vya moto katika kipindi cha sikukuu za mwishoni mwa mwaka.

Mkurugezi wa Masoko wa SBL, Anitha Rwehumbiza, akizungumza jana wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Kijitonyama, Dar es Salaam, alisema takwimu zinaonyesha ajali za barabarani ni moja ya vyanzo vikuu vya vifo nchini.

Alisema sababu kubwa ni uzembe barabarani, mwendo kasi na kuendesha vyombo vya moto wakiwa wametumia kilevi hasa katika msimu wa sikukuu, hivyo elimu ya usalama barabarani ni muhimu kwa watumiaji wote.

"Katika msimu huu, SBL na Jeshi la Polisi wameelimisha madereva kuhusu umuhimu wa kuzingatia sheria za usalama barabarani na kuacha kuendesha vyombo vya moto wakiwa wametumiwa kilevi.

"Madereva magari, waendesha pikipiki na bajaji wameelimishwa juu ya unywaji kwa kiasi na kuaswa kuwa mabalozi wa usalama barabarani kwa wenzao na watumiaji wengine wa barabara.

"Kupitia ushirikiano huu na Jeshi la Polisi Tanzania tunategemea madereva magari na pikipiki tuliowapa mafunzo watakuwa mabalozi wazuri hasa katika kipindi hiki cha sikukuu ambapo tumewahimiza kutokunywa na kuendesha vyombo vya moto.

"Madereva wetu wote wana jukumu la kuhakikisha abiria wao wamefika kwenye maeneo wanayokwenda salama," alisisitiza.

Alitoa ushauri kwa watumiaji wa pombe kunywa kwa kiasi, kunywa maji katikati ya unywaji pombe na kuwa na dereva maalum (asiyelewa) na kuhakikisha kutoendeshwa na dereva aliyetumia kilevi kupitiliza.

Mwanasheria wa Kikosi na Mkuu wa Dawati la Elimu Jeshi la Polisi Usalama Barabarani Makao Makuu, Kamanda Deus Sokoni, alifurahishwa na juhudi za SBL katika kuelimisha madereva bodaboda na bajaji kuhusu usalama barabarani hasa katika kipindi hiki cha sikukuu.

"Niwapongeze SBL kwa jitihada hii kwa sababu inavutia na kuhusisha kila mdau. Mafunzo haya nina amini kabisa yatazuia ajali zisizokuwa na msingi na matukio mbalimbali ya barabarani katika kipindi hiki cha sikukuu," alisema Kamanda Sokoni.

# DC akabidhi zawadi iliyotolewa na Samia

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa zawadi mbalimbali za vyakula kwa ajili ya sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya kwa Kituo cha Aloysia cha kulelea watoto walio katika mazingira magumu kilichoko wilayani Iramba mkoani Singida.

Vitu vilivyotolewa ni mchele kilo 75, mbuzi watatu, maharage kilo 46, mafuta ya kupikia lita 20 na viungo mbalimbali vya kupikia.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, akikabidhi vyakula hivyo juzi kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema Rais ametoa vitu hivyo kutokana na upendo mkubwa alionao kwa watu wake hususani kwa watoto.

"Rais ana upendo kwa watu wote lakini ana upendo zaidi kwa watoto na anawataka msome kwa bidii, mpendane na muwapende watu wengine," alisema Mwenda wakati akizungumza na watoto wa kituo hicho.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani hapa, Martha Mlata, alisema kuwalea watoto walio katika mazingira magumu hiyo ndiyo ibada njema kwa kuwa wanasaidiwa hadi wanabadilisha tabia zao na kuwapa njema.

"Rais Samia anaupenda sana Mkoa wa Singida na ndiyo maana ametoa mamilioni ya shilingi kujenga shule ya sekondari maalum kwa ajili ya wanafunzi wa kike, someni sana ili mje mpate fursa ya kujiunga kwenye shule hiyo," alisema.

Mlata alisema kutokana na upendo anaoonyesha Rais, jukumu la wananchi ni kuzidi kumwombea ili aendelee kuiongoza nchi vyema kwa maendeleo zaidi.

Mwangalizi wa Kituo cha Aloysia, Sister Ester, alisema kituo hicho kinatoa huduma za malezi, elimu, afya, chakula lishe na elimu ya stadi za maisha.

Alisema mafanikio yaliyopatikana kwenye kituo hicho ni pamoja na kuwawezesha watoto kubadilika tabia na mwenendo waliokuwa nao uliotokana na athari za mazingira waliyokuwa wakiishi.




Wananchi wakiwa kwenye foleni ya kununua nyama kwa ajili ya Sikukuu ya Krimasi kwenye bucha la Ubungo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Viongozi wa dini, wazee kimila wasisitizwa kukemea ukatili

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

VIONGOZI wa dini, wazee maarufu na viongozi wa kimila wilayani Masasi wamesisitizwa kuikumbusha jamii kuepuka vitendo viovu vya kikatili dhidi ya wanawake na watoto ikiwamo mauaji ambayo yamekuwa yakijitokeza wilayani humo.

Wito huo ulitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, alipokuwa akifungua kikao cha tathmini ya mpango wa maendeleo wa wilaya hiyo uliofanyika mjini hapo.

Kitta alisema viongozi wa dini pamoja na wa kimila bado wana wajibu wa kuendelea kuikumbusha jamii kuepuka na kuachana na tabia ya vitendo viovu vya mauaji, ubakaji na ukatili dhidi ya wanawake na watoto ambavyo vimekuwa vikitokea wilayani Masasi.

Alisema viongozi hao wakiyatumia vyema majukwaa kupitia kwenye nyumba za ibada na wa kimila wakiendelea kuijengea jamii imani ya kwamba vitendo hivyo ni vibaya, inaweza kubadilika na kuachana na vitendo hivyo vya ukatili.

"Kwanza nawashukuru sana viongozi wa dini na wale wa kimila kwa kuendelea kuiombea Masasi na hadi sasa kumekuwa na utulivu, amani na upendo pia tusiache kuiombea jamii kuacha vitendo viovu," alisema Kitta.

Alisema jamii ikiwa na hofu ya Mungu pamoja na imani ya kimila hata maovu yanayoendelea kutokea yanaweza kutoweka na kuishi kwa amani na upendo. Kitta alisema viongozi wa dini waendelee kuiombea Wilaya ya Masasi ili matokeo ambayo yamekuwa yakiendelea ya unyanyasaji wa kijinsia pamoja na mauaji ya wanawake yasiwe yanajitokeza.

Hamisi Baina, Katibu wa Baraza la Waislamu Wilaya ya Masasi (BAKWATA), alisema viongozi wa dini wanafanya kazi kubwa ya kuikumbusha jamii kuwa na hofu ya Mungu.

Alisema amani yoyote ile inatokana na mtu kuwa na imani ya dini na hata matukio yanayotokea kwa sasa ndani ya Wilaya ya Masasi kama jamii ingekuwa na hofu na Mungu yasingekuwapo. Naye Yusufu Nanyoho, mzee maarufu alisema wanasikitishwa na vitendo viovu vinavyoendelea kujitokeza na kwamba bado vyombo vya ulinzi na usalama vinapaswa kufanya kazi kwa weledi ili kuwabaini wahusika na wachukue hatua.

# Mtambo wa kufua umeme kupigwa mnada kisa deni

**Na Christina Mwakangale**

MTAMBO wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi wa Kampuni ya Aqua Power Tanzania, unaozalisha takribani megawati 45 mkoani Mtwara, unatarajiwa kupigwa mnada baada ya mmiliki wake kushindwa kulipa deni analodaiwa na benki.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Wakili Adronicus Byamungu alisema kampuni hiyo ambayo tayari imewekwa chini ya usimamizi wake, mtambo wake utauzwa ikiwa ni sehemu ya mali ya mdaiwa ili kulipa deni la benki.

"Mtambo ulikuwa unafanya kazi na umefanya kazi kwa miaka miwili hadi kufikia Oktoba mwaka 2020. Umeme wote uliokuwa unazalishwa alikuwa akinunua Dangote," alisema wakili huyo kutoka Kampuni ya ADCA Veritas Law Group Advocates.

Byamungu alisema mtambo huo ulioko eneo la kilomita za mraba 15,807 kiwanja namba moja block 'A' Hiyari Area wilayani Mtwara, utauzwa kwa zabuni na yeyote atakayeshinda zabuni hiyo, tangu tangazo la zabuni lilipotolewa hadi Januari 6 mwakani.

"Mdaiwa kiasi anachodaiwa kinafungiwa hadi mteja anipe rukhsa. Ninauza mtambo huu kwa zabuni tangu siku nitoe tangazo hadi Januari 6 mwaka 2023 kulingana na watuma maombi wenye nia ya kununua mtambo huu," alisema wakili huyo. Pia alisema itatolewa nafasi kwa mnunuzi yeyote ili kukagua kwa kutumia wataalamu wao, akisema mtambo huo ni sehemu ya mali alizonazo mdaiwa, kufidia deni analodaiwa na benki.

# Mbunge atunukiwa kwa kusimamia maendeleo

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

MBUNGE wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, amesema fedha zinazotolewa na serikali kupitia Mfuko wa Jimbo zitumike kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati alipozungumza na wananchi katika hafla ya kukabidhiwa tuzo ya heshima ya kutambua mchango wake katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo iliyotolewa na asasi ya kiraia ya Tanzania Youth Elite Association.

Mtaturu alisema tuzo hiyo itakuwa chachu kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya serikali kwenye jimbo lake.

"Tuzo hii ni kwa ajili ya wananchi wa Singida Mashariki na Wanaikungi wote, hii tuzo itupe chachu ya kutekeleza zaidi, nikuhakikishie Katibu Mkuu wa TYEC tuzo hii imetuongeza nguvu, kama tulifanya kwa asilimia 10 tutaongeza hadi kufika asilimia 80," alisema.

Mbunge huyo alisema kuwa licha ya kufanya vizuri, bado kuna maeneo kwenye jimbo hilo yanakabiliwa na changamoto za maji, elimu na afya.

"Tutatumia rasilimali vizuri kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa sehemu salama kwa wananchi na tunataka Singida Mashariki kuwa jimbo la mfano kuhakikisha kuwa huduma zinafika kwenye maeneo yote," alisema.

Mtaturu alisema ili kufanikisha hayo, utii, nidhamu na kuunga mkono juhudi za serikali katika kufanikisha maendeleo ndiyo itakuwa silaha itakayotumika kuibadilisha Wilaya ya Ikungi na kuwa ya mfano nchini.

Katibu Mkuu wa Asasi ya Kiraia ya Tanzania Youth Elite Community, Ng'wigulu Shigela, alitaja sifa zinazowafanya wao kuwanutuku viongozi, wadau na wafanyabiashara wanaooneka kuisaidia jamii katika mambo mbalimbali.

"Siyo kila mtu tunamtunuku tuzo hizi, tumekuwa tukiangalia watu wanaokuwa wakifanya kazi kubwa za maendeleo katika jamii pamoja na wale wanaomsaidia Rais," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Richard Rwehumbiza, alisema jamii nyingi hasa ya kitanzania huwa zinaona umuhimu wa kitu pale tu kile kitu au mtu anapoondoka, hivyo akawaomba wadau wengine kuunga mkono juhudi za maendeleo zinazofanywa na mbunge huyo.



Meneja Mkuu wa Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, Cheick Sangare (kushoto), akikabidhi zawadi ya Krismasi kwa mmoja wa wagonjwa waliolazwa katika Hospitali ya Bugarama, Elizabeth Nicolaus (kulia), alipoongoza ujumbe wa baadhi ya wafanyakazi wa mgodi huo kutembelea kituo hicho na kutoa zawadi mbalimbali jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC Masasi asimikwa kiongozi mkuu wa kimila

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MKUU wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, amesimikwa rasmi cheo cha kiongozi mkuu wa kimila wa wilaya hiyo ambaye kwa sasa atatambulika kwa jina la Apia Mwene (Mwenye Mwanamke).

Heshima hiyo ya kimila na desturi iliyotolewa na viongozi hao wa kimila wa makabila ya Wamakuwa na Wayao ni sehemu ya kutambua mchango wa maendeleo unaofanywa na mkuu wa wilaya.

Heshima hiyo imelenga kutambua na kuthamini jitihada chanya za maendeleo zinazofanywa na kiongozi huyo katika kuijenga Wilaya ya Masasi na kwa sasa wilaya hiyo imepiga hatua kubwa katika sekta mbalimbali ikiwamo, maji, miundombinu ya barabra, elimu, afya na nishati.

Tukio hilo la kusimikwa limefanyika jana wilayani hapo mbele ya Machifu, Mwamwenye na Ma-Apia Mwene wa katika kikao cha Tathmini ya Mpango ya Maendeleo ya wilaya hiyo kilichoongozwa na mkuu wa wilaya na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa maendeleo. Akizungumza baada ya usimikwaji kwa mkuu wa wilaya, Chifu mkuu wa kimila na desturi Wilaya ya Masasi, Chifu Akaluma, alisema kwa mila na desturi za makabila ya Wamakuwa na Wayao wanapomuona kiongozi yeyote ndani ya eneo husika anafanya mambo mazuri ya maendeleo kwa ajili ya ustawi wa wananchi kiongozi huyo anapaswa kupewa heshima ya kimila.

Alisema kwa heshima ya viongozi wa kimila na desturi wilaya ya Masasi kwa pamoja wameamua kumsimika mkuu huyo kutambua mchango wake wa maendeleo anaoufanya ndani ya wilaya hiyo ikiwa ni pamoja na kuwatambua viongozi hao kimila na kuwashirikisha katika mipango ya mandeleo inayopangwa na kutekelezwa.

"Sisi kama viongozi wa kimila tumeamua kumsimika mkuu wetu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, kama heshima kwake kwa sababu amekuwa mstari wa mbele katika kusukuma maendeleo ndani ya wilaya yetu...tunamshukuru sana," alisema Chifu Akaluma.

Alisema wilaya hiyo imekuwa na maendeleo makubwa yanayosimamiwa na mkuu huyo wa wilaya na amekuwa kiongozi anayeshirikisha wadau mbalimbali ili kupata mawazo ya pamoja katika kuijenga Masasi.

Chifu Akaluma alisema katika sekta ambazo Wilaya ya Masasi zimepiga hatua na kusababisha viongozi hao wa kimila kufarijika nayo ni elimu, afya, barabara, maji na usambazaji wa umeme vijijini jambo ambalo jamii ya Masasi kwa sasa inapata huduma zote za msingi zilizo bora.

Akitoa neno la shukrani kwa viongozi hao wa kimila, mkuu huyo wa wilaya aliwashukuru viongozi hao kwa heshima waliyompatia ya kumsimika kuwa kiongozi wa kimila katika wilaya hiyo kwa cheo cha Apia Mwene.

Aidha, aliwashukuru viongozi hao kwa kutambua uongozi wake na kile anachokifanya kwa ajili ya maendeleo ya Masasi na kwamba ataendelea kushirikisha makundi yote ikiwamo viongozi wa kimila kupanga na kutekeleza mikakati ya maendeleo Masasi.

# Rais Samia atoa zawadi ya Krismasi kwa watoto

**Na Lulu Mussa**, DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amekabidhi zawadi mbalimbali za sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya kwenye kituo cha Safina kilichoko Ntyuka jijini Dodoma kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Zawadi zilizokabidhiwa ni pamoja na mchele, unga wa ngano, sabuni, sukari, mafuta, vinywaji pamoja na mbuzi wawili, Mkuu wa Mkoa akisema zawadi hizo ni kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya watoto katika kipindi hiki cha sikukuu.

Alisema Dk. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametuma salamu za upendo na kuwaomba watoto hao kukua katika maadili ya kumpendeza Mungu na wanadamu.

"Lengo na dhumuni la Mheshimiwa Rais ni kuona watoto wanasherekea sikukuu kwa furaha na amani, kumbukeni kuwa chochote anachokifanya ni kwa ajili ya Watanzania wote ikiwa ni pamoja na ujenzi wa madarasa ili watoto mpate elimu bora na kuongeza kiwango cha utafulu, hivyo mkiwa darasani msikilize mwalimu na mkirudi kituoni muda wa jioni jisomeeni," alisisitiza.

Aliongeza: "Chochote unachokifanya, fanya kwa bidii, kila mtoto ana ndoto na malengo yake ya baadaye. Serikali inatambua mchango wenu ndiyo maana Rais Samia ameamua kutoa zawadi hizi za vyakula na kiasi cha fedha ili wote mfurahie sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya."

Mkuu wa Mkoa aliwashukuru waangalizi wa watoto hao kwa kujitoa kwao kuwalea katika maadili mema na kumwomba Mungu kuendelea kuwabariki walezi na wahudumu wengine katika malezi ya watoto hao.

"Jukumu lenu ni pamoja na kuhakikisha watoto hawa wanasoma ili kuyatumia madarasa yanayojengwa na serikali ili tuwe na kizazi chenye maadili mema ya kitanzania na ndoto za kutimiza malengo ya watoto wetu," aliagiza.

Mlezi wa Kituo cha Safina, Neckson William, aliishukuru serikali kwa kutoa zawadi za sikukuu kwa watoto.

"Tunaishukuru serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutusaidia Kituo cha Safina, tumefurahi sana kwa kuwa tuna watoto ambao pia wapo nje ya Safina. Kituo kina watoto wa kuanzia umri wa miaka miwili na mwaka huu tumefanikwa kupeleka chuo kikuu watoto wawili," alibainisha.

Kituo cha Safina kilianzishwa mwaka 2004 na kina jumla ya watoto 40, wavulana 35 na wasichana watano. Kitua hicho pia kinawasaidia watoto ambao wanatoka katika mazingira magumu.

# DC aagiza mgambo, polisi kudhibiti uhalifu mitaani

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, Abbas Kayanda, ameagiza askari 157 wa Jeshi la Akiba (mgambo) kuungana na Jeshi la Polisi, kuzunguka mitaani kudhibiti uhalifu au uvunjifu wa amani, wakati wa sikukuu za mwisho wa mwaka.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipokwenda kufunga mafunzo ya Jeshi la Akiba katika Uwanja wa Mandela, Manispaa ya Moshi.

"Nendeni mkakabiliane na matukio ya uhalifu na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake, watoto na wazee huko mitaani, kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi ili wananchi waweze kufanya shughuli zao kwa amani na utulivu.

"Kumekuwapo na matukio mengi kwenye jamii ya kihalifu, hivyo ni wakati wa kutokomeza uhalifu huo kwa misingi ya haki. Mkaishi viapo vyenu vya kusimamia haki, uwajibikaji na uzalendo. Kaweni mfano wa kuigwa, huku mkijitahidi kuifundisha jamii mienendo yenu mema mliyoipata huku. Hatutegemei kuwaona nyinyi ndiyo wa kwanza kufanya matukio ya uhalifu,"alisema.

Mshauri wa Jeshi la Akiba wa Wilaya ya Moshi, Luteni Kanali, William Mgayo, alisema askari hao wa mgambo wamepata mafunzo mbalimbali, ikiwamo mbinu za kivita, silaha, usomaji wa ramani na sheria za jeshi, ambazo zitawasaidia kuwa raia wema na kulisaidia taifa kwa uzalendo wao.

Akisoma risala ya wahitimu wa mafunzo hayo, Neville Mtenga, alisema tatizo walilonalo kwa sasa ni kukosekana kwa sare za jeshi hilo, hivyo wanaomba Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na serikali kuona namna ya kusaidia upatikanaji wa sare hizo.

Wakati huo huo, askari wa Jeshi la Polisi katika Mkoa wa Kilimanjaro wamenufaika na mfumo maalum wa closed user group (CUG) unao wawezesha kufuatilia mienendo na taarifa za kiuhalifu.

Wanaonufaika zaidi na mfumo huo ulioratibiwa na Jukwaa la Maendeleo la Mkoa wa Kilimanjaro (KDF) kwa ubia na Kampuni ya Simu za Mkononi ya Vodacom ni maofisa, wakaguzi na askari Polisi 1,504.

KDF na Vodacom, wameingia makubaliano ya kuwapa polisi wa Mkoa wa Kilimanjaro na wafanyakazi wote wa jeshi hilo, namba mpya za simu ili waweze kuwasiliana bure na hakuna atakayeingia gharama ya kuwasiliana na polisi



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera (kushoto), akikabidhiwa vifaa vya kuwasaidia wanawake kujifungua kwa usalama 100 vya Sh. milioni 2.8 kwa kituo cha afya Mirerani vilivyonunuliwa na mchimbaji madini ya Tanzanite, Charles Mullo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mifumo ya ikolojia ya mito, maziwa hatarini kutoweka

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

HALI ya binadamu na wanyamapori kutumia chanzo kimoja cha maji inatishia ustawi wa mifumo ikolojia ya Mto wa Mbu, Longido na Ziwa Natron iliyoko Mkoa wa Arusha, ikiwamo uvutiaji wa biashara ya uwindaji wa kitalii.

Maeneo yaliyoathirika zaidi kwa kunyang'anyana maji ni Bwawa la Kiseriani lililoko katika Pori Tengefu la Ziwa Natron na Chemichemi ya Kimokoa iliyoko chini ya Mlima Longido, ambayo wananchi wake wamekuwa wakiwazuia wanyamapori kwenda kunywa maji.

Inaelezwa kuwa sababu kubwa ni wafugaji wamekuwa wakitegemea eneo hilo kulisha mifugo yao na mgongano mwingine wa binadamu na wanyamapori kugombea maji, uko katika eneo la Tingatinga.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalumu kuhusiana na athari za mabadiliko ya tabianchi namna yanavyoathiri shughuli za uwindaji wa kitalii, Kamanda wa Mifumo Ikolojia ya Mto wa Mbu/Longido/Lake Natron, Augustino Ngimilanga, alisema Desemba 11, mwaka huu, mfugaji wa jamii ya Kimasai alifariki katika Kijiji cha Tingatinga, Wilaya ya Longido kutokana na kuzuia tembo wasinywe maji.

"Yaani binadamu anazuia tembo wasinywe maji kwa ajili ya mifugo yake, lakini tembo anaona njia rahisi ya kupata maji ni vurugu, ambayo imesababisha kifo cha huyo mfugaji wa Tingatinga. Tingatinga kuna kitalu cha uwindaji (Enduimet WMA Hunting). Sasa Desemba 11, mwaka huu tembo walikuwa wameenda kunywa maji jirani na maboma ya wafugaji, kwa bahati mbaya mfugaji mmoja mwenye eneo ambalo liko karibu na maji, alijaribu kwenda kuwafukuza hao tembo, hakujua kulikuwa kuna kundi kubwa kiasi gani la tembo.

Mifumo hiyo ya ikolojia ya Mto wa Mbu/Longido/Lake Natron, ambayo ni maarufu kwa uwindaji wa kitalii na utalii wa picha, iko chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori nchini (TAWA).

Aidha, katika Pori la Akiba la Longido Game Controlled Area, alisema nako pia kuna tatizo kama hilo eneo la Kimokoa, chini ya Mlima Longido, ambako kuna chemichemi za maji na wananchi wamekuwa wakiwazuia wanyamapori kwenda kunywa maji, kwa sababu wao wamekuwa wakilisha mifugo yao.

Mapori hayo yako katika wilaya tatu za Mkoa wa Arusha za Longido, Monduli na Ngorongoro. Yalianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mimea na Wanyamapori, wakati huo ikitwa Fauna and Flora Audience ya Mwaka 1951, na yaliendelea kutambuliwa kwa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Namba 12 ya Mwaka 1974.

Baadaye yakaendelea kutambuliwa na Sheria ya Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009, kwa Tangazo la Serikali Namba 269 la Mwaka 1974 na kwa sasa yana jumla ya vitalu saba vya uwindaji wa kitalii.

# Shirika la Tusonge CDO kupambana na mabadiliko tabianchi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TISHIO la mabadiliko ya tabianchi yanayosababishwa zaidi na shughuli za binadamu na mkusanyiko wa gesi ukaa kwenye mazingira, ambalo linachagizwa na wastani wa kiwango cha joto, kimeligusa Shirika la Maendeleo la TUSONGE CDO kuahidi kujikita kukabiliana na hali hiyo katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha.


Athari na madhara ya mabadiliko ya tabianchi kwa sasa ni ongezeko la nyuzijoto kuongezeka kwa kasi na hali ya matukio mabaya ya hali ya hewa, kuanzia kwa mawimbi ya joto, ukame, mafuriko, dhoruba za msimu wa baridi, vimbunga na mioto ya mwituni.

Akizungumza juzi katika Mji wa Moshi, wakati wa mkutano wa 11 wa shirika hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa TUSONGE CDO, Aginatha Rutazaa, alisema katika utendaji wao mwaka ujao kuna mambo hawawezi kuyaacha ambayo yamejitokeza mwaka huu.

"Kwa hiyo tunawajibu wa kuangalia kwamba kule tunakokwenda, tunakwenda kufanya nini na majibu hayo wote mnayo. Kwa sababu kila mtu kwenye kijiji chake, kwenye familia yake, kwenye eneo lake, kuna mambo anayoyaona kwamba kama nitaweza kuyafanya kwa mwaka 2023, yanaweza yakawa na tija kubwa katika maisha yangu, maisha ya familia yangu na maisha ya kijiji au jamii inayonizunguka.

Kwa mujibu wa Rutazaa, wanaamini kwamba watakwenda kuchangia kuondoa adha hizo kwa pamoja wakishikamana kwenda kupunguza chachu ya makali ya maisha ndani ya jamii inayowazunguka wanakotekeleza miradi yao.

Novemba mwaka huu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, alinukuliwa akisema Tanzania itatekeleza kwa vitendo mwaka ujao maazimio ya mkutano wa wanachama wa Umoja wa Mataifa, kuhusu mabadiliko ya tabianchi.



## Arusha wakamilisha ujenzi wa madarasa, mabweni

**Novatus Makunga,** ARUSHA

MKOA wa Arusha umekamilisha kwa asilimia 100 ujenzi wa madarasa 258 na mabweni mawili yaliyojengwa na serikali kwa kutumia fedha za Mpango wa Maendeleo ya Ustawi wa Taifa na Mapambano ya Uviko-19, Sh. bilioni 5.36.

Akitangaza jana kukamilika kwa miradi hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alisema tayari amepokea madarasa 17 vya Halmashauri ya Meru ikiwa ni sehemu ya vyumba hivyo.

Mongella alisema kuwa Mkoa wa Arusha ulipokea fedha hizo Agosti mwaka huu na ulielekezwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), uwe umekamilisha vyumba hivyo kabla ya Januari 2023, kwa ajili ya kuwapokea wanafunzi wapya wa kidato cha kwanza.

"Sisi katika Mkoa wa Arusha tulipeana maelekezo mpaka katikati ya Desemba mwaka huu, madarasa yote yawe yamekamilika. Tulikuwa na fatiki ya kufuatilia mara kwa mara miradi hii katika wilaya zote za mkoa wetu na ujenzi umekwenda vizuri," alisema.

Aliongeza kwamba ujenzi huo umefanywa na mafundi jamii wa maeneo husika, wakisimamiwa na kamati za ujenzi za shule pamoja na wahandisi wa ujenzi katika Halmashauri za Wilaya na Jiji la Arusha.

Baada ya kukamilika kwa miradi hiyo, Mongela, aliwaagiza viongozi wa Wilaya za Monduli, Longido, Ngorongoro, Karatu na Arusha, kuendelea na mchakato wa kuyapokea madarasa hayo katika maeneo yao na kuendelea na matayarisho ya kuanza kwa muhula wa masomo wa mwaka 2023.

Aidha, aliwahakikishia wazazi wenye watoto 13,400 waliochaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza Januari mwakani kuwa watoto wote wataanza kwa pamoja, kwamba hakuna wanafunzi watakaoingia kwa awamu.

Katika makabidhiano hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Zainab Makwinya, alisema Sh. milioni 340, zimetumika katika ujenzi wa vyumba vya madarasa 17.

# Machinga mpakani waomba kuondolewa vikwazo

**Na Woinde Shizza,** MKINGA

WAFANYABIASHARA wadogo wanaofanya shughuli zao za kibiashara katika mpaka wa Horohoro na Lungalunga, unaozitengenisha Tanzania na Kenya wamewaomba wakuu wa nchi hizo kuendelea kuondoa vikwazo vya kibiashara ili kuwawezesha wananchi wengi kuchangamkia fursa za kiuchumi.

Ombi la wafanyabiashara hao limekuja wakati mataifa hayo yakiwa yamekamilisha mradi wa ujenzi wa miundombinu ya Barabara ya Tanga/Horohoro, inayojengwa kwa ufadhili wa Hisani ya Watu wa Marekani, kupitia miradi ya milenia.

Wakizungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti baadhi ya wafanyabiashara akiwamo Joseph Mwanganya, kutoka Kaunti ya Lungalunga nchini Kenya, alisema licha ya nchi hizo mbili kuwa na miundombinu bora mipakani, bado wanakwama kufikia malengo yao ya kibiashara kutokana na kuwapo kwa baadhi ya vikwazo vya kibiashara.

"Moja ya vikwazo hivyo ni kupitisha mifugo na baadhi ya biadhaa za ndani zinazozalishwa katika kila nchi, ndiyo maana tunawasihi Rais Samweli Ruto (Kenya) na Samia Suluhu Hassan (Tanzania), kuendelea kupunguza vikwazo vya kibiashara ili biashara iwe rahisi zaidi kupitisha kutoka nchi moja hadi nyingine.

Zaidi Mwanganya alieleza: "Sisi tunataka uhuru wa kufanya biashara hasa hizi ndogo, turuhusiwe kupita mipakani na kupitisha biashara mazao ya mifugo na mifugo."

Aidha, mfanyabiashara na mkazi wa Duga Maforoni, Wilaya ya Mkinga mkoani Tanga, Zahoro Juma, alisema kwa sasa upande wa Tanzania biashara zimeimarika sana kutokana na uwapo wa barabara nzuri ambayo inarahisisha usafirishwaji wa bidhaa mbalimbali.

"Kuna vikwazo vidogo vidogo vya kiforodha, lakini kubwa biashara zinakwenda vizuri hivi sasa kutoka Tanga hadi Horororo, unatumia saa moja kusafiri, tofauti na miaka ya nyuma tulikuwa tunatumia saa sita, kwa kilomita 65 tu kufika Horohoro kutoka Nairobi, Kenya," alisema.

Akizungumzia mkakati wa serikali, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omary Mgumba, alisema serikali inajitahidi kupunguza vikwazo kwa wafanyabiashara wadogo katika mpaka huo na biashara zimeimarika sana tofauti na miaka ya nyuma.

Alisema: "Tunawaruhusu kufanyabiashara kilometa 10 ndani ya Tanzania na Kenya bila vikwazo. Hivi sasa miundombinu imeimarika hasa barabara, kwa hiyo ni fursa kwa wafanyabiashara wadogo kuitumia na serikali imetenga maeneo ya uwekezaji".



Meneja wa RUWASA Mkoa wa Tanga, Mhandisi Upendo Lugongo, akipanda juu ya tangi la maji lililojengwa kwenye Kata ya Ngulwi, Wilaya ya Lushoto juzi, alipotembelea kukagua miradi ya maji ambayo itagharimu zaidi ya Sh. milioni 578. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Madiwani watafuta dawa wazazi wakaidi kuchangia chakula shuleni

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MADIWANI wa Halmashauri ya Jiji la Tanga wameanza kutafuta mwarobaini wa tatizo la baadhi ya wazazi na walezi, kugomea kuchangia chakula cha wanafunzi katika shule za msingi.

Wamesema hakuna atakayekwepa jukumu hilo, kwa kuwa suala la afua za lishe ni mkakati wa kitaifa. Akizungumza katika kikao kazi cha kamati ya lishe cha wilaya hiyo, Naibu Meya wa Jiji hilo, Mwanaidi Chombo, alisema ili kudhibiti tatizo hilo lisiendelee kuota mizizi madiwani wote wamekubaliana kutekeleza mpango mkakati wa kusisitiza masuala ya lishe kila kitongoji, kijiji, mtaa na kata.

"Kama halmashauri, madiwani tunakuja kivingine. Halmashauri yetu imejiwekea mpango mkakati wa kuhakikisha kila mwanafunzi shuleni anapata chakula ili kuinua kiwango cha ufaulu.

"Ninavyozungumza nanyi ni kwamba tayari madiwani, tumeanza kutekeleza mkakati huo kwa kukutana na kutoa elimu ya lishe kwa wananchi, juu ya umuhimu wa wanafunzi kupatiwa chakula wakiwa shuleni," alisema Chombo.

Naibu Meya huyo alisema wanalazimika kuingia mtaani kutoa hamasa hiyo kwa kuwa lishe shuleni ni suala la kitaifa, hivyo inawapasa kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye alitia saini mikataba ya lishe kwa niaba ya Watanzania.

"Hivyo hatuna budi kwenda kutoa elimu kwa wazazi na walezi ili waweze kuchangia chakula shuleni na wanafunzi waweze kukaa muda wote wa mchana wakiendelea na masomo yao. Hii itapunguza sana utoro, lakini itaongeza ufaulu kwa wanafunzi." Ofisa Lishe wa Halmashauri hiyo, Salina Mustafa, wakati akiwasilisha mada juu ya umuhimu wa chakula shuleni, alitaja faida za lishe kwa wanafunzi kuwa ni pamoja na wanafunzi hao kujifunza vizuri.

Alisema chakula kinapoandaliwa shuleni kinakuwa katika hali ya usalama, lakini wanafunzi wanakula kwa muda muafaka, wanapata ari ya kuwahi shuleni wakiamini muda wa wao kupata chakula ukifika wanakipata shuleni.

Alisema: "Wanafunzi wanaopata chakula shuleni wanakuwa rahisi kuelewa na kujifunza. Uwapo wa chakula shuleni huongeza vichocheo vya kuamsha ari ya kuwahi na kuhudhuria shule na pia kupenda kusoma na hupunguza utoro, hasa shule za kata ambazo hazina uzio."

# Nipashe Spotika



ZIJUE IMANI ZA KISHIRIKINA KWENYE SOKA DUNIANI UK.16 - 17



## ISIKUPITE

Ronaldinho, Kylian Mbappe, Lionel Messi, wote wametwaa Kombe la Dunia mwaka unaofuata baada tu ya kuijunga na Paris Saint Germain. Ronaldinho alitua PSG 2001, mwaka 2002 akatwaa Kombe la Dunia, Mbappe (PSG - 2017) mwaka 2018 akabeba Kombe la Dunia, Messi (PSG - 2021), mwaka 2022 amebeba Kombe la Dunia.

## MTIFUANO...

Mshambuliaji wa Manchester City, Erling Braut Haaland, akiruka kihunzi dhidi ya beki wa kati wa Liverpool, Nathaniel Phillips, kwenye mechi ya Kombe la Carabao iliyopigwa Uwanja wa Etihad wiki iliyopita na City kuibuka na ushindi wa mabao 3-2. **PICHA: MTANDAO**



MARTINEZ

# MAKIPA 5-BORA KOMBE LA DUNIA LA FIFA 2022

**DOHA,** Qatar

MICHUANO ya Kombe la Dunia ya FIFA ya 2022, iliyochukua muda wa wiki sita imefikia kikomo na imedhihirika kuwa ni timu gani bora zaidi. Kuanzia Novemba 20, timu 32 zilichuana vikali katika mashindano hayo ya kifahari nchini Qatar. Kila timu ilileta wachezaji wake bora na waliwakilisha timu zao kadri walivyoweza.

**Katika kila mashindano, mtu anayelinda nyadhifa ni mmoja wa washiriki muhimu wa kila timu. Kipa mzuri anaweza kuwa tofauti kati ya mafanikio na kushindwa kwa timu katika mashindano kama Kombe la Dunia.**

Makala haya yatawaangazia makipa watano ambao wamejizolea umaarufu mkubwa ndani ya wiki sita zilizopita kutokana na uchezaji wao nchini Qatar. Bila kuchelewa, hapa kuna orodha ya makipa watano bora kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022...

**#5. Jordan Pickford (England)**

Mlinda mlango wa Uingereza, Jordan Pickford, amekuwa mmoja wa wachezaji bora katika nafasi yake kwenye Kombe la Dunia nchini Qatar. Mchezaji huyo wa Everton alikuwa na kiwango bora kabisa.

Pickford alianza mechi zote za England katika dimba hilo huku wakiangukia katika hatua ya robo fainali, na kufungwa na Ufaransa. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alikuwa katika toleo lake la pili la Kombe la Dunia na alifungwa mabao matatu katika mechi tano.

Pickford aliokoa jumla ya mabao saba katika mechi zake tano kwenye michuano hiyo. Alikuwa wa kuvutia kwa 'Simba Watatu' hao katika mbio zao za robo fainali.

**#4. Wojciech Szczesny (Poland)**

Mchezaji bora zaidi katika hatua ya makundi, Wojciech Szczesny, alikuwa mmoja wa makipa bora wa mashindano hayo. Kipa huyo wa Poland aliichezea nchi yake vema walipotoka katika hatua ya 16-bora.

Szczesny ndiye aliyekuwa chaguo bora zaidi katika goli la Poland kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022. Mchezaji huyo wa Juventus alifungwa mabao mawili katika mechi nne alizocheza na timu yake ya taifa kwenye michuano hiyo. Hasa zaidi, aliokoa penalti dhidi ya Saudi Arabia na Argentina katika hatua ya makundi. Ni Ufaransa na Argentina pekee ndio waliweza kumfunga.

Szczesny aliokoa jumla ya hatari 23 katika mechi zake nne alizocheza kwenye mashindano hayo. Kipa huyo mzoefu alichangia kwa kiasi kikubwa kuiongoza nchi yake kwenye hatua ya mtoano kabla ya kuambulia kipigo kwa Ufaransa.

**#3. Yassine Bounou (Morocco)**

Yassine Bounou mzaliwa wa Canada alikuwa mmoja wa makipa bora kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022. Alikuwa langoni kwa timu ya Morocco ambayo ilishangaza kwenye mashindano hayo, huku wakimaliza katika nafasi ya nne baada ya mbio za kihistoria.

Bounou alifungwa mabao matatu katika mechi sita alizochezea Morocco kwani alicheza mechi zote isipokuwa moja tu. Kipa huyo wa Sevilla alitoa maonyesho kadhaa ya ubora kwa nchi yake huko Qatar. Kiwango chake bora, bila shaka, kilikuwa dhidi ya Hispania katika hatua ya 16-bora ambapo aliokoa penalti tatu kwenye mikwaju hiyo.

Bounou aliisaidia Morocco kuwa na kiwango bora dhidi ya Croatia, Hispania na Ureno, timu tatu bora katika soka la Ulaya. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, alikuwa nguzo muhimu kwa Morocco.

**#2. Dominik Livakovic (Croatia)**

Mnamo 2018, Danijel Subasic alikuwa muhimu kwa mbio za kihistoria za Croatia hadi fainali. Mwaka huu, Dominik Livakovic alichukua jukumu hilo kikamilifu na bila shaka alimshinda mtangulizi wake kwenye hatua kubwa kuliko zote.

Kipa wa Dinamo Zagreb, Livakovic alifungwa mabao mawili katika mechi saba za Kombe la Dunia na kuiongoza timu yake kumaliza katika nafasi ya tatu. Alionyesha darasa lake katika hali zote za ndani ya mchezo na mikwaju ya penalti. Aliokoa jumla ya penalti nne katika mikwaju ya penalti katika mashindano hayo, sawa na rekodi iliyowekwa na Subasic mnamo 2018.

Livakovic aliokoa mabao 25 kutokana na mikwaju 31 aliyokabiliana nayo, na kuzuia asilimia 80 ya mashuti aliyokumbana nayo yasiingie wavuni.

**#1. Emiliano Martinez (Argentina)**

Emiliano Martinez wa Argentina alikuwa mlinda mlango bora wa Kombe la Dunia. Mchezaji huyo wa Aston Villa alichangia kwa kiasi kikubwa katika mbio za nchi yake kupata ushindi katika michuano hiyo nchini Qatar.

Martinez alitunukiwa tuzo ya shindano ya Golden Glove. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, alicheza mechi nyingi za kiwango cha juu nchini Qatar, lakini ushujaa wake wa mikwaju ya penalti dhidi ya Uholanzi katika robo fainali na Ufaransa kwenye fainali ulijitokeza kwa wengi.

Aliokoa penalti mbili za kwanza za Uholanzi kutoka kwa Virgil Van Dijk na Steven Berghuis. Pia alidaka ya Kingsley Coman kwenye fainali.

Martinez alilazimika kuokoa mara saba pekee kwenye michuano hiyo, lakini ameokoa mabao machache muhimu. Uokoaji wake wa mwisho kwa kumnyima Garang Kuol katika dakika za mwisho za raundi ya 16 uliisaidia Argentina kushinda changamoto ya Australia. Pia aliokoa hatari kubwa ya kumnyima Randal Kolo Muani katika hatua za mwisho za fainali.

# SABABU 3 KWA NINI BELLINGHAM ATAAMUA KUTUA LIVERPOOL




**LONDON,** England

LIVERPOOL kwa muda mrefu imekuwa ikitajwa kuvutiwa na Jude Bellingham pamoja na Manchester City na Real Madrid. Lakini je, nafasi ya Liverpool ina uhalisia kiasi gani linapokuja suala la kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Uingereza mwenye umri wa miaka 19?

**Ripoti zinaonyesha kuwa familia ya Bellingham inapendelea ahamie Anfield na inalenga kufanya uhamisho huo ufanyike msimu ujao wa majira ya joto.**

Licha ya ada ya uhamisho ya pauni milioni 100 kutajwa, kuna uwezekano mkubwa kwamba Liverpool wanaweza kupata kipaji hicho dhidi ya wapinzani wao wa Premier League, Manchester City na miamba ya Uhispania, Real Madrid.

Hapa kuna sababu tatu kwa nini mashabiki wa Liverpool wanaweza kuwa na matumaini...

**#1. Kusimama kama mchezaji nyota**

Liverpool wamekuwa wakikabiliwa na masuala ya kiungo wa kati msimu mzima na wamekuwa wakimlilia mchezaji mwenye ubora wa kweli katikati ya uwanja.

Si hivyo tu, lakini safu ya kiungo imeanza kuzeeka vibaya - Henderson ana umri wa miaka 32, Thiago ana miaka 31, Milner anakaribia kufikisha miaka 37 na Fabinho Oktoba atafikisha miaka 30.

Hii inasababisha maumivu makali ya kichwa kwa Jurgen Klopp kwani Mjerumani huyo anatazamia kuunda safu ya kiungo imara kwa miaka mingi ijayo.

Mandhari ya Manchester City na Real Madrid, hata hivyo haiwezi kuwa tofauti zaidi. Manchester City wana utajiri katika safu yao ya kiungo, wakiwamo Kevin de Bruyne, Bernardo Silva, Ilkay Gundogan, Rodri na Kalvin Phillips.

Kadhalika, Real Madrid ina wataalamu wenye uzoefu, Luka Modric na Toni Kroos ambao wanazeeka pia, lakini wanaimarishwa na wanaoanza kuchipukia Aurelien Tchouameni, Eduardo Camavinga na Federico Valverde.

Ni sawa kusema kwamba Bellingham hatajitokeza wala kuleta mapinduzi katika safu zao za kati. Akiwa Liverpool hata hivyo, angejitokeza kama nyota kwenye jukwaa la dunia na kuwa mtu muhimu katika kusaidia kubadilisha maisha ya Liverpool.

Kama Jurgen Klopp alivyowahi kusema kuhusu Philippe Coutinho: “Nilimwambia kaa hapa na watahitimisha kwa kujenga sanamu kwa heshima yako. Nenda mahali pengine, Barcelona, Bayern Munich, Real Madrid, na utakuwa mchezaji mwingine tu. Hapa unaweza kuwa kitu zaidi.”

Kwa upande wa Countinho, Klopp hangeweza kuwa sahihi zaidi.

**#2. Urafiki na wachezaji wa sasa wa Liverpool**

Jambo moja lililodhihirika wazi wakati wa kampeni za Kombe la Dunia za England ni jinsi Jude Bellingham alivyokuwa karibu na wachezaji wawili wa Liverpool Trent Alexander-Arnold na nahodha wa Liverpool, Jordan Henderson.

Kulikuwa na picha nyingi zilizotolewa za watatu hao wakiwa pamoja wakati wa mazoezi, lakini urafiki wao nje ya uwanja ndio uliovutia macho. Kwa hakika, Alexander-Arnold alichapisha picha akiwa na Bellingham kwenye akaunti yake ya Instagram walipokuwa wakipiga “wakitembea mjini” jioni moja huko Qatar.

Bila shaka hii haihalalishi kwamba bidhaa hii ya akademi ya Birmingham City itachagua Liverpool kwa sababu ni marafiki na baadhi ya wachezaji wa kikosi hicho. Walakini, hili hakika litakuwa jambo muhimu kwa Kinda huyo Mwiingereza anapofikiria jinsi anavyoweza kutulia katika kwa kila klabu.

Furaha nje ya uwanja ni muhimu sawa na furaha ndani yake na kuwa na marafiki kama Alexander-Arnold na Henderson kutasaidia sana kumshawishi Bellingham kwamba mustakabali wake wa muda mrefu uko Anfield.

**#3. Kufuata nyayo za Steven Gerrard**

Bellingham hajaficha jinsi anavyovutiwa na nahodha wa zamani wa Liverpool, Steven Gerrard.

Kijana huyo ametaja mara nyingi kabla kwamba Gerrard alikuwa mfano wake wa kuigwa wakati akikua na hata amehifadhi sehemu za michezo yake.

Kwa hivyo, akiwa na umri wa miaka 19 tu, Bellingham ana nafasi nzuri ya kumuiga nahodha huyo wa zamani wa Liverpool na kuwa gwiji wa safu ya kiungo ya Liverpool. Huku mkataba wa Naby Keita ukiisha msimu ujao wa majira ya joto, jezi namba 8 ambayo Gerrard alikuwa maarufu kwa miaka mingi sana itapatikana hivi karibuni.

Fursa ya kuchukua jezi ya mfano wake wa kuigwa utotoni pale Anfield inawakilisha matarajio ya kuvutia sana kwa kiungo huyo wa kati wa Borussia Dortmund na inaweza kuwa ngumu sana kupinga.

**NJE YA UWANJA**

FAINALI za Kombe la Dunia la Fifa nchini Qatar 2022, zimeweka rekodi ya mabao mengi zaidi kufungwa (172), zikifuatiwa na zilizofanyika Brazil 2014 (171) na zile za Ufaransa 1998 (171), Urusi 2018 (169), Korea na Japan 2002 (161) na Ujerumani 2006 (147).



# ZIJUE IMANI ZA KISHIRIKINA KWENYE SOKA DUNIANI



RONALDO

**LONDON,** England

TUMESIKIA mashabiki wakiwa na imani potofu tofauti kabla, wakati na hata baada ya michezo na haipaswi kushangaza kwamba hata wachezaji, mameneja, na marais wa timu wana yao.

**Imani ya mwisho au dhana kwamba matokeo fulani au matukio yanaweza kuathiriwa na nguvu zisizo za kawaida ambazo ziko karibu nasi na zinaweza kushawishi uamuzi wa mtu, inaweza kuonekana kuwa ya ajabu kwa baadhi ya watu. Lakini ushirikina na mila mara nyingi zaidi zimekita mizizi na kuwekezwa katika historia ya timu au hata katika utambulisho wa mtu binafsi.**

Makala haya yanaangalia matukia kadhaa yanayofanywa na wachezaji, makocha na viongozi wa timu ambayo yanaashiria imani potofu za kishirikina.

### Cristiano Ronaldo

Mshindi mara tano wa Ballon d'Or na mmoja wa wachezaji wakubwa wa wakati wote, hilo ndilo linalokujia akilini unaposikia jina la Cristiano Ronaldo. Kwa hivyo wakati mazungumzo ya ushirikina yanapokuja na wachezaji na mbinu yao wenyewe ya kile kinachoweza kuwafanya wawe bora.

Hata hivyo, kwa miaka yake kama mwanamichezo wa kulipwa, Ronaldo amekuza mambo fulani ambayo yamekuwa ni kama ya kishirikina. Kutoka kuwa mchezaji wa kwanza kushuka akiwa anasafiri kwa mchezo kwa ndege, akiweka mguu wake wa kulia kwenye nyasi kwanza, akisimama kwa njia ile ile wakati wa mipira ya adhabu na mengine mengi.

Zote zinaonekana zimefanya kazi, kwani nyota huyo wa Ureno ana mataji matatu ya Ligi Kuu, matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, mawili ya LaLiga, moja la Serie A, taji moja la Euro na bila shaka, tuzo tano za Ballon d'Or.

### Ufaransa 1998

Ingawa walitinga fainali ya Kombe la Dunia kwa ustadi na vipaji vya wachezaji kwenye timu yao, ni nani anayeweza kusema kwamba kile walichokifanya kabla ya mechi hakijasaidia kazi yao. Wafaransa hao walikuwa na kikosi cha nyota cha Kombe la Dunia, pamoja na Zinedine Zidane, Marcel Desailly, Didier Deschamps, Emmanuel Petit na chipukizi Thierry Henry.

Lakini licha ya hayo yote, wao, au tuseme Laurent Blanc, walikuwa na ibada ya kufurahisha ya kabla ya mechi, ambapo beki angembusu kichwa kilichonyolewa cha kipa Fabien Barthez. Na ushindi ulipoongezeka, ndivyo idadi ya mabusu iliongezeka na mwishowe, Blanc aliifanya timu nzima ya Ufaransa kumbusu kichwa cha kipa huyo mwenye umri wa miaka 26, wakati huo kutoka kwa wachezaji wa akiba hadi makocha, wote walienda hadi kwa Barthez na kumbusu kichwa.

### Romeo Anconetani

Mojawapo ya imani potofu za ajabu kwenye orodha hii, rais wa zamani wa AC Pisa, Romeo Anconetani, mwanasoka na kocha wa zamani wa Italia, alitumia chumvi tu uwanjani kwa sababu alidhani ingeisaidia timu yake. Kadiri mchezo ulivyokuwa mkubwa ndivyo chumvi inavyokolea uwanjani!

Romeo Anconetani hakuwa tofauti na alitenda sawasawa na Waitaliano wengine ambao waliamini kwamba hata kucheza kamari dhidi ya timu yao kungeongeza nafasi za bahati nzuri zaidi. Bado, labda rais wa AC Pisa alienda mbali sana.

Wakati wa mechi muhimu dhidi ya Cesena, rais huyo wa zamani aliingia uwanjani na alikwenda uwanjani na kuweka chuvi kwenye kona nne za uwanja.

### Pele

Kwa urahisi, mmoja wa wachezaji bora zaidi wa wakati wote, gwiji wa Brazil na mmoja wa wafungaji mabao bora zaidi naye yupo kwenye orodha hii ya ushirikina. Wakati wa hali duni katika kipindi chake cha uchezaji mshambuliaji huyo alihusisha na jezi ambayo alikuwa amempa shabiki baada ya mechi. Gwiji huyo wa Brazil aliendelea kumtuma rafiki yake kwa misheni ya kufuatilia jezi hiyo.

Kama bahati ingekuwa hivyo, rafiki huyo alifaulu kufuatilia jezi hiyo na kuirudisha kwa Pele, ambaye kiwango chake cha ufungaji kilirejea baada ya muda mfupi. Lakini rafiki huyo aliacha kutafuta jezi hiyo na badala yake alimpa mshindi huyo mara tatu wa Kombe la Dunia jezi aliyoitumia kwenye mechi iliyopita.

Imani kwamba jezi ilikuwa zaidi ya kutosha kwa hadithi ya Brazil, na kiwango chake.

### Raymond Domenech

Raymond Domenech alikuwa kocha wa Ufaransa na anajulikana kwa mikwaruzano yake na Patrick Vieira, David Trezeguet na hata kumtoa Karim Benzema kwenye kikosi chake.

Domenech alikuwa na tatizo hasa la kutowataka wachezaji wenye nyota ya nge katika vikosi vyake, akiwataja kama wazembe, wasioaminika, wasumbufu na wanaotafuta umakini.

## Nukuu

"Ninatumai fainali zijazo za wanaume za Kombe la Dunia mwaka 2026 zitakazoshirikisha timu 48 badala ya 32, India ina nafasi ya kufuzu, nini ninachokitaka kuwahakikishia mashabiki wa India ni kwamba tunawekeza sana India kulifanya soka la India kuwa kubwa. Nchi kubwa kama hiyo inahitaji ushindani mkubwa katika soka pamoja na timu kubwa ya soka, hivyo tunalifanyia kazi hilo," **Gianni Infantino, Rais wa Fifa.**



"Desemba 18, 2022. Leo Messi mwenye umri wa miaka 34, atashinda Kombe la Dunia na kuwa mchezaji bora zaidi wa wakati wote. Nitazame miaka saba iliyopita," **Injinia wa Kimarekani, Jose Miguel Polanco, ambaye amejizolea umaarufu baada ya miaka saba iliyopita (mwaka 2015) kutabiria Argentina na Messi watatwaa Kombe la Dunia 2022.**



"Messi [Lionel], ameshinda Kombe lake la kwanza la Dunia, kama historia yake inavyostahili. Rafiki yangu mpendwa, Mbappe, akifunga mabao manne kwenye fainali. Ilikuwa ni zawadi gani kutazama tamasha hili la mustakabali wa mchezo wetu. Na nisingeweza kushindwa kuipongeza Morocco kwa kampeni ya ajabu. Ni vema kuona Afrika iking'ara," **Salamu za Gwiji wa Brazil, Pele kwa Argentina baada ya kutwaa Kombe la Dunia Qatar 2022.**





# MANDONGA NA USIKU WA MABINGWA ARUSHA

**Na Saada Akida**

MASIKIO na macho ya wakazi wa Arusha na vitongoji vyake na hata Tanzania kwa ujumla yataelekezwa katika 'derby' ya ngumi kati ya mafahari wawili kutoka Kata ya Manzese, Iddi Pialali akizipiga na Mfaume Mfaume kutoka Kata ya Mabibo.

**Pambano hili linafanyika leo usiku katika Ukumbi wa ICC Lake Nyasa ulioko jiji hilo la baridi huku likisindikizwa na jumla ya mabondia 10 watakaopanda ulingoni kuonyeshana ubabe siku hiyo iliyopewa jina la 'Usiku wa Mabingwa'.**

Katika mapambano hayo 10, tisa yatakuwa ya utangulizi ambayo yatawakutanisha mabondia Hamad Furahisha, Zawadi Kutaka, Hassan Ndonga, Haidary Mchanjo, Halima Vunja Bei, Sylvester Urio, Karim Mandonga na Ramadhani Kumbele.

Mabondia hao watausindikiza usiku huo wa Mfaume na Pialali huku bondia mwenye vituko na mbwembwe nyingi, ambaye ameibuka kuwa kivutio kwa Watanzania, Karim Mandonga akizichapa dhidi ya Ali Baba.

Mapambano hayo ya Usiku wa Mabingwa ambayo yatafunga mwaka 2022 na kuukaribisha 2023 kibabe yatakuwa chini ya Promota wa Ngumi za kulipwa nchini, Selemani Semunyu.

Semunyu ni miongoni mwa wadau wa masumbwi waliomwibua Mandonga huko kwao Morogoro alipokuwa akiishi na kumleta katika ngumi, ambapo amekuwa kivutio kikubwa katika mchezo namba mbili nchini kwa kuwa na mashabiki wengi baada ya soka.

Mandonga amekuwa maarufu na kuvutia watu wengi kupenda masumbwi kutokana na mikwara yake anayoonyesha kabla ya pambano licha ya kwamba zaidi ya mara mbili zilizopita alipopanda ulingoni alipata kipigo ambacho hakikuwa na ubishi kuwa kaonewa.

Bondia huyo alipanda ulingoni Julai 30, 2022 akichapika kwa TKO katika raundi ya nne dhidi ya Shaban Kaoneka, lakini kabla ya pambano hilo lililofanyika Songea, mikwara ya Mandonga ilikuwa siyo ya nchi hii.

Baada ya pambano hilo, imekuwa kichekesho nchini kila unapotaja jina la Mandonga watu humshangilia hivyo kujiongezea mashabiki wengi pamoja na ubalozi katika mikoa mbalimbali ikiwamo Songea na Mtwara.

Mandonga mwenye rekodi ya kucheza mapambano matano kabla ya pambano lake dhidi ya Salim Abeid kutoka Tanga, ameshinda moja kwa KO kati ya hayo matatu amepigwa kwa KO huku akitoka sare moja.

Huyo ndiye Mandonga ambaye wakazi wa Arusha na vitongoji vyake watamshuhudia leo mubashara akifanya kwenye ulingoni.

Bondia ambaye amekuwa na misemo tofauti tofauti kila anapokuwa na pambano, ambapo alianza na 'Mandonga Mtu Kazi', 'Mtumbwi wa Vibwengo' baada ya kuchapika kwa Shaban Kaoneka akaibuka na kaulimbiu yake nyingine ya 'Mwanaume alii na bahari haikauki' na sasa akitamba na 'Ngumi ya Ndoige'.

**Maandalizi**

Mabondia wote wameshafika jijini Arusha na kila mmoja yuko tayari kwa ajili ya kufanya kazi hiyo kwa kuonyesha ubabe wake.

"Kila kitu kinaenda vizuri ukizingatia asilimia 90 ulingo uliopo ni wakisasa na tayari umeshafungwa kinachosubiriwa ni kuona nani kati ya mabondia hao wataibuka na ushindi," anasema Semunyu.

**Kwa nini Arusha**

Semunyu anasema amefanya mapambano mikoa mbalimbali lakini Arusha hakuwahi kufanya, hivyo akapokea maombi mengi kutoka jijini humo kwa ajili ya kupeleka pambano kwa kuwakutanisha mabondia wazawa.

"Nimeleta huku kwa sababu wameniomba na nimeleta usiku huu wa mabingwa kwa ajili ya kuwapa burudani wakazi wa Arusha na ninaimani watafurahia burudani watakayopata," anasema promota huyo.

**Malengo**

Semunyu anasema kabla ya Arusha, amefanya mapambano mengi sana mikoa mbalimbali kwa kuwaibua mabondia wachanga pamoja na kuwapa nafasi ya kuonekana.

"Ni kweli ngumi zamani zilikuwa juu lakini kwa sasa mchezo huo umeporomoka ghafla na sasa tunapambana kuhakikisha unarejea katika ubora ule wa miaka ya nyuma," anasema promota huyo.

---

**NDANI YA 18**




KATIKA soka la wanaume duniani kwa sasa, Kylian Mbappe hadi sasa ndiye mchezaji anayeongoza kwa kufunga mabao mengi zaidi kwa mwaka huu, akiwa amefunga mabao 55 katika mechi 55 kwa klabu na timu yake ya taifa, akifuatiwa na Erling Haaland mwenye mabao 43 yaliyotokana na mechi 40 katika klabu na timu ya taifa.

# SOKA



**REKODI**
*Ametwaa Kiatu cha Dhahabu Kombe la Dunia la Fifa Qatar 2022 akiwa amefunga mabao nane.
*Katika soka la wanaume duniani kwa sasa, Kylian Mbappe hadi sasa ndiye mchezaji anayeongoza kwa kufunga mabao mengi zaidi kwa mwaka huu, akiwa amecheka na nyavu mara 55 kwenye mechi 55 kwa klabu na timu yake ya taifa, anafuatiwa na Erling Haaland mwenye mabao 43 yaliyotokana na mechi 40 klabu na timu ya taifa.

**MKALI WA WIKI**

**JINA KAMILI:** Kylian Mbappe Lottin
**KUZALIWA:** Desemba 20, 1998 (miaka 24)
**ALIPOZALIWA:** Paris, Ufaransa
**KIMO:** 1.78 m (5 ft 10 in)
**NAFASI:** Mshambuliaji
**KLABU:** Paris Saint-Germain
**JEZI:** Namba 7/ Taifa Na.10

TUMESIKIA mashabiki wakiwa na imani potofu tofauti kabla, wakati na hata baada ya michezo na haipaswi kushangaza kwamba hata wachezaji, mameneja, na marais wa timu wana yao.

Uk. 16-17



MESSI LIONEL NA ALVAREZ

# ASISTI 5 - BORA ZAIDI KOMBE LA DUNIA 2022

**DOHA,** Qatar

KATIKA soka kufunga mabao ni jambo muhimu, ingawa wafungaji hupata sifa mara nyingi kuliko wale wanaotengeneza nafasi muhimu kwa timu.

**Kutengeneza nafasi au kupanga wachezaji wenzako wafunge lazima iwe nyuma ya kupata bao la upande wako. Wakati mwingine, mtoaji wa pasi anafanya sehemu kubwa ya kazi ambayo mshambuliaji anaihitaji.**

Makala haya yanaangalia 'asisti' (pasi za mwisho) tano bora zaidi kwenye Kombe la Dunia la 2022 nchini Qatar...

**#5. Son Heung-min kwa Hwang Hee-chan (Korea Kusini vs Ureno)**

Korea Kusini ilipata ushindi mnono katika mchezo wao wa mwisho wa hatua ya makundi dhidi ya Ureno na kutinga hatua ya 16 bora. Ricardo Horta aliwafungia vijana wa kocha Fernando Santos dakika ya tano ya mchezo kabla ya Kim Young-gwon kusawazisha.

Walihitaji sana pointi zote tatu na hawakuweza kupata mshindi hadi dakika ya 91. Son Heung-min alichukua mpira kutoka ndani ya nusu yake na kukimbia na alipokuwa karibu na sanduku la wapinzani, aliinua kichwa chake na kumuona Hwang Hee-chan mbele yake.

Son alisubiri kwa sekunde mbili zaidi, akiwavutia walinzi watatu kwake kabla ya kumtengenezea pande nzuri fowadi huyo wa Wolverhampton Wanderers.

Alifanya kazi nzuri na kushinda mchezo kwa upande wake. Korea Kusini ilikuwa imepia hatua moja kubwa zaidi kwenye hatua ya makundi. Lakini yote yalitokana na juhudi na uwapo wa wawili hao.

**#4. Daley Blind kwa Denzel Dumfries (Uholanzi vs Marekani)**

Uholanzi ilitawala dhidi ya Marekani kwa sehemu kubwa ya mchezo wao hatua ya 16-bora. Mabeki wao wa pembeni walikuwa wamejaa na Denzel Dumfries ndiye alikuwa kinara wa onyesho hilo kwa kutoa pasi mbili za mabao na bao moja. Daley Blind alijifanyia vema pia, akifunga bao na kutengeneza asisti.

Baada ya kuwa mbele kwa 2-0, Uholanzi iliwapa Marekani mwanga wa matumaini kwa kuruhusu bao katika dakika ya 76. Dakika chache tu baada ya Marekani kupata bao lao, Blind alipokea mpira kwenye winga na kumpasia Dumfries na kwa usahihi kabisa aliuweka mpira wavuni.

**#3. Lionel Messi kwa Nahuel Molina (Argentina vs Uholanzi)**

Argentina walitarajiwa kupata shida kujaribu kuvunja safu ya ulinzi ya Uholanzi katika mchezo wao wa robo fainali. Walipata ugumu wa kupata upenyo, lakini hiyo ilikuwa hadi Messi alipoamua kuchukua mambo mikononi mwake. Alipokea mpira si mbali sana ndani ya nusu ya Uholanzi.

Messi mwenye umri wa miaka 35, kisha akaingia ndani, akimkokota Nathan Ake. Wakati Messi akiingia ndani, beki wa kulia wa Argentina, Nahuel Molina alikimbia hadi kwenye eneo la hatari. Messi aliinua kicha na kumuona.

Alitoa pasi ya bila kuangalia katika miguu ya Ake na kumfikia Molina akaupata na kufunga.

**#2. Vinicius Junior kwa Lucas Paqueta (Brazil vs Korea Kusini)**

Brazil iliibomoa kabisa Korea Kusini katika kipindi cha kwanza cha mchuano wao wa hatua ya 16-bora. Selecao hao waliweka mpira kwenye lango la Wakorea mara nne ndani ya dakika 36 na bao lao la nne lilikuwa jambo la kupendeza.

Brazil walianza moja ya shambulizi lao la kushtukiza na ilikuwa hali ya tatu kwa nne wakati Neymar akimchezea mpira Vinicius kwenye winga ya kushoto.

Wakati huo, Richarlison na Raphinha walichukuliwa na alama zao, Neymar alionekana kukimbilia moja kwa moja kuelekea langoni. Hapo ndipo Lucas Paqueta alipoingia eneo la tukio na kuchelewa kuingia kwenye boksi.

Vinicius akatoa pasi ya kuvutia iliyochongwa hadi kwenye njia yake na kiungo huyo akapiga mpira kwenye kona ya chini na kufunga bao.

**#1. Lionel Messi kwenda kwa Julian Alvarez (Argentina vs Croatia)**

Josko Gvardiol, beki wa kati wa Croatia mwenye umri wa miaka 20, alikuwa na Kombe la Dunia la kupendeza na anachukuliwa kuwa mmoja wa mabeki bora wa michuano hiyo.

Huku matokeo yakiwa 2-0, Messi akapokea mpira kwenye wingi ya kulia. Gvardiol akamfuata kumkaba, lakini Messi mshindi mara saba wa Ballon d'Or, akamshinda na kukimbia hadi kwenye mstari wa mbele na kupiga krosi.

Messi kisha akaonyesha nguvu ya ajabu ya kumzuia anapopiga hatua kwenye eneo la hatari na kisha kutoa pasi kwenye miguu ya Gvardiol kumtafuta Alvarez. Alichohitaji kufanya mshambuliaji huyo mchanga ni kufunga kiurahisi tu.

**JE, WAJUA?**



WACHEZAJI waliopiga pasi za muhimu Kombe la Dunia Qatar 2022, Antoine Griezmann (21), Lionel Messi (21), Ousmane Dembele (11), Theo Hernandez (11), Kylian Mbappe (11), Cody Gakpo (11), Angel Dimaria (10) na Dusan Tadic (10).





# UWT yampongeza Rais Samia utekelezaji miradi ya maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UMOJA wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Mbeya, umefanya kongamano maalumu la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ndani ya mkoa huo na taifa.

Kongamano hilo lilifanyika mwishoni mwa wiki jijini hapo na kuwashirikisha wajumbe 490 pamoja na baadhi ya viongozi wa serikali akiwamo Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson.

Kongamano hilo lilitanguliwa na maandamano ya amani ya waliokuwa wanaimba nyimbo mbalimbali za kumpongeza Rais Samia kwa kuendelea kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na amani ya nchi.

Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Maryprisca Mahundi, aliwataka wanawake nchini kuendelea kumuunga mkono Rais Samia katika shughuli mbalimbali za maendeleo anazozifanya kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Alisema kiongozi huyo alipokea kijiti cha uongozi wa taifa katika kipindi kigumu ambacho kilikuwa ni cha majonzi baada ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli.

Mahundi ambaye ni Naibu Waziri wa Maji, alisema pamoja na hali hiyo amekuwa akipambana kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo iliyoanzishwa na muasisi wake pamoja na kubuni miradi mipya ambayo inamanufaa kwa wananchi.

Aliitaja baadhi ya miradi ambayo inawanufaisha wananchi kwenye Mkoa wa Mbeya kuwa ni pamoja na miradi ya maji ambayo imegharimu fedha nyingi, miradi ya vituo vya kutolea huduma za afya ndani ambavyo asilimia kubwa ya wanufaika ni wanawake.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia alisema katika Jiji la Mbeya, serikali imejenga vyumba vya madarasa kwenye shule mbalimbali za msingi na sekondari ili kuwasaidia wanafunzi kusomea kwenye mazingira rafiki.

Alisema zipo baadhi ya shule mpya zimejengwa ikiwamo Shule ya Sekondari Iziwa na Shule ya Sekondari ya Dk. Tulia iliyoko Itende kwa lengo la kuwapunguzia wanafunzi umbali wa kwenda kusoma shule za kata zingine.

Alisema pia serikali imeanza kujenga mabweni kwenye baadhi ya shule kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa kike kukaa shuleni ili kuwaepusha na vikwazo mbalimbali vya elimu ikiwamo kuwaepusha na 'mafataki'.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema serikali inaendelea na mchakato wa kupanua Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) kuanzia Uyole hadi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) kwa kuifanya kuwa ya njia nne.

Alisema serikali inaendelea kuboresha Uwanja wa Ndege wa Songwe ili kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo.

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Mbeya, Edna Mwaigomole, aliishukuru Taasisi ya Maryprisca Women Foundation kwa kuisaidia UWT kuandaa kongamano hilo.



Wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Mbeya wakiwa pamoja baada ya kumaliza mkutano mkuu maalum uliofanyika juzi jijini humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watanzania washauriwa kuwatembelea watoto yatima

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATANZANIA wameshauriwa kutembelea vituo vya kulelea watoto yatima vilivyoko kwenye maeneo yao kwa lengo la kuwafariji watoto wanaolelewa kwenye vituo hivyo.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Mayeka Mayeka, alitoa ushauri huo juzi alipotembelea Kituo cha Kulelea watoto yatima cha Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde Iwambi jijini Mbeya.

Mayeka alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, wakati wa kuwasilisha msaada wa chakula na vitu mbalimbali kwenye kituo hicho vilivyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwenye vituo vya watoto yatima.

Mayeka alisema watoto wanaolelewa kwenye vituo hivyo wanahitaji kufarijiwa kwa kutembelewa mara kwa mara na kupewa zawadi mbalimbali hasa kipindi cha sikukuu ili na wao wajisikie kuwa sehemu ya jamii.

Alisema watoto hao wanahitaji mahitaji mbalimbali kama ilivyo kwa watoto wenye wazazi ikiwamo chakula na mavazi na hivyo akawataka wananchi kuwasaidia.

"Kuna vitu tunaweza tukawa tunavyo majumbani mwetu lakini pengine hatuna matumizi navyo, kwa hiyo unaweza ukawaletea watoto hawa vikawasaidia," alisema Mayeka. Alisema Rais Samia aligawa vitu hivyo kwenye mikoa yote nchini ili kuwasaidia watoto hao kusherehekea vizuri sikukuu za mwisho wa mwaka kama watoto wengine.

Uongozi wa Kanisa la KKKT Dayosisi ya Konde ulimshukuru Rais Samia kwa kuwakumbuka watoto wanaolelewa kwenye kituo hicho.

Viongozi hao walisema watoto wanaolelewa kwenye kituo hicho wanahitaji vitu mbaimbali ikiwamo mahitaji ya shule.

Baadhi ya watoto wanaolelewa kwenye kituo hicho waliwashukuru wadau mbalimbali ambao wamekuwa wakiwatembelea na kuwafariji kwa nyakati tofauti.

Mmoja wa watoto hao, Dorcas Mwambwalo, alisema vitu walivyopatiwa na Rais Samia vitawasaidia kusherehekea vizuri sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya.

Alisema asilimia kubwa ya vitu walivyopelekewa ni vyakula mbavyo ni mchele, mafuta ya kupikia na sukari.

## Waomba kuboreshewa mifereji kujikinga na mafuriko

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wameiomba serikali kuwaboreshea mifereji ya maji ili kupunguza mafuriko ambayo yameanza kuwaathiri kwenye makazi yao wakati wa mvua.

Wananchi hao walieleza kuwa mvua inaponyesha maji hujaa kwenye mifereji iliyoko na kuanza kusambaa barabarani na kwenye makazi yao hali ambayo ni hatari kiafya.

Mmoja wa wananchi hao, Tilson Kamwela alisema serikali imejenga mifereji lakini haina uelekeo wa kusafirisha maji na badala yake maji yanajaa na kuanza kusambaa kwenye makazi ya watu.

Alisema wiki iliyopita maji yaliacha mkondo na kuanza kupita juu ya Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) kisha yakavuka kwenye makazi yao na kuharibu vitu.

Alisema maji hayo yaliingia katika baadhi ya nyumba hali iliyowalazimu wananchi kuyakimbia makazi yao.

"Asubuhi tuliwahi kuyatoa maji kwenye nyumba zetu, hii mifereji imejengwa mwaka huu lakini ukiangalia haina uelekeo, imezibwa pande zote mbili hali ambayo inayafanya maji yakijaa yawe yanaingia kwenye makazi yetu," alisema Kamwela.

Mariam Julius alisema katika Mtaa wa Kabale kuna mifereji miwili ambayo inapeleka maji baada ya mfereji mmoja kuzibwa ili usipeleke maji katika Bonde la Ifisi ambako awali ndiko mkondo ulikuwa unaelekeza maji.

Aliwaomba viongozi wa serikali kuwasaidia kuboresha mifereji hiyo ili waendelee kuishi kwa amani tofauti na sasa ambapo wanahofu maji kuingia tena kwenye nyumba zao.





# Washauri vituo vya kulea watoto yatima vipewe ruzuku

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kutoa ruzuku kwa vituo ambavyo vinatoa huduma za kulea watoto waishio katika mazingira magumu vinavyotambulika kisheria.

Ushauri huo ulitolewa na Mwenyekiti wa kinamama katika Kanisa la TAG Upendo Revival Christian Center Area "D", Kissa Mwakipesile, baada ya kutoa msaada wa vitu mbalimbali katika kituo cha kulelea watoto waishio katika mazingira magumu cha Safina Street Network kilichoko eneo la Airport.

Msaada uliotolewa ni vyakula, mavazi, sabuni, mafuta ya kupikia na vifaa vya shule.

Kissa alisema kuna vituo vingi vinavyolea watoto waishio katika mazingira magumu vinakabiliwa na matatizo mbalimbali hususani za kiuchumi, hivyo serikali inatakiwa kuona uwezekano wa kuviwezesha ili viweze kutoa huduma za uhakika kwa watoto.

Alisema kuwa umoja wa kinamama wamelazimika kutoa misaada hiyo kwenye kituo hicho ikiwa ni sehemu ya kutimiza maandiko matakatifu ambayo yanaeleza wazi kuwa dini iliyo nzuri ni kuwajali yatima, wajane na wale wasiojiweza.

"Kwa kuzingatia maandiko matakatifu umoja wa kinamama wa Kanisa la TAG Upendo Revival Christian Center Area "D" tumetoa misaada ya mahitaji muhimu kwa watoto wa kituo cha kulelea watoto waishio katika mazingira magumu cha Safina SN kwa lengo la kuwafanya watoto hao wasijisikie wapweke na badala yake waweze kufurahia sikukuu kama zilivyo familia nyingine.

Mwenyekiti huyo aliiomba jamii pia kutambua kuwa watoto waishio katika mazingira magumu wanahaki sawa na watoto wengine.

Mchungaji Msaidizi wa Kanisa la TAG Upendo Rivival Christian Center Area "D", Rehema Vangast, alisema kuwa ongezeko la watoto wengi waishio katika mazingira magumu kunatokana na familia nyingi kuwa na migogoro isiyoisha.

Alisema pamoja na migogoro ya kifamilia pia malezi yamekuwa hafifu kwani wazazi na walezi wengi wanatumia muda mwingi kufanya shughuli za utafutaji badala ya kuangalia mwenendo wa familia zao pamoja na kuwaonya watoto wao pale wanapokuwa wamekosea.

# H'shauri zanufaika programu kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HALMASHAURI tatu za Mkoa wa Dodoma zimeanza kunufaika na utekelezaji wa programu ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuendeleza Mitaji kwa ajili ya Maendeleo (UNCDF) kupitia mfumo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza jijini hapo wakati wa kikao kazi cha kutambulisha programu hiyo Mkurugenzi wa Mazingira, Dk. Andrew Komba, alisema awamu ya kwanza ya programu hiyo inatekelezwa katika halmashauri tatu ambazo ni Chamwino, Kondoa na Mpwapwa.

"Utekelezaji wa programu hii itaongezea jamii mtaji katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yana athari kubwa katika maisha yao ya kila siku," alisema.

Dk. Komba ambaye alimwakilisha Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Dk. Switbert Mkama, alisema baada ya kupata matokeo tarajiwa itaendelea na kufikia kati ya halmashauri 10 hadi 15 katika awamu wa pili ya programu.

Kuhusu kikao kazi hicho, Dk. Komba alisema ni fursa kwa washiriki kuweza kupitia taarifa mbalimbali za kimazingira zikiwamo biashara ya kaboni ambayo tayari serikali imeandaa mwongozo na kanuni zake.

Alisema kikao hicho pia kitawapa fursa ya kujadili kuhusu mchango wa kitaifa wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, tathmini ya athari ya mazingira kimkakati.

"Huu ni mwendelezo wa jitihada za kitaifa za kushughulikia athari za mabadiliko ya tabianchi na kulinda uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za binadamu hususani katika serikali ya mitaa, vijiji na vitongoji,"alisema.

Aidha, Dk. Komba alisema nchi 24 duniani zinatekeleza programu hiyo huku Tanzania ikiwa mojawapo na hukutanisha mawaziri wa kisekta wanaounda bodi inayokutana kila mwaka kujadili namna ya kuwezesha jamii kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Serikali inaamini programu hii italeta tija iwapo itakuwa na ufanisi kwa sababu ni miongoni mwa programu zinazotambua dhana ya kuona fedha za mabadiliko ya tabianchi zinamfikia mlengwa moja kwa moja kwa maana kijiji husika,"alisema.

Kikao hicho cha siku mbili kilihusisha washiriki kutoka katika wizara mbalimbali ambazo zinashughulikia programu hiyo.



Ofisa Afya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Mary Semngindo (kulia), akimpatia chanjo mtoto Yohana Baraka aliyezaliwa hospitalini hapo usiku wa kuamkia Krismasi jana. Aliyempakata mtoto ni mama wa mtoto, Abigael Muhuya mkazi wa Chang'ombe jijini Dodoma. Kushoto ni Ofisa Muuguzi, Furaha Mbwilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# BMH yazindua kikosi kazi kupinga unyanyasaji kijinsia

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa (BMH) imezindua kikosi kazi ambacho kitakuwa kinatoa elimu ya kupinga unyanyasaji wa kijinsia.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Msaidizi wa Utafiti na Ubunifu wa Hospitali, Hindu Ibrahim, Dodoma ni mkoa wa pili kwa kuwa na kesi nyingi za ukatili wa kijinsia.

"Kwa hiyo, kikosi kazi hiki kinachoundwa na watumishi wa BMH kitasaidia kutoa elimu kwa wagonjwa wanaokuja hapa hospitalini," alisema.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Mkoa wa Dodoma, Josephine Mwaipopo, aliishukuru BMH kwa kusimama kama daraja kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia.

Alisema suala la ukatili linapaswa kupigwa vita na kila mmoja wetu siyo kuiachia serikali katika mapambano hayo.

Alisema wamekuwa wakijitahidi kutoa semina na kufanya makongamano mbalimbali ikiwamo kutoa elimu kwa jamii kuhusu kupinga ukatili wa kijinsia katika maeneo mbalimbali hapa nchini. "Hospitali hii imekuwa ni msaada mkubwa kwetu katika vita dhidi ya ukatili wa kijinsia kwa kuwahudumia waathirika wa ukatili wa kijinsia," alisema Josephine.

Mkuu wa Dawati la Jinsia kutoka Jeshi la Polisi, Inspekta Jelda Luyangi, alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia vimeshamiri sana katika Mkoa wa Dodoma.

Pamoja na kushamiri alisema jeshi hilo liko mstari wa mbele kupambana na suala hilo kuhakikisha linatokomezwa katika maeneo mbalimbali.

Kutokana na hilo aliwataka wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa juu ya kupambana na ukatili hapa nchini.

"Vitendo vya ubakaji na ulawiti ndiyo vinaongoza kwa Mkoa wa Dodoma na ukatili dhidi ya watoto," alifafanua.





# SMZ kuisapoti Taasisi ya Karume kuzalisha wataalamu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kuiimarisha Taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia (KIST) ili izidi kuzalisha wataalamu watakaoendeleza ukuaji wa sayansi na teknolojia nchini.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo juzi katika hotuba yake iliyosomwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, katika mahafali ya nane ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume Mbweni Zanzibar.

Alisema serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na taasisi hiyo katika kufanikisha ukuaji wa teknolojia Zanzibar kwa kutoa wataalamu wengi ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya Zanzibar.

Rais Dk. Mwinyi alisema serikali imeandaa mipango madhubuti ya miradi ambayo itafanywa katika taasisi hiyo ikiwamo ujenzi wa majengo ya madarasa na makazi ya wanafunzi.

Aidha, alisema serikali imedhamiria kuzipa kipaumbele taasisi za elimu katika kuziwezesha kutokana na mchango mkubwa na muhimu hasa kuzalisha wataalamu wa fani za uhandisi jambo ambalo ni msingi wa maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Alisema kuna mradi wa (SEBET) uliolenga kuwasaidia vijana katika kuwapa ujuzi utakaoendana na soko la ajira katika uchumi wa buluu mradi ambao utaimarisha na kuanzisha mafunzo ya ngazi tofauti.

"Mradi huu utaimarisha na kuanzisha mafunzo katika ngazi ya astashahada na stashahada zifuatazo; uhandisi wa vyombo vya baharini, uhandisi wa vipoza hewa, usarifu wa mazao ya bahari, matunda na mboga," alisema.

Aidha, alitumia fursa hiyo kuwashukuru wahisani mbalimbali waliosaidia Taasisi ya Karume tangu ilipoanzishwa kwa kuiwezesha kupata maendeleo ya kitaaluma ikiwamo Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Teknolojia (UNESCO) ambao wamefadhili kuanzisha mafunzo ya fani zinazohusisha usarifu wa mazao ya baharini, usarifu wa matunda na mboga.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, alieleza kuwa Taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia inakwenda sambamba na kasi ya serikali kwa kuwa wabunifu kwa kuanzisha fani mbalimbali zikiwamo za kukuza uchumi wa buluu.

Aidha, aliitaka taasisi hiyo kuanzisha fani za kuwafunza walimu watakaofundisha fani za uhandisi ili kurahisisha kupata wakufunzi watakaosaidia kufundisha katika taasisi hiyo.

Mkuu wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume, Dk. Mahmoud Abdulwahab Alawi, alisema taasisi hiyo imefanikiwa kuanzisha fani za uchumi wa buluu ili kuunga mkono serikali katika kukuza uchumi wake kupitia sekta hiyo.

Pia alisema taasisi hiyo imefanikiwa kuanzisha kituo cha ujasiriamali kwa lengo la kusaidia vijana kujikwamua kiuchumi kwa kujiajiri na kuajiriwa.




Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdallah (kulia), akiwa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, katika mahafali ya nane ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume Mbweni Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wizara ya Afya yapokea vifaa tiba vya mil.35/-

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imepokea vifaa mbalimbali ikiwamo vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 35 kutoka kwa Taasisi ya Noah and Good People kwa ajili kusaidia utoaji wa huduma za afya kwa jamii.

Akizungumza jana wakati wa kupokea vifaa hivyo, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Fatma Mrisho, aliishukuru taasisi hiyo kwa kuunga jitihada za serikali katika kutoa huduma bora za afya kwa wananchi.

Makabidhiano ya vifaa hivyo yalifanyika katika Hospitali ya Kidimni iliyoko Wilaya ya Kati Unguja ambapo taasisi hiyo inasaidia kupata taarifa sahihi za magonjwa kutokana na kutumia teknolojia ya kisasa katika kuhifadhi taarifa mbalimbali.

Katibu mkuu huyo alimtaka Mganga Mkuu wa Hospitali hiyo kuomba dawa kwa wakati kutokana na uhitaji na ongezeko la wagonjwa wanaofika kituoni hapo.

Mkurugenzi wa Kinga na Elimu Afya, Dk. Salim Slim, alisema taasisi hiyo imejenga hospitali ambayo inawasaidia wananchi wa Wilaya ya Kati kupata huduma za afya jambo ambalo limeweza kupunguza mrundikano wa wagonjwa katika vituo vingine.

Alisema kupatikana kwa vifaa hivyo kutasaidia uboreshaji wa huduma za uchunguzi hasa za mama na mtoto na kupunguza vifo.

Hivyo aliitaka jamii kuwekeza zaidi katika afya kwa kujenga tabia ya kupima mara kwa mara, ili kujua na kujikinga na maradhi yanayopoteza nguvu kazi ya taifa na kuipa gharama kubwa serikali katika kutibu.

Mwendeshaji wa taasisi hiyo, Noah Park, alisema wanaendelea kushirikiana na serikali kuisaidia jamii hasa kwa wananchi maskini katika sekta mbalimbali ikiwamo ya afya ili kumudu gharama za matibabu.

Daktari Mkuu wa Hospitali ya Kidimni, Rajab Haji Rajab, alisema vifaa hivyo vitasaidia uchunguzi kwa wajawazito na vitarahisha utoaji wa huduma.

# Waziri apiga 'stop' mitihani taifa kusahishiwa shule binafsi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, amepiga marufuku kwa maofisa wa Baraza la Mitihani Zanzibar kupeleka mitihani ya taifa kusahishwa katika vituo vya shule binafsi.

Alitoa onyo hilo jana visiwani Zanzibar alipokutana na watendaji wa Baraza la Mitihani la Zanzibar kwa ajili ya kubadilishana na kujenga mikakati ya kuleta ufanisi katika kazi zao.

Alisema Serikali ya Zanzibar imejipanga kuimarisha Baraza la Mitihani la Taifa na kuwa chombo kinachojitegemea katika kufanya shughuli zake za kusimamia majukumu ya elimu.

Alisema katika kusimamia majukumu yake suala la uadilifu linahitajika kwa kiwango kikubwa kuanzia kwa watendaji wake kujipima majukumu yao.

Mussa alisema katika miaka ya nyuma kumejitokeza matukio ambayo kwa kiasi kikubwa yamepoteza sifa na ubora wa Baraza la Mitihani kufuatia kuvuja kwa mitihani inayotayarishwa na taaasisi hiyo.


Alisema ni kinyume na maadili kwa Baraza la Mitihani la Taifa, mitihani ya taifa inasahihishwa katika vituo vya shule binafsi wakati zipo shule nyingi zinazomilikiwa na wizara zikiwa na nafasi ya kutosha.

"Kuanzia sasa napiga marufuku mara moja watendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa kupeleka mitihani ya serikali kusahihishwa katika vituo vya shule binafsi...hili silikubali na katika kipindi cha uongozi wangu halitakuwapo kwa sababu ni kinyume na sheria za wizara," alisema.

Mkurugenzi wa Baraza la Mitihani la Taifa Zanzibar, Othman Omar Othman, alisema kwa sasa wapo katika hatua za mwisho za utayarishaji wa mifumo ya mitihani ambayo lengo lake utaweka bayana utaratibu mzima wa matayarisho yake hadi katika usahihishaji.

Aidha, alisema wapo katika mchakato wa marekebisho ya sheria za mitihani ya taifa katika utayarishaji wake kwa lengo la kuleta ufanisi bora.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khamis Abdalla, aliwataka watendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa kujitathmini zaidi katika utekelezaji wa majukumu yao ambayo kwa kawaida yanaongozwa na uadilifu.





# Wananchi wapewa miche kudhibiti athari za mazingira

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wa Pandagichiza na Mwalukwa wilayani Shinyanga wamepewe miche ya miti kwa ajili ya kupanda kwenye maeneo yao ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na athari za mazingira.

Hatua hiyo ilifikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kwa kushirikiana na Shirika la Organisation of People Empowenment (OPE).

Akieleza jitihada wanazozifanya katika kukabiliana na athari za kimazingira, Ofisa Miradi kutoka OPE, Mpuya alisema shirika hilo limeanzisha kampeni ya kupanda miti wilayani humo, sambamba na kuotesha kitalu cha miche ambayo inatolewa bure kwa wananchi ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

"Kabla ya kuigawa miche kwa wananchi, hua tunawapatia kwanza elimu ya upandaji, kuitunza na faida ya miti na katika kata hizi mbili ambazo ni za mfano Pandagichiza na Mwalukwa tumeshawapatia wananchi miche 75,650," alisema Mpuya.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Shinyanga, Boniphace Chambi, alilipongeza shirika hilo kwa hatua hiyo akisema ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali za kuhamasisha wananchi kupanda miti kwa wingi.

Aidha, aliwasihi wananchi kupanda miti kwenye maeneo yao ya mipaka, hali ambayo itasaidia kutatua migogoro ya ardhi.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Edward Maduhu, alisema halmashauri hiyo imepanga kupanda miti milioni 1.5 kwa mwaka mzima.

Baadhi ya wananchi ambao wamepewa miche walilishukuru shirika hilo na kueleza kuwa wananchi wa maeneo ya vijijini wengi wao hawana elimu juu ya faida ya miti na ndiyo maana wamekuwa wakiikata ovyo na wengine kuchoma mikaa bila ya kujua madhara yake.




Mkuu wa Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga, Festo Kiswaga, akiendesha trekta lililotolewa na Benki ya NBC kwa mkulima Hamisi Majogoro kutoka Halmashauri ya Ushetu (hayupo pichani), lenye thamani ya Sh. milioni 53 jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Maofisa kampuni inayojenga SGR matatani tuhumu rushwa

**Na Halima Ikunji,** TABORA

KAIMU Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Paul Chacha, ameuagiza uongozi wa Kampuni ya Yapi Merkezi kuwaondoa maofisa wao tisa wa vitengo vya ajira, usaili na afya wanaotuhumiwa kuomba rushwa kwa watu wanaomba kazi katika kampuni hiyo.

Kampuni hiyo kwa sasa inajenga Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Makutopora mkoani Dodoma hadi Tabora.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki katika kikao cha pamoja kilichowakutanisha viongozi wa kampuni hiyo na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Tabora Mjini.

Alisema Serikali ya Wilaya na Mkoa wa Tabora haitaweza kuwavumilia watumishi hao wanaomba rushwa kwa Watanzania wanaomba ajira kwenye mradi huo mkubwa unaotekelezwa mkoani humo.

Alisema wamepokea malalamiko mengi toka kwa Watanzania kwamba wamekuwa wakiombwa rushwa kati ya Sh. 250,000 hadi Sh. 300,000 ndipo waweze kupata ajira ndani ya kampuni hiyo.

Aidha, aliwataka vijana na wananchi wanaofika kupata ajira katika kampuni hiyo watoe taarifa kwa serikali pindi atakapotokea mtu kuwaomba rushwa.

Alieleza kuwapo kwa watu tisa ambao ni Watanzania waliokuwa wakijihusisha na uombaji wa rushwa na upokeaji tayari wamesimamishwa kazi na uchunguzi unaendelea.

Pamoja na mambo mengine katika kikao hicho serikali imeishauri kampuni hiyo kuweka rangi kwenye mafuta yao wanayoagiza ili inapotokea hujuma iweze kubainika.

Hatua hiyo inafuatia Jeshi la Polisi Tabora kukamata mafuta dumu 64 za lita 20 pamoja na watuhumiwa tisa akiwamo dereva wa kampuni hiyo akihusishwa na wizi huo ambao wanasubiri kufikishwa mahakamani.

Meneja Mradi kutoka Kampuni ya Yapi Merkezi, Gokhan Ginar, alisema kuwa wapo tayari kumfukuza kazi mtu yoyote atakayebainika kuhusika na tuhuma za rushwa katika ajira.

Naye Mhandisi Ayubu Mdachi ambaye ni Meneja wa Mradi wa Ujenzi wa SGR kutoka Shirika la Reli Tanzania (TRC) alisema hadi sasa ujenzi wa reli hiyo umefikia asilimia 3.08 katika kipindi cha nusu mwezi.

Aliongeza kuwa hadi sasa watu walioajiriwa ni 2,993 kati ya watu 7,000 ambao wanatarajiwa kupata ajira katika vitengo mbalimbali.

# Imani za kishirikina zakwamisha kutokomeza matukio ukatili

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wamekuwa wagumu kutoa taarifa za vitendo vya ukatili wa kijinsia wanavyofanyiwa wanawake na watoto katika vyombo vya sheria kwa kuogopa kurogwa.

Hali hiyo imeelezwa kusababisha kesi hizo kutatuliwa katika ngazi ya jamii kinyemela.

Hayo yalibainishwa jana na Laurent Thomas mkazi wa Kata ya Shilela, wakati wa mjadala wa ushiriki wa wanaume na vijana katika kupambana na ukatili wa kijinsia ndani ya jamii, uliondaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa ufadhili wa KOICA.

Alisema watoto wenye umri mdogo hususani wa kike wamekuwa wakifanyiwa vitendo hivyo kwa wingi huku wazazi wakiogopa kufichua uovu huo kwa kutoa taarifa katika Jeshi la Polisi au Ofisi ya Mtendaji wa Kata kwa kuogopa kufanyiwa vitendo vya kishirikina na watuhumiwa hao.

"Wanaofanya vitendo vya kikatili kwa watoto wetu ni watu wetu wa karibu na tunaowaamini, sasa wazazi wanashindwa kutoa taarifa katika vyombo vya sheria kwa kuogopa kuvunja undugu au kurogwa na wahusika hii inafanya matukio kuendelea kuongezeka kila siku,"alisema Thomas.

Naye Patrick Mihayo alisema baadhi yao wamekuwa mstari wa mbele katika kusimamia ndoa za utotoni na kwamba hali hiyo imekuwa ikifanyika kutokana na mkanganyiko wa Sheria ya Mtoto ya mwaka 1977 na 2019 kuwa mtoto anayetakiwa kuolewa anatakiwa kuwa na umri gani.

Aidha, alisema ndoa hizo zimekuwa zikifanyika katika maeneo ya vijijini kwa kiwango kikubwa kutokana na hali ya ugumu wa maisha iliyoko katika baadhi ya familia na zimekuwa hazidumu kwa muda mfupi kwa kuwa bado watoto hawajapevuka na hawafahamu namna ya kumlea mume.

Mwakilishi wa Jeshi la Polisi kutoka Kituo cha Polisi Bugarama Msalala, Sajenti Mbwana, alisema licha ya vitisho hivyo wazazi wengine huwazuia watoto wao kwenda shuleni hasa kipindi cha mitihani ya kuhitimu elimu ya msingi na sekondari jambo ambalo ni kinyume na sheria.

Alisema wanafanya hivyo ili watoto wasiweza kusoma hali ambayo itakuwa rahisi inapofika miezi mitatu bila ya kuonekana shule kufukuzwa shule kwa sababu ya utoro na kupata muda wa kumwozesha bila kipingamizi.

Ofisa Mradi wa TGNP, Jackson Malangalila, alisema ni kosa kisheria kumwozesha mtoto ambaye hajafikisha miaka 18 na mtu ukibainika utachukuliwa hatua kali ikiwamo kufikishwa mahakamani.

## HABARI KIMATAIFA

# Papa: Wakumbukeni wanyonge na maskini

**VATICAN**

PAPA Francis amesema vita na machafuko mengine yanayoendelea katika baadhi ya maeneo duniani ni kutokana na uchoyo na tamaa ya madaraka, na hayo yamesababisha wengine kuwaangamiza majirani zao.

Aliyasema hayo usiku wa kuamkia jana wakati akisherehekea Krismasi ya 10 ya upapa wake, katika Kanisa la St Peter's jijini Vatican ambalo waumini takribani 7,000 walishiriki, huku maongezi yake yakionekana kulenga vita vya Ukraine.

Papa Francis alisema vita na machafuko mengine hutokana na uroho na tamaa ya madaraka.

**"Kama ilivyo kawaida, waathiriwa wa uchoyo huu wa kibinadamu ni wanyonge wasiojiweza na walioko hatarini.**

Hii ilikuwa mara ya kwanza katika miaka miwili tangu janga la COVID kuanza, kwa umati mkubwa wa waumini kuhudhuria misa hiyo ya mkesha wa Krismasi mjini Rome, huku hotuba yake ikijikita katika mada ya uchoyo na matumizi katika viwango tofauti tofauti.

Pia aliwataka waumini kutafakari zaidi kuhusu matumizi makubwa ambayo hushuhudiwa kwenye sherehe za Krismasi. Na badala yake wabaini maana halisi ya Krismasi ili wawakumbuke wale wanaoteseka kutokana na vita na umaskini.

"Wanaume na wanawake katika ulimwengu wetu, katika njaa yao ya kutaka utajiri na madaraka, wanawaangamiza hata majirani, kaka na dada zao, ni vita vingapi tumeona! Na katika maeneo mangapi, hata leo 'jana' je, utu na uhuru wa binadamu zinadharauliwa," alihoji.

Inaelezwa kuwa tangu Russia ilipoivamia Ukraine Februari 24, mwaka huu, Papa Francis amevikemea vita hivyo karibu katika kila hafla yake ya hadharani, angalau mara mbili kila wiki, huku akilaani kile anachokiita kuwa ukatili na uchokozi usiokuwa na msingi.

Hata hivyo katika hotuba yake ya usiku wa kuamkia jana, Papa Francis hakuitaja Ukraine.

"Kama ilivyo kawaida, waathiriwa wa uchoyo huu wa kibinadamu ni wanyonge wasiojiweza na walioko hatarini," alisema huku akishutumu ulimwengu uliojaa tamaa ya fedha, madaraka na anasa.

"Zaidi ya yote, ninawafikiri watoto ambao wameuliwa kutokana na vita, umaskini na dhuluma," akiwataja pia watoto ambao hawajazaliwa, watu maskini na watoto waliosahaulika.

Akilinganisha hali ya Yesu Kristo aliyezaliwa horini mwa ng'ombe na umaskini wa leo, Papa alisema "Horini penye hali ngumu na kukataliwa Mungu alijitokeza mwenyewe. Anakuja hapo kwa sababu tunaweza kuona shida ya ubinadamu wetu. Hali hiyo ya kutokujali na ukosefu wa usawa unasababishwa na uchoyo wa kumiliki vitu na kuvitumia.

Aidha, mapema mwezi huu, Papa Francis aliwahimiza watu kupunguza matumizi yao kwenye sherehe za Krismasi na zawadi. Badala yake watume fedha watakazobaki nazo kwa Waukraine ili kuwasaidia wakati huu wa majira ya baridi kali. **DW**

## Marufuku yatolewa wanawake kufanya kazi mashirika ya kiraia

**KABUL,** Afghanistan

TALBAN imepiga marufuku wanawake kufanya kazi katika mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), agizo lililolaaniwa na Umoja wa Mataifa (UN), ikisema kuwa hatua hiyo inakiuka haki za kimsingi.

Ilielezwa kuwa watawala hao wa Kiislamu walihalalisha hatua hiyo kwa kusema wafanyakazi wa kike wa NGOs wamevunja kanuni za mavazi kwa kutovaa hijabu.

Aidha, ilibainishwa kuwa amri hiyo ilijiri siku chache baada ya wanafunzi wa kike kupigwa marufuku kutoka vyuo vikuu. Wafanyakazi wa kike wa NGOs wa Afghanistan wanaofanya kazi kama wachumaji wakuu katika kaya zao waliiambia BBC juu ya woga wao na kutokuwa na uwezo.

Mmoja wa wakazi hao ambaye jina lake lilihifadhiwa, alihoji kwamba ikiwa hawezi kwenda kwenye kazi yake, ni nani anayeweza kutengemeza familia yake.

Mwanamke wwingine alitilia shaka maadili hayo ya Taliban, akisema sasa atapata shida kulipa bili zake na kulisha watoto wake. Huku wengine wakidai kuwa ulimwengu unawatazama na haufanyi chochote.

Kwa mujibu wa taarifa ya BBC, iliyochapishwa jana agizo hilo lilitolewa na Wizara ya Uchumi kwa NGOs za kitaifa na kimataifa, huku ikitishia kufuta leseni ya shirika lolote ambalo halikufuata maelekezo hayo.

Hatua hiyo imezusha hasira za kimataifa, huku Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, akisema ana wasiwasi mkubwa, akiongeza kuwa hali hiyo itavuruga usaidizi muhimu na wa kuokoa maisha kwa mamilioni.

"Wanawake ni muhimu katika shughuli za kibinadamu duniani kote. Uamuzi huu unaweza kuwa mbaya kwa watu wa Afghanistan," alisema Blinken. **BBC**



Papa Francis akihutubia katika misa ya mkesha wa Krismasi jana jijini Vatican. **PICHA: DW**

## Saba wauawa makabiliano ya kikabila

**KHARTOUM,** Sudan

MAPIGANO ya kikabila huko Darfur yamesababisha vifo vya takriban watu saba katika eneo hilo la magharibi mwa Sudan lililoharibiwa na vita, shirika rasmi la Suna liliripoti Jumamosi.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki iliyopita na Shirika la Suna, na kuongeza kuwa mapigano baina ya makabila yalizuka Desemba 21, mwaka huu, katika kitongoji karibu na Nyala, mji mkuu wa jimbo la Darfur Kusini.

Shirika hilo lilisema wanaume waliopanda ngamia na pikipiki walianzisha mashambulizi katika kijiji cha Amouri, na kwamba cha mwisho kilichomwa moto na kusababisha watu kuuawa.

Shirika la serikali la Sudan lilisema tangu wakati huo, mtu mwingine aliuawa na mzozo huo umeenea katika vijiji jirani, ambavyo vingi vimeteketezwa kwa kiasi na biashara zao kuporwa.

Chanzo cha matibabu kimethibitisha kwa shirika la habari la AFP kuwasili kwa watu 20 waliojeruhiwa kwa risasi katika hospitali ya Nyala.

Wataalamu wanasema, tangu mapinduzi ya mkuu wa jeshi Jenerali Abdel Fattah al-Burhane Oktoba 2021, migogoro ya kikabila imelipuka kutokana na ombwe la usalama lililotokana na mapinduzi hayo.

UN ilisema vita vya 2003 huko Darfur kati ya utawala wa Waarabu wengi wa Omar al-Bashir na waasi kutoka makabila madogo wanaolaani ubaguzi vilisababisha vifo vya watu 300,000 na milioni 2.5 kuyahama makazi yao, hasa katika miaka ya kwanza ya vita.

Bashir, ambaye sasa yuko gerezani, alitimuliwa mwaka 2019 kwa shinikizo kutoka mitaani na jeshi.

Darfur inasalia kutikiswa mara kwa mara na ghasia, hasa kati ya makabila hasimu. Machafuko ambayo husababishwa, miongoni mwa mambo mengine, na migogoro ya kimaeneo na ugumu wa kupata maji. **RFI**

# HABARI PICHA



Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la KKKT Usharika wa Muheza, mkoani Tanga, John Ndimbo, akiwatakia mkono wa heri ya Krismasi waumini wa kanisa hilo jana katika ibada ya Krismasi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Askofu Mkuu wa Kanisa la Azania Front, Alex Malasusa (kushoto), akisalimiana na mmoja wa waumini wa kanisa hilo, Zekeho Mapunda, baada ya kumalizika kwa Ibada ya Sikukuu ya Krismasi iliyofanyika kanisani hapo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Askofu Mkuu wa Kanisa la The Free Pentecostal Church of Tanzania (FPCT}, Stivie Mulenga, akiwabariki waumini wa kanisa hilo jijini Tanga jana baada ya kumalizika kwa ibada ya Sikukuu ya Krismasi. **PICHA: OSCAR ASSENGA**



Mkazi wa Kijiji cha Genge Stesheni wilayani Muheza mkoani Tanga aliyefahamika kwa jina la Mama Kijazi, jana akiandaa chakula kwa ajili ya sikukuu ya Krismasi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Waumini wa Kanisa la St Alban, wakiwa katika Ibada ya Sikukuu ya Krismasi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

BURUDANI

# Asha Baraka awajia juu wanaomtongoza DM

**Na Mwandishi Wetu**

MMILIKI wa Bendi ya African Stars 'Twanga Pepeta', amefichua kuwa kuna baadhi ya wanaume kazi yao ni kukaa kwenye simu kutwa nzima na kutongoza wanawake kwenye DM.

Akasema kuna baadhi ya wanaume hasa vijana wamekuwa hawana shughuli nyingine, kazi yao kuingia kwenye DM na kujaribu bahati yao kwa kutongoza wanawake.

"Ningekuwa kiongozi mkubwa siku moja au mbili ningewanyoosha, ningewazimia data siku nzima ili watu wafanye kazi waache umbea na mambo mengine yasiyo na maana wanawake wakapike, waache kuunguza mboga, kuna wanaume nao hawafanyi shughuli yoyote kazi ni simu, simu na wao.

"Mwanaume mmoja utakuta anatongoza wanawake hata 50 DM, yaani kakaa tu kazi yake ndiyo hiyo, hajui huyu ni mama yake mzazi, ana umri gani, yaani kazi ni kutafuta bahati, watu hawafanyi kazi wanatafuta bahati. Si tunaona, jamani mtuache wengine watu wazima sisi, tuna watoto na wajukuu, kwani siku hizi hata hizo data siwashi mara kwa mara, sisomi ujumbe fanyeni kazi vijana acheni mambo hayo," alionya.





# SHILOLE AGEUKIA WANAWAKE KUHESHIMU WAUME ZAO

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa Bongo Fleva na mwigizaji, Shilole, amewataka wanawake wenzake kuwaheshimu waume zao akisema hilo ndilo linalodumisha upendo na kusababisha waishi kwa muda mrefu.

Alisema kuwa mwanamke hata kama uwe na pesa nyingi, lakini kama huna heshima kwa mume wako ni kazi bure tu.

"Mimi hata kama nataka mume wangu aniletee kitu kiko karibu natanguliza neno samahani. Neno samahani linabeba kila kitu. Mwenzangu anafurahi kwa sababu anaona namwonyesha upendo sana. Namwambia tu mume wangu samahani, anainuka anakuja namwambia nataka hiki, analeta.

"Ni hivi lazima umuheshimu mume haijalishi awe mdogo au mkubwa, kitu kikubwa ambacho wanaume wanahitaji kutoka kwa wake zao ni heshima, mwanamke hata kama uwe na pesa kiasi gani kama huna heshima ni changamoto tu," alisema msanii huyo ambaye ameolewa na mumewe aitwaye Rommy.

# *Sofi amtega Harmonize*

**Na Mwandishi Wetu**


MREMBO Sofi aliyecheza kama 'video queen' kwenye ngoma ya msanii Harmonize iitwayo 'Amelowa', amesema atamtangaza rasmi mpenzi wake mpya 2023, huku akikanusha kuwa yeye ndiye sababu ya penzi na msanii huyo na Kajala kuvunjika.

Sofi amesema mashabiki wa muziki wakae tayari kuona mahusiano yake kama atakuwa Harmonize au mwingine basi watajua baada ya mwezi huu kumalizika.

"Siku ikifika kujua mahusiano yangu mtajua kama Harmonize kama ni mwingine, subirini mwaka uishe na hiyo kuniambia kuwa mimi nimesababisha uhusiano uvunjike waelewe mimi ni msichana, siyo kila wanachokiona ni rahisi hivyo, waache kuunganisha vitu, mimi niko bize nina mambo yangu kwa hiyo waniache," alisema.

Akasema licha ya kwamba kuna watu wanamzushia kutoka na msanii huyo, lakini wajiulize kwani ana ubaya gani?

"Siyo kweli lakini mimi nina ubaya gani? Mimi namshauri tu Harmonize atafute mrembo mkali kama mimi, tupo, majimbo yako wazi kaka yangu usiogope, " alisema msanii huyo.



# SAIDO AWAAHIDI MAKUBWA SIMBA IKIIVAA KMC KIRUMBA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba ikishuka Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza leo kucheza dhidi ya KMC kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara raundi ya 18, mchezaji mpya wa miamba hiyo ya Kariakoo, aliyetambulishwa juzi akitokea Geita Gold, amewaahidi wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuwa atacheza na kujituma kuliko hata alipokuwa akichezea timu zingine kwa sababu amejiunga na klabu ambao inapendwa na familia yake.

**Akizungumza kwa mara ya kwanza jijini Mwanza baada ya kutua kwa ajili ya kujiunga na wenzake, Saido amesema amepata bahati kubwa kujiunga na Simba kwa sababu familia yake, baba yake mzazi, mtoto wake mkubwa na mkewe, wote ni mashabiki wa kutupwa wa Simba na walimpigia simu baada ya kutambulishwa rasmi.**

"Kwingine kote nilikopita ilikuwa ni masuala ya kazi tu, lakini sasa imekwenda kwenye timu ambayo familia yangu inaipenda zaidi.

"Sisi kwetu ni mashabiki wa Simba, baba yangu hata kama alikuwa anavaa jezi za timu nyingine ni kwa sababu tu ya kumsapoti mtoto wake yuko kazini, yeye ni Simba tangu mimi niko mdogo nakuta yeye ni mnyama, mtoto wangu mkubwa ni mpenzi wa kutupwa na klabu hii baada ya kutangazwa tu, alinipigia simu yeye na mama yake, kwa sababu nimekwenda kwenye timu wanayoipenda.

"Yaani nimekwenda kwenye timu ya familia na kwa hiyo nitajitahidi kucheza kwa uwezo wangu wote kuliko hata nilikopita kwa sababu mafanikio yangu na furaha hayaendi kwa wanachama na mashabiki tu, bali hata familia yangu," alisema Saido aliyesajiliwa kwa mkataba wa mwaka mmoja na nusu.

Kuhusu habari zinazosemwa kuwa amekuwa mchezaji asiye na nidhamu, alisema kuna watu wachache walitengeneza propaganda hizo kwa ajili ya kumchafua, lakini anashangaa kule kule ambako walisema hayo, walikuwa wakimpigia simu.

"Unajua kuna msemo nimeukuta hapa Tanzania, unasema ukitaka kumpiga mbwa, basi mpe jina baya, sitoliongelea hilo suala, haina haja na nimekaa kimya miezi sita, kama ningekuwa mtovu wa nidhamu nisingepigiwa simu na watu wa huko huko, mengine namuachia Mungu atanisafisha na wanajua, walitaka kuniharibia tu jina, kuna mambo mengi sana mabaya lakini nikiongea itaonekana labda kwa sababu nimekuja huku.

Iweje nionekane mtovu wa nidhamu siku chache tu kabla ya mkataba wangu kumalizika?" Alisema mchezaji huyo wa kimataifa wa Burundi huku akieleza kwamba alikuwa na ndoto ya kucheza timu moja na Clatous Chama.

Wakati huo huo, Simba ambayo inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 38, leo itakuwa ugenini dhidi ya KMC ambayo imeipeleka mechi hiyo jijini Mwanza.

Kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa Septemba 7, mwaka huu, timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2 na baada ya hapo, ndipo Simba ilipomchukua kocha Juma Mgunda, hivyo itakuwa ni mara yake ya kwanza kucheza na timu hiyo.

Akizungumzia mechi hiyo, alisema maandalizi yote yamekamilika japokuwa hatokuwa na kinara wao wa mabao, Mosses Phiri.

"Maandalizi yamekamilika tuko tayari kupambana na KMC, hatutokuwa na Phiri alipata maumivu kwenye mechi dhidi ya Kagera Sugar, lakini niwatoe shaka Wanasimba kuwa anaendelea vizuri, Simba ina wachezaji wengi na ndiyo maana alipotoka siku ile aliingia mwingine," alisema Mgunda.

Kuhusu Saido, Mgunda alisema kwa sasa ni mchezaji wa Simba amekuja kuitumikia, wamempokea vizuri na wanatambua ni mmoja wa wachezaji mahiri nchini.

## MAZOEZI KWANZA...



Baadhi ya wanachama wa Klabu ya Wajumbe wa Mungu Jogging, wakifanya mazoezi ya viungo chini ya mwalimu wao, Joseph Kisaka (kushoto), kwenye eneo la wazi la Kanisa la Waadventisha Wasabato Mbezi Luis, Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

## Opa wa Simba Queens kinara

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA tegemeo wa timu ya soka ya wanawake ya Simba (Simba Queens), Opa Clement, pamoja na mchezaji wa Fountain Gate Girls, Cynthia Musungu, wanaongoza kwa ufungaji wa mabao kwenye ligi hiyo kila mmoja akicheka na nyavu mara matatu mpaka sasa, ikiwa kwenye raundi ya tatu.

Wakati mchezaji huyo wa Simba Queens akiwa na idadi hiyo ya mabao, timu yake inakamata nafasi ya nne ikiwa na pointi nne na mabao sita ya kufunga, wakati Cynthia timu yake ikiongoza ligi na pointi zake tisa, ikicheza mechi zote tatu na kushinda.

Kwa mujibu wa takwimu za ligi hiyo ya wanawake, wachezaji hao wanafuatiwa na wenzao wa Simba Queens, Yanga Princes, Alliance Girls na JKT Queens wenye mabao mawili kila mmoja.

Wachezaji hao ni raia wawili wa kigeni, Mkongomani Pambani Kuzoya wa Simba Queens, Mnigeria Chioma Wogu wa Yanga Princess, pamoja na Watanzania wawili, Winfrida Charles wa Alliance Girls na Stumai Abdallah wa JKT Queens.

Wakati Fountain Gate Princess ikiongoza ligi, Alliance Girls inashika nafasi ya pili ikiwa na pointi saba, JKT Queens ikiwa kwenye nafasi ya tatu ikilingana kila kitu na timu hiyo iliyoshika nafasi ya pili, zikiwa zimetofautishwa tu alfabeti, huku Simba Queens ikishika nafasi ya nne.

Yanga Princess inashika nafasi ya tano kwa kuwa na pointi nne kama Simba, lakini imezidiwa bao moja la kufunga, ikiwa na mabao matano, Baobab iko kwenye nafasi ya sita pia kwa pointi nne, lakini imefunga mabao matatu tu.

Timu ya Ceasiaa Queens ina pointi tatu kwenye nafasi ya saba, nafasi ya nane ikishikiliwa na Amani Queens, Mkwawa Queens nafasi ya tisa na The Tigers Queens inashika mkia, zote hizo zikiwa na pointi moja moja.

# Mwakinyo, Mmarekani sasa kuzichapa Januari

**Na Saada Akida**

KAMISHNA wa Idara ya Michezo Visiwani Zanzibar, Ameir Mohamed Makame, amesema wametoa muongozo kwa promota wa Hassan Mwakinyo kusogeza pambano lake mbele alilotarajia kucheza visiwani humo, hadi watakapomaliza mchakato wa usajili wa katiba na kupata viongozi wa muda.

Amesema badala ya pambano hilo kuchezwa Desema 30, mwaka huu, sasa litafanyika mwishoni mwa Januari, mwakani ikiwa ni baada ya kumaliza kwa mchakato huo wa uchaguzi.

Kauli hiyo imetolewa na kiongozi huyo jana wakati akizungumza na Nipashe lililotaka kujua maandalizi ya pambano hilo, ambalo Mwakinyo anatarajiwa kuvaana na bondia Mmarekani Peter Dodson katika Uwanja wa Mao Tse Tung, kuwania mkanda wa WBC International Super Welterweight.

Kamishna Ameir, alisema baada ya kuona maneno mengi katika mitandao ya kijamii, walifanya kikao na promota wa pambano hilo, Shomari Kimbau na kumtaka asogeze mbele pambano hilo hadi Januari.

Alisema Zanzibar wameruhusiwa kucheza ngumi, lakini wanatakiwa kupata viongozi ambao watasimamia mchezo huo kwa muda kwa kuandaa kanuni na sheria za ngumi za kulipwa na ridhaa.

"Hatujakataa pambano la Mwakinyo kufanyika hapa Zanzibar, bali tunatakiwa kufuata utaratibu kwanza, tumeongea na promota wake kumweleza anatakiwa kusogeza mbele hadi Januari mwakani kwa sababu sasa hivi tuko katika kusajili mchezo huo pamoja na kupata uongozi wa muda utakaosimamia ngumi," alisema Kamishna huyo.

Alisema wamekuwa wakifuata taratibu za usajili wa mchezo huo kulingana na mafunzo na maelekezo waliyopata Baraza la Michezo la Taifa la Tanzania (BMT), ili kuhakikisha hawafanyi makosa na kufungiwa.

"Tunahitaji Mwakinyo na promota wake wawe watulivu, Visiwani na Bara ni wamoja, lakini katika sekta ya michezo huwa haziingiliani, tumewataka wasogeze mbele badala ya Desemba mwaka huu hilo pambano lichezwe Januari mwishoni kwa sababu tutakuwa tumekamilisha kanuni, sheria na kupata uongozi wa muda wa kusimamia mchezo wa ngumi," alisema Ameir.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### VILLA KUMUUZA COUTINHO

Aston Villa iko tayari kumuuza kiungo wa Brazil, Philippe Coutinho, 30, katika dirisha la usajili la Januari, ikiwa ni baada ya mwaka mmoja tangu mchezaji huyo atue Villa Park. ***(Football Insider)***

### EMERY HAMTAKI MARTINEZ

KOCHA Aston Villa, Unai Emery, hataki kufanya kazi na kipa Muargentina Emiliano Martinez, 30, na yupo tayari kumtoa mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwezi ujao. ***(Fichajes - in Spanish)***

### LIVER BASI KWA BELLINGHAM

Liverpool itanyosha mikono juu katika mpango wa kujaribu kumsajili kiungo wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham, 19, kwa sababu wanaamini kuwezesha dili hilo kukamilika kwa mchezaji huyo kuna utata mwingi. ***(AS - in Spanish)***

### SOYUNCU KUTUA ATLETICO

Atletico Madrid imekubaliana malipo binafsi na Caglar Soyuncu, 26, hadi mwaka 2027 - na beki huyo wa kati wa Leicester City na Uturuki atajiunga na miamba hiyo mapema Januari, ingawa hata hivyo atakuwa mchezaji huru Julai mwakani. ***(Nicolo Schira)***

### RICE ANUKIA CHELSEA

CHELSEA ipo katika nafasi nzuri zaidi ya kumsajili kiungo wa England, Declan Rice, 23, ambaye anaingia miezi 18 ya mwisho katika mkataba wake na West Ham. ***(Athletic)***

### GVARDIOL KUWA GHALI ZAIDI

CHELSEA itamfanya mlinzi wa kati wa RB Leipzig, Josko Gvardiol, 20, kuwa beki ghali zaidi katika historia ya soka kama itafanikiwa kumsajili mchezaji huyo katika dirisha la Januari. ***(Football London)***

### SKRINIAR LULU LIVER, SPURS

LIVERPOOL na Tottenham ni miongoni mwa Klabu za Ligi Kuu England zipo tayari kuwasilisha ofa ya kumsajili beki wa Inter Milan, Milan Skriniar, 27. ***(Teamtalk)***

### SUAREZ KUTIMKIA BRAZIL

MSHAMBULIAJI wa Uruguay, Luis Suarez, 35, anajiandaa kujiunga na Gremio ya Brazil kwa mkataba wa miaka miwili. ***(Cesar Luis Merlo, via Mail)***

### SPURS KWA GIL, SARR

TOTTENHAM imeonyesha kuvutiwa na winga wa Hispania, Bryan Gil, 21, na kiungo wa Senegal, Pape Sarr, 20, wakati huu dirisha dogo la usajili likikaribia kufunguliwa. ***(Relevo, via Mail)***

### ALONSO KUJIFUNGA BARCA

BEKI wa kushoto wa Hispania, Marcos Alonso, 31, yupo mbioni kusaini mkataba mpya na Barcelona baada ya kutua kwa uhamisho huru akitokea Chelsea majira ya joto. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### OTAMENDI AMULIKWA BENFICA

BENFICA imetoa ofa mpya ya miaka miwili kwa beki wa kati wa Argentina, Nicolas Otamendi, 34, ambaye atamaliza mkataba wake majira ya joto yajayo huku akiwa anataka kuendelea kucheza Ulaya, lakini mazungumzo hayajaendelea. ***(Fabrizio Romano)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI, PSG WAKUBALIANA KUSAINI MKATABA MPYA

**PARIS,** Ufaransa

NAHODHA wa Argentina, Lionel Messi, amefikia "makubaliano kimsingi" ya kuongeza mkataba na Paris St-Germain, kwa mujibu wa mchambuzi wa BBC Sport, Guillem Balague.

**Messi, 35, ambaye ameiongoza Argentina kutwaa Kombe la Dunia nchini Qatar, atamaliza mkataba na miamba hiyo ya Ufaransa ifikapo Juni mwakani.**

Mapema wiki hii, Rais wa Barcelona, Joan Laporta, alisema "angependa" Messi arudi kwa miamba hiyo ya Hispania klabu ambayo aliitumikia kwa miaka 21.

Lakini Balague alisema Barca bado haijamfuata Messi kuhusu kumtaka kurejea.

Atasaini mkataba wa mwaka mmoja ukiwa na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja zaidi na makubaliano yamekuja baada ya mazungumzo ya miezi minne kati ya Mkurugenzi wa Soka wa PSG, Luis Campos na babaye Messi, Jorge.

**● ● ● Kivitendo wote wamekubaliana, si kwamba hataki kurudi Barcelona, ila...**

Hilo likifuatiwa na mazungumzo muhimu walipokutana Doha na Mwenyekiti wa PSG, Nasser Al-Khelaifi.

"Kivitendo wote wamekubaliana na PSG," alisema mchambuzi huyo wa soka la Ulaya, Balague. "Barcelona bado haijamfuata yeye baba yake kutoa ofa yoyote.

"Hivyo si kwamba Messi hataki kurudi Barcelona. Hajaulizwa swali.

"Messi ni mwenye furaha kwa yote na atakaporejea kutoka mapumzikoni makubaliano yataendelea kwa kasi.

"Maisha yake Paris yapo katika uwiano mzuri, furaha, kila mmoja analifurahia hilo na kuna uwezekano wa kutwaa tena Ligi ya Mabingwa Ulaya. Jumlisha kwamba itamsaidia kuwa mwania tuzo ya Ballon d'Or kwa mara nyingine."

Mshindi huyo mara saba wa tuzo ya Ballon d'Or, alitangazwa Mchezaji Bora wa Fainali za Kombe la Dunia wakati Argentina ikitwaa ubingwa huo baada ya kushinda kwa mikwaju ya penalti 4-2 dhidi ya Ufaransa.

Baada ya kuondoka Barcelona 2021, Messi alisaini mkataba wa miaka miwili kama mchezaji huru, ukiwa na kipengele cha kuongeza mwaka wa tatu.

Hadi sasa amecheza mechi 53 za Ligue 1, akiifungia mabao 23 kwenye mashindano yote.

Raia huyo wa Argentina tayari sasa ametwaa Kombe la Dunia mara moja, Ligi ya Mabingwa mara nne, Copa America mara moja, La Liga mara 10 akiwa na Barcelona na ubingwa wa Ligue mara moja akiwa na PSG.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,059,8

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 28,29 NA 30 DISEMBA 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/12/22 | 17:00 | Troyes vs Nantes | 2.34 | 3.48 | 2.78 |
| 02. 28/12/22 | 17:00 | Istanbulspor vs Kasimpasa | 2.78 | 3.53 | 2.31 |
| 03. 28/12/22 | 22:00 | Portimonense vs Casa Pia Atletico | 2.36 | 3.14 | 2.99 |
| 04. 28/12/22 | 22:45 | St Johnstone vs Hearts | 2.85 | 3.15 | 2.46 |
| 05. 28/12/22 | 22:45 | Livingston vs St Mirren | 2.32 | 3.38 | 2.88 |
| 06. 29/12/22 | 17:00 | Giresunspor vs Gaziantep BB | 2.47 | 3.34 | 2.69 |
| 07. 29/12/22 | 19:00 | Girona vs Rayo Vallecano | 2.36 | 3.15 | 3.05 |
| 08. 29/12/22 | 21:15 | Betis vs Athletic Bilbao | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 09. 29/12/22 | 22:00 | GD Estoril vs Boavista | 2.27 | 3.13 | 3.18 |
| 10. 29/12/22 | 22:45 | Blackburn vs Middlesbrough | 2.53 | 3.22 | 2.68 |
| 11. 29/12/22 | 22:45 | Wigan vs Sunderland | 2.69 | 3.19 | 2.54 |
| 12. 29/12/22 | 23:00 | Nice vs Lens | 3.14 | 2.89 | 2.43 |
| 13. 30/12/22 | 11:45 | Western United vs Brisbane Roar | 2.49 | 3.24 | 2.74 |

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa


SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LEWANDOWSKI ATAKA KUCHEZA NA MESSI



**BARCELONA,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Robert Lewandowski, amesema itakuwa ni 'ndoto' kwake kucheza pamoja na nyota wa Paris Saint-Germain (PSG), Lionel Messi.

Lewandowski alijiunga na Barcelona majira ya joto akitokea Bayern Munich kwa ada ya kiasi cha Euro milioni 45, ambazo zitaongezeka hadi kufikia Euro milioni 50. Nyota huyo wa Poland ametoa msaada mkubwa hapo Camp Nou tangu atue na amekuwa sababu ya 'Blaugrana' hao kuongoza kwenye msimamo wa La Liga.

Amekuwa silaha muhimu katika kuiongoza safu ya ushambuliaji ya Blaugrana hao, akifunga mabao 18 na kutoa pasi za mwisho 'assists' nnne kwenye mechi 19 alizoichezea katika mashindano yote. Hata hivyo nyota huyo wa kimataifa wa Poland amefunguka kwamba angependa siku moja kucheza pamoja na nyota wa PSG, Messi.

Ameliambia gazeti la Mundo Deportivo: "Si juu yangu mimi. Bila shaka, tunaona kwamba kwa sasa anacheza zaidi kama kiungo mchezeshaji, pengine anafunga mabao machache na kutoa pasi zaidi kwa wachezaji wenzake, lakini bado anafunga."

"Lakini ukimlinganisha na wakati mwingine, kwa sasa ni mchezaji ambaye kila mshambuliaji angependa kucheza naye."

Messi aliondoka Barcelona na kujiunga na PSG katika majira ya joto mwaka 2021 baada ya 'Blaugrana' hao kushindwa kuongeza mkataba wake.

Mshindi huyo mara saba wa tuzo ya Ballon d'Or hakuwa na mwanzo mzuri katika msimu wake wa kwanza Parc des Princes kwa kiwango chake cha kawaida. Hata hivyo amerejesha kiwango chake msimu huu, akiwa tayari amefunga mabao 12 na kutoa pasi za mwisho 'assists' 14 katika mechi 19 alizocheza hadi sasa.



# Conte kupumzisha wa Qatar leo

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Tottenham, Antonio Conte, amependekeza kuwa atachagua wachezaji ambao hawakujumuishwa katika vikosi vyao vya timu ya taifa kwenye Kombe la Dunia nchini Qatar wakati wa mechi yao ya leo ya Ligi Kuu England dhidi ya Brentford.

Ligi Kuu England inarejea leo Jumatatu, ikiwa ni siku nane tu baada ya mechi ya fainali ya Kombe la Dunia kupigwa Qatar.

Conte tayari amesema wachezaji ambao walijumuishwa mchezo wa fainali, Wafaransa Hugo Lloris na Muargentina Cristian Romero hawatawafaa 'Nyuki' hao.

"Ukweli sina furaha," Conte alisema. "Kwa upande mmoja, unafuraha kwa sababu kwa ajili ya klabu yangu, Tottenham, kuwa na wachezaji 12 Kombe la Dunia inamaana kwamba tuko katika njia sahihi kujaribu kuwa washindani na kujaribu kushinda kitu fulani.

"Lakini ni kawaida kwan ba unapokuwa na wacheza wengi wanacheza michuan kama hii, zaidi wakati w msimu [wa ligi], kama sas si rahisi kwa sababu hali y kimwili haiwi katika kiwang cha juu. "Ni vigumu kuwap muda mrefu wa kupumzik na kwa uhakika kwa kuw na wachezaji ambao h wakucheza Kombe la Dun tulifanya kazi kwa wiki nn kwa sasa wapo katika ha nzuri kimwili.

344,733/-

# GWAMBINA YAENDELEA KUSUSIA CHAMPIONSHIP

Na Adam Fungamwango

TIMU ya Gwambina FC, imeendelea kususia mechi za Championship licha ya kukatwa pointi 15 na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye kikao chake cha Desemba 13, mwaka huu.

**Gwambina imerudia tena kile kile ilichokifanya dhidi ya African Sports, na Mbuni FC, baada ya juzi kushindwa kufika kwenye Uwanja wa CCM Gairo, Morogoro kucheza dhidi ya Fountain Gate.**

Hiyo ni mechi ya tatu kwa timu hiyo iliyocheza Ligi Kuu msimu wa 2020/21 kushindwa kufika uwanjani na huenda ikaadhibiwa tena kwa mara nyingine.

Desemba 4, timu hiyo ilinyang'anywa pointi 15 kwa kushindwa kutokea kwenye uwanja wa Nyamagana Mwanza, ikiwa mwenyeji wa timu ya African Sports kitu ambacho kilisababisha kamati hiyo kuipoka pointi hizo.

Hata baada ya adhabu hiyo, bado timu hiyo ilishindwa tena kutokea kwenye uwanja huo huo wa Nyamagana kucheza dhidi ya Mbuni Desemba 19, kabla ya juzi kurudia tena.

Kwa sasa inasubiriwa tena kamati hiyo itakuja na uamuzi gani mwingine kulingana na kanuni za Ligi ya Championship.

Ligi hiyo iliendelea tena juzi, African Sports ikiifunga Mashujaa mabao 2-1 Uwanja wa Mkwakwani, Tanga, Mbuni ikipata kibano cha bao 1-0 dhidi ya Kitayosce, Shekh Amri Abeid, Arusha, JKT Tanzania ikifumua Pamba bao 1-0 katika Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam, Ndanda ikilazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Pan Africans, Nangwanda Sijaona, Mtwara, Biashara United ikiloa nyumbani kwa bao 1-0 dhidi ya Mbeya Kwanza, Uwanja wa Karume, Musoma, Mara na Copco ikichapwa bao 1-0 nyumbani dhidi ya KenGold.

**TUSIFU...**



Waimbaji wa Kwaya wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT), Jimbo Kuu la Dar es Salaam, wakiimba wakati wa Ibada ya Sikukuu ya Krismasi jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Simba yamfunga Inonga hadi 2025

INATOKA UKURASA 32

inaelekea ukingoni.

Inonga ndiye beki bora wa Ligi Kuu nchini msimu uliopita, huku akiwa beki bora Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kabla ya kutua nchini.

Wakati mkataba wake ukielekea ukingoni amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa zikiwamo Yanga na Azam FC.

Simba ilimsajili mchezaji huyo Agosti mwaka jana akitokea Klabu ya DC Motema Pembe ya Jamhuri ya Kidemkorasi ya Congo.

Beki huyo aliingia moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza na si kuwa tegemeo tu, bali pia kipenzi cha wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

## *Fei Toto, Yanga kwazidi kunoga*

INATOKA UKURASA 32

ume cha taratibu kwa maslahi ya soka la Tanzania.

"Sheria kwa mchezaji yeyote ambaye anataka kuvunja mkataba na klabu anatakiwa aitaarifu klabu na asubirie majibu ya klabu na kukaa meza moja kwa sababu klabu inamsajili mchezaji ikiwa na malengo yake.

"Ikimbukwe kuwa mchezaji ni mfanyakazi na si mwanachama wa klabu hiyo, yawapo makubaliano ya pande zote mbili mezani ili kutolea maamuzi kwani Fei ana haki zake na klabu ina haki yake.

"Ukiangalia vifungu vya Fifa vinaruhusu mchezaji kuvunja mkataba ama kununua mkataba wake wakati huo kukiwa na aina ya vipengele ambavyo vinaweza kumruhusu mchezaji kuweza kuvunja ama kununua mkataba wake.

"Mkataba ni siri ya mtoaji na mpokeaji, hivyo kama kuna kipengele cha kuvunja mkataba kinatakiwa kiwekwe bayana kwenye mkataba kuona mchezaji anatakiwa afanye nini pale anapotaka kuvunja mkataba na kama hakipo itakuwa ni mapungufu, hivyo kunaweza kuwa na utata," alisema na kuongeza;

"Kipengele chochote cha kuvunja mkataba kinatakiwa kiwe na maelezo na sababu zake kama ambavyo Fifa wameelekeza katika kifungu cha 15, mchezaji anaweza kuvunja mkataba kutokana na sababu tofauti na wakati huo huo imeweka wazi kuwa mchezaji hawezi kuingia klabuni na kuomba kuondoka ndani ya miezi mitatu sheria hairuhusu.

"Naona ni vema busara itumike kwa ama mchezaji kuweza kukaa mezani pamoja kuzungumza ili kumaliza suala hili kwa maslahi ya mchezaji, klabu na soka la Tanzania kwa upana wake," alisema Kisoki.



# SUPA JACKPOT
# MECHI WIKI HII
## BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/12/22 | 18:00 | Everton FC vs Wolverhampton Wanderers | 2.31 | 3.25 | 3.05 |
| 02. 26/12/22 | 18:00 | Bristol City vs West Bromwich Albion | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 03. 26/12/22 | 18:00 | Rotherham United vs Stoke City | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 04. 26/12/22 | 18:00 | Burton Albion vs Lincoln City | 2.37 | 3.30 | 2.90 |
| 05. 26/12/22 | 18:00 | Cambridge United vs Shrewsbury Town | 2.60 | 3.25 | 2.65 |
| 06. 26/12/22 | 18:00 | Charlton Athletic vs Peterborough United | 2.70 | 3.30 | 2.55 |
| 07. 26/12/22 | 18:00 | Exeter City vs Portsmouth FC | 2.65 | 3.35 | 2.55 |
| 08. 26/12/22 | 19:00 | FC Annecy vs AS Saint-Etienne | 2.90 | 3.25 | 2.37 |
| 09. 26/12/22 | 20:00 | Goztepe Izmir vs BB Bodrumspor | 2.50 | 3.35 | 2.65 |
| 10. 26/12/22 | 20:15 | Cardiff City vs Queens Park Rangers | 2.48 | 3.20 | 2.80 |
| 11. 26/12/22 | 22:45 | Royal Charleroi SC vs RSC Anderlecht | 2.80 | 3.45 | 2.38 |
| 12. 26/12/22 | 22:45 | Luton Town vs Norwich City | 2.75 | 3.30 | 2.50 |
| 13. 26/12/22 | 23:00 | Valenciennes FC vs Amiens SC | 2.46 | 3.20 | 2.85 |
| 14. 26/12/22 | 23:00 | Pau FC vs Paris FC | 2.95 | 3.20 | 2.38 |
| 15. 26/12/22 | 23:00 | Quevilly-Rouen Metropole vs Grenoble Foot | 2.46 | 3.05 | 2.95 |
| 16. 26/12/22 | 23:00 | SC Bastia vs SM Caen | 3.05 | 3.10 | 2.38 |
| 17. 26/12/22 | 23:00 | Nimes Olympique vs EA Guingamp | 2.90 | 3.25 | 2.40 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATATU - 26/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 3713 | Brescia vs Palermo | 2.18 | 3.03 | 3.43 |
| 15:00 | 2207 | Watford vs Millwall | 2.03 | 3.22 | 3.61 |
| 15:30 | 1240 | Sunderland vs Blackburn | 2.30 | 3.17 | 3.03 |
| 15:30 | 4829 | Brugge vs OH Leuven | 1.42 | 4.77 | 6.16 |
| 15:30 | 5570 | Brentford vs Tottenham | 3.62 | 3.57 | 1.91 |
| 17:00 | 1757 | Como vs Cittadella | 2.34 | 3.02 | 3.12 |
| 17:00 | 1810 | Glentoran Belfast vs Linfield Belfast | 2.33 | 3.16 | 2.82 |
| 17:00 | 2860 | Benevento vs Perugia | 1.95 | 3.18 | 3.97 |
| 17:00 | 2947 | Ascoli vs Reggina | 2.82 | 2.92 | 2.62 |
| 17:00 | 3024 | Spal vs Pisa | 2.58 | 3.07 | 2.73 |
| 17:00 | 4047 | Venezia vs Parma | 2.82 | 3.12 | 2.47 |
| 17:00 | 4843 | Kerala Blasters FC vs Delhi Dynamos FC | 1.99 | 3.45 | 3.25 |
| 17:00 | 5515 | Altinordu vs Caykur Rizespor | 3.84 | 3.60 | 1.78 |
| 17:00 | 5521 | Cagliari vs Cosenza | 1.49 | 4.05 | 6.13 |
| 17:30 | 3556 | Caernarfon Town vs Bala Town | 4.65 | 4.17 | 1.55 |
| 17:30 | 4427 | The New Saints vs Airbus UK Broughton | 1.01 | 13.70 | 39.16 |
| 18:00 | 1009 | AFC Wimbledon vs Newport | 2.43 | 3.12 | 2.87 |
| 18:00 | 1015 | Charlton vs Peterborough | 2.62 | 3.31 | 2.52 |
| 18:00 | 1038 | Crystal Palace vs Fulham | 2.02 | 3.43 | 3.43 |
| 18:00 | 1154 | Union Saint Gilloise vs Oostende | 1.34 | 5.19 | 7.39 |
| 18:00 | 1411 | Everton vs Wolverhampton | 2.26 | 3.16 | 3.11 |
| 18:00 | 1416 | Bristol City vs West Bromwich | 2.96 | 3.21 | 2.32 |
| 18:00 | 1459 | Fleetwood Town vs Sheffield Wed | 4.38 | 3.53 | 1.76 |
| 18:00 | 1545 | Accrington vs Barnsley | 3.27 | 3.27 | 2.13 |
| 18:00 | 1557 | Middlesbrough vs Wigan | 1.64 | 3.62 | 5.16 |
| 18:00 | 1755 | Sheffield Utd vs Coventry | 1.67 | 3.70 | 4.74 |
| 18:00 | 1947 | Exeter vs Portsmouth | 2.57 | 3.31 | 2.57 |
| 18:00 | 2832 | MK Dons vs Forest Green | 1.83 | 3.48 | 4.07 |
| 18:00 | 2870 | Southampton vs Brighton | 3.22 | 3.42 | 2.09 |
| 18:00 | 2905 | Preston vs Huddersfield | 1.86 | 3.32 | 4.17 |
| 18:00 | 2936 | Rotherham vs Stoke City | 2.97 | 3.26 | 2.29 |
| 18:00 | 3381 | Hull City vs Blackpool | 2.07 | 3.27 | 3.42 |
| 18:00 | 5466 | Leicester vs Newcastle | 3.12 | 3.37 | 2.16 |
| 18:15 | 1813 | KMC vs Simba | 5.16 | 3.66 | 1.26 |
| 19:00 | 4424 | Annecy FC vs St Etienne | 2.97 | 3.22 | 2.31 |
| 20:00 | 1907 | Goeztepe vs Bodrumspor | 2.87 | 3.35 | 2.21 |
| 20:00 | 5587 | Frosinone vs Ternana | 1.78 | 3.46 | 4.35 |
| 20:15 | 1862 | Cardiff vs QPR | 2.37 | 3.22 | 2.88 |
| 20:15 | 2670 | Kortrijk vs Racing Genk | 5.97 | 4.67 | 1.44 |
| 20:30 | 2709 | Aston Villa vs Liverpool | 4.26 | 3.87 | 1.70 |
| 21:00 | 4956 | Le Havre vs Bordeaux | 2.22 | 3.08 | 3.28 |
| 21:30 | 4962 | Maccabi Netanya vs Maccabi Haifa | 4.88 | 4.00 | 1.55 |
| 22:30 | 1516 | Bari vs Genoa | 3.07 | 2.97 | 2.40 |
| 22:45 | 3765 | Luton Town vs Norwich City | 2.58 | 3.22 | 2.62 |
| 22:45 | 5897 | Charleroi vs Anderlecht | 2.93 | 3.47 | 2.24 |
| 23:00 | 1629 | Arsenal vs West Ham | 1.54 | 3.94 | 5.63 |
| 23:00 | 3140 | Metz vs Niort | 1.74 | 3.48 | 4.58 |
| 23:00 | 3735 | Bastia vs Caen | 2.81 | 3.00 | 2.56 |
| 23:00 | 4033 | Valenciennes vs Amiens | 2.51 | 3.01 | 2.86 |
| 23:00 | 4964 | Nimes vs Guingamp | 2.87 | 3.22 | 2.38 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Desemba 26, 2022
Nipashe



Messi, PSG wakubaliana kusaini mkataba

UKURASA 29

# FEI TOTO, YANGA KWAZIDI KUNOGA

## ●●● Azam FC yafunguka, Sputanza nayo yaingilia kati, yasema...

**Saada Akida na Hadija Mngwai**

WAKATI Azam FC, kwa mara ya kwanza ikiibuka na kuweka wazi kuhusu suala la kuhusishwa na kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto', Chama cha Wachezaji wa Mpira wa Miguu Tanzania (Sputanza), kimeingilia kati na kutoa kauli yake.

**Kumekuwa na mvutano mkubwa kuhusu suala la Fei Toto kuandika barua kwa uongozi wa klabu ya kuvunja mkataba kwa kutumia kipengele kinachomtaka kulipa Sh. milioni 100 na mishahara ya miezi mitatu endapo atataka kuvunja mkataba wake, jambo ambalo amelitekeleza.**

Fei Toto, ambaye anahusishwa kuivutia Azam FC, katika barua yake hiyo, alieleza kuambatanisha na risiti za benki kwa kuilipa Yanga jumla ya Sh. milioni 112, ikiwa ni pamoja na mishahara ya miezi mitatu, lakini mara moja klabu hiyo ilitoa taarifa kuwa imezirejesha fedha hizo kwa mchezaji huku ikimtaka kuheshimu mkataba wake.

Lakini jana uongozi wa Azam FC, umefunguku kuhusu kiungo kuhusishwa na Fei Toto, baada ya kusema hakuna timu ambayo haitahitaji huduma yake, ingawa kwa sasa wao wanaheshimu mkataba wa kiungo huyo na klabu yake ya sasa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema kulingana na uwezo na ubora wa kiungo huyo hakuna timu ambayo haitahitaji kupata huduma yake, lakini wao wanaheshimu mkataba wa nyota huyo na Yanga.

Alisema kwa sasa suala la usajili wanafuata mapendekezo ya benchi la ufundi kulingana na mahitaji ya kikosi chao kwa ajili ya kujiimarisha zaidi kuwania ubingwa.

"Hatuwezi kumzungumzia mchezaji wa timu nyingine kwa sababu tunaheshimu mikataba, suala la usajili liko mikononi mwa benchi la ufundi na tutafuata mapendekezo yao ya aina ya wachezaji tutakaowasajili, lakini kikubwa ni kufanya mapinduzi makubwa kuboresha kikosi chetu," alisema Popat.

Wakati hali ikiwa hivyo kwa Azam, Yanga na Fei Toto, Mwenyekiti wa Sputanza, Mussa Kisoki, amesema ni vyema kuwapo na makubaliano kwa pande zote mbili hata kama kutakuwa na uvunjifu wa taratibu kwa mchezaji kutaka kuondoka kiny-

INAENDELEA UK. 31



# Simba yamfunga Inonga hadi 2025

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imetangaza kumwongeza mkataba beki wake raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Henock Inonga, kwa kumsainisha mkataba mwingine wa miaka miwili ambao utamweka hapo hadi mwaka 2025.

Simba imeonekana kumuwahi beki huyo wa kati ambaye uwezo wake kwenye mechi za Ligi Kuu na za kimataifa umeonekana kuzivutia klabu nyingi ndani na nje ya nchi, huku mkataba wa awali ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwaka huu.

Katika taarifa yao jana, klabu ya Simba imesema imemwongeza mkataba baada ya kufikia makubaliano, huku ikikanusha kuwa alikuwa mbioni kuondoka.

"Mkataba wa awali wa Inonga ulikuwa unamalizika mwishoni mwa msimu huu na leo (jana), ameongezewa mkataba wa miaka mingine miwili na atasalia klabuni hapo hadi 2025.

"Kumekuwa na taarifa kutoka vyanzo mbalimbali vya habari kuwa yu mbioni kuondoka jambo ambalo halina ukweli wowote," ilieleza.

Katika dirisha hili dogo la usajili uongozi wa klabu ya Simba umeeleza unadhamiria kuboresha kikosi kwa kuongeza wachezaji wapya kama ilivyopendekezwa na benchi la ufundi, sanjari na kuwaongeza mikataba wachezaji wote ambao

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >